# Nipashe

Jumatano Februari 27, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579852

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mwili wazikwa baada ya miezi tisa

UKURASA 21




UKURASA 13

# NI MAJONZI

**RUGE** afariki dunia nchini Afrika Kusini, Rais Magufuli amlilia... *Endelea ukurasa wa 2*



## Mume alilima Bunge barua kuhusu mkewe

UKURASA 2

## Wakopaji benki watahadharishwa

UK 2






**MICHEZO** YANGA YAITANGAZIA HATARI ALLIANCE FC UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Tahadhari wakopaji benki

**Na Waandishi Wetu**

IDADI ya nyumba, magari na viwanja vinavyopigwa mnada kutokana na wamiliki kushindwa kurejesha mikopo, imeendelea kuongezeka nchini.

Kutokana na changamoto hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe, amewataka wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuwa makini katika ukopaji, kuweka malengo mahususi wakati wa kukopa fedha na kuepuka kukurupuka kukopa kwenye taasisi za fedha.

Alisema tahadhari hiyo itawasaidia kuepuka fedheha ya kupigwa mnada kwa mali zao walizoziweka dhamana ya mikopo.

Nipashe ilizungumza na mkurugenzi huyo wiki iliyopita jijini Dar es Salaam kuhusu kushamiri kwa matangazo ya minada ya mali za wakopaji kwenye benki na taasisi nyinginezo za fedha kwenye vyombo vya habari nchini.

Itembe alisema mteja kukumbwa na hali ya mbaya ya kiuchumi hadi kushindwa kulipa madeni inasababishwa na mambo mengi, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa nidhamu ya usimamizi wa biashara.

Alisema inawezekana biashara kwenda vibaya tofauti na matarajio, lakini pia benki husika huenda imeshindwa kumsimamia vyema mteja husika na kumshauri kitaalamu jinsi ya kulipa deni lake.

"Kwa mazingira ya sasa, biashara inahitaji kufanywa katika uhalisia, hakuna nafasi ya kufanya ujanjaujanja, kila kitu kinapaswa kulipiwa ipasavyo," alisema.

Itembe aliongeza: "Kwa wale waliokuwa wanategemea kupenya katika njia zao ili kupata faida kubwa, hawawezi kufanikiwa, udhibiti wa serikali upo imara."

Aliongeza kuwa wakopaji wazuri waliojipanga wapo na wanaendelea kunufaika kwa mikopo kwa kuwa wanalipa kwa wakati na wanafanya biashara zao kwa njia halali na hawapati usumbufu.

MINADA MIPYA

Wiki iliyopita, Benki ya Access ilitangaza kupiga mnada mali za wateja wake, zikiwamo nyumba na viwanja zilizoko katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam kutokana na wateja kushindwa kutimiza matakwa ya mkataba wa mkopo.

Ilisema jumla ya wateja 15 waliokopa kupitia benki hiyo, mali zao zitaanza kupigwa mnada kuanzia Machi 6 hadi 21, mwaka huu katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Katika tangazo lililotolewa na kampuni

INAENDELEA UK 8



Mbunge wa Chama cha Wananchi (CUF), Jimbo la Malindi Zanzibar, Ally Saleh, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu athari za mgogoro unaoendelea ndani ya chama hicho. Kulia ni Mbunge wa Mchinga, Hamidu Bobali. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mume alilima Bunge barua kuhusu mkewe

**Na Romana Mallya**

WAKILI maarufu jijini Dar es Salaam, Moses Kaluwa, ameliandikia Bunge barua kutaka aliyekuwa mke wake, Bonnah Kaluwa, ambaye ni Mbunge wa Segerea (CCM), kutokutumia jina lake.

Hatua hiyo inatokana na mwanasheria huyo na mkewe kuachana mwaka jana kwa talaka kwa kile kilichodaiwa kuwa kukosekana kwa uaminifu ndani ya ndoa yao.

Hata hivyo, mbunge huyo amekiri kuwa mume wake huyo wa zamani ameliandikia Bunge barua ya kumtaka abadili jina lake baada ya kuachana rasmi kwa talaka.

Awali, katika mitandao ya kijamii kulizagaa taarifa ambayo ilieleza kuwa mume wa mbunge huyo ametuma barua ofisi ya Bunge ikimtaka Bonnah aache kutumia majina yake ya mwisho baada ya kupeana talaka.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa mbunge huyo ametakiwa kubadili majina kwenye nyaraka rasmi na mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram, website na Twitter) ambako utekelezaji umeshafanyika.

Taarifa hiyo ikimnukuu mtu wa karibu wa mwanamume huyo, ikidai kuwa kuachana kwao kumetokana na tuhuma za muda mrefu kuwa baada ya Bonnah kuwa mbunge, amekuwa si mwaminifu kwenye ndoa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mwaka jana wakati wa vikao vya Bunge, mume wake alifanya safari ya ghafla kwenye makazi ya mbunge huyo na kumkuta akiwa na mwanamume mwingine.

Taarifa hiyo ilizidi kudai kuwa juhudi za kuwapatanisha zilifanyika na kushindikana

INAENDELEA UK 8

# Uangalizi maalum waliotibiwa kimeta

**Na Godfrey Mushi, SAME**

SERIKALI imesema hadi sasa hakuna idadi ya vifo vilivyoongezeka kutokana na kuibuka kwa ugonjwa hatari wa kimeta ambao unadaiwa kuua watu watano na ng'ombe 21, wilayani Same, mkoani Kilimanjaro.

Vilevile, imesema imeweka uangalizi maalum kwa watu wanne waliotibiwa baada ya kuugua maradhi yanayohusishwa na virusi hivyo hatari.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema jana kuwa, hatua zilizochukuliwa kudhibiti ugonjwa huo usiendelee kuenea ni pamoja na wataalamu wa afya na serikali kuweka uangalizi maalum kwa watu wanne waliopona na kuruhusiwa kutoka hospitalini.

"Tulichofanya ni kuweka uangalizi maalum kwa watu wanne ambao hata hivyo wamesharuhusiwa kutoka hospitalini, naamanisha walikokuwa wamelazwa," alisema.

Katika Wilaya ya Rombo ambayo inapakana na nchi jirani ya Kenya, serikali imeanza jana kampeni maalum ya kusisitiza wananchi kufukia mizoga ya wanyama waliokufa au kuwateketeza kwa moto wa mafuta ya dizeli chafu.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, alisema operesheni hiyo ya kuzuia kusienee ugonjwa huo wala kuingia katika eneo lao, imeanza jana chini ya maofisa mifugo na madaktari wa mifugo.

"Leo (jana) muda huu nimetokea maeneo ya jirani na mpakani kuongeza nguvu ya kutoa elimu kwa wananchi, nimewaambia ni marufuku kula nyama ambayo haijachinjwa wala kuthibitishwa na daktari na mizoga yote ichomwe moto," alieleza Hokororo. Juzi, Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Prof. Philimon Wambura, aliwatahadharisha wananchi kuhusu tishio la kuwapo kwa nyama ya ng'ombe yenye ugonjwa.

Aliwataka wawe makini kwa kuhakikisha wananunua kitoweo hicho kwenye maeneo yaliyosajiliwa nchini.

Vyombo vya habari viliripoti juzi kuwa kutokea kwa vifo vya watu watano na ng'ombe 21 kutokana na ugonjwa huo wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro. Prof. Marwa alisema ugonjwa huo ni hatari kwa kuwa ng'ombe anakufa ghafla akiwa amenona, hivyo watu wenye tamaa ya fedha wanaweza kuuza nyama hiyo pasipo kujali athari zitakazojitokeza.

"Hatari inaweza kuwakabili zaidi wale wanaopenda kula nyama zisizokaguliwa ambazo haziuzwi kwenye maeneo rasmi yaliyosajiliwa, sasa wabadilike, waache kununua vichochoroni kuepuka shida zinazosababishwa na ugonjwa huo hatari," alisema.

# Tahadhari wakopaji benki

Na Waandishi Wetu

IDADI ya nyumba, magari na viwanja vinavyopigwa mnada kutokana na wamiliki kushindwa kurejesha mikopo, imeendelea kuongezeka nchini.

Kutokana na changamoto hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Charles Itembe, amewataka wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuwa makini katika ukopaji, kuweka malengo mahususi wakati wa kukopa fedha na kuepuka kukurupuka kukopa kwenye taasisi za fedha.

Alisema tahadhari hiyo itawasaidia kuepuka fedheha ya kupigwa mnada kwa mali zao walizoziweka dhamana ya mikopo.

Nipashe ilizungumza na mkurugenzi huyo wiki iliyopita jijini Dar es Salaam kuhusu kushamiri kwa matangazo ya minada ya mali za wakopaji kwenye benki na taasisi nyinginezo za fedha kwenye vyombo vya habari nchini.

Itembe alisema mteja kukumbwa na hali ya mbaya ya kiuchumi hadi kushindwa kulipa madeni inasababishwa na mambo mengi, ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa nidhamu ya usimamizi wa biashara.

Alisema inawezekana biashara kwenda vibaya tofauti na matarajio, lakini pia benki husika huenda imeshindwa kumsimamia vyema mteja husika na kumshauri kitaalamu jinsi ya kulipa deni lake.

"Kwa mazingira ya sasa, biashara inahitaji kufanywa katika uhalisia, hakuna nafasi ya kufanya ujanjaujanja, kila kitu kinapaswa kulipiwa ipasavyo," alisema.

Itembe aliongeza: "Kwa wale waliokuwa wanategemea kupenya katika njia zao ili kupata faida kubwa, hawawezi kufanikiwa, udhibiti wa serikali upo imara."

Aliongeza kuwa wakopaji wazuri walio-jipanga wapo na wanaendelea kunufaika kwa mikopo kwa kuwa wanalipa kwa wakati na wanafanya biashara zao kwa njia halali na hawapati usumbufu.

MINADA MIPYA

Wiki iliyopita, Benki ya Access ilitangaza kupiga mnada mali za wateja wake, zikiwamo nyumba na viwanja zilizoko katika maeneo ya Jiji la Dar es Salaam kutokana na wateja kushindwa kutimiza matakwa ya mkataba wa mkopo.

Ilisema jumla ya wateja 15 waliokopa kupitia benki hiyo, mali zao zitaanza kupigwa mnada kuanzia Machi 6 hadi 21, mwaka huu katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Katika tangazo lililotolewa na kampuni

INAENDELEA UK 8



Mbunge wa Chama cha Wananchi (CUF), Jimbo la Malindi Zanzibar, Ally Saleh, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu athari za mgogoro unaoendelea ndani ya chama hicho. Kulia ni Mbunge wa Mchinga, Hamidu Bobali. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mume alilima Bunge barua kuhusu mkewe

Na Romana Mallya

WAKILI maarufu jijini Dar es Salaam, Moses Kaluwa, ameliandikia Bunge barua kutaka aliyekuwa mke wake, Bonnah Kaluwa, ambaye ni Mbunge wa Segerea (CCM), kutokutumia jina lake.

Hatua hiyo inatokana na mwanasheria huyo na mkewe kuachana mwaka jana kwa talaka kwa kile kilichodaiwa kuwa kukosekana kwa uaminifu ndani ya ndoa yao.

Hata hivyo, mbunge huyo amekiri kuwa mume wake huyo wa zamani ameliandikia Bunge barua ya kumtaka abadili jina lake baada ya kuachana rasmi kwa talaka.

Awali, katika mitandao ya kijamii kulizagaa taarifa ambayo ilieleza kuwa mume wa mbunge huyo ametuma barua ofisi ya Bunge ikimtaka Bonnah aache kutumia majina yake ya mwisho baada ya kupeana talaka.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa mbunge huyo ametakiwa kubadili majina kwenye nyaraka rasmi na mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram, website na Twitter) ambako utekelezaji umeshafanyika.

Taarifa hiyo ikimnukuu mtu wa karibu wa mwanamume huyo, ikidai kuwa kuachana kwao kumetokana na tuhuma za muda mrefu kuwa baada ya Bonnah kuwa mbunge, amekuwa si mwaminifu kwenye ndoa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mwaka jana wakati wa vikao vya Bunge, mume wake alifanya safari ya ghafla kwenye makazi ya mbunge huyo na kumkuta akiwa na mwanamume mwingine. Taarifa hiyo ilizidi kudai kuwa juhudi za kuwapatanisha zilifanyika na kushindikana

INAENDELEA UK 8

# NI MAJONZI

Na Mwandishi Wetu

MKURUGENZI wa Vipindi wa Clouds Media Group (CMG), Ruge Mutahaba, amefariki dunia jana usiku nchini Afrika Kusini alikokuwa akipatiwa matibabu.

Ruge alipelekwa nchini humo mwishoni mwa mwaka jana kutokana na kusumbuliwa na matatizo ya figo.

Kutokana na kifo hicho, Rais John Magufuli, jana usiku alituma salamu za rambirambi kwa familia yake na kusema amepoteza kijana wake muhimu katika tasnia ya habari nchini.

Rais Magufuli katika rambirambi hiyo aliyoitoa pia kupitia kwenye mtandao wa kijamii wa 'Tweeter' alisema: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha kijana wangu Ruge Mutahaba. Daima nitakukumbuka kwa mchango wako mkubwa katika tasnia ya habari, burudani, na juhudi za kujenga fikra za maendeleo kwa vijana. Poleni wanafamilia, ndugu, jamaa na marafiki. Mungu amweke mahali pema. Amina."

Taarifa za msiba Ruge zilitangazwa rasmi na Millad Ayo katika kipindi cha Amplifier kikiendelea Clouds jana usiku.

Wakati Ayo akiendelea na kipindi hicho ndipo taarifa za msiba huo zilipokuja na kulazimika kutangaza kuwa, kipindi hicho kimeishia wakati huo baada ya kupata taarifa za msiba huo.

"Tunaomba radhi kwa sasa kipindi cha Amplifier kwa leo kitaishia hapo tumepata taarifa za kushtusha ambazo zimemjeruhi kila mmoja humu ndani na kubadilisha hali ya hewa," alisema na kuongeza:

"Mmoja wa waasisi na Mkurugenzi wa wa vipindi na uzalishaji Clouds Media Group Ruge Mtahaba ametutoka leo (jana) huko Afrika Kusini alikokuwa amekwenda kwa matibabu, mioyo yetu imejeruhiwa sana tutaendelea kuwapa taarifa zote, pumzika kwa amani" alimaliza.

Mmoja wa wafanyakazi wa Clouds, Hassan Ngoma, aliiambia Nipashe kwamba msiba wa Ruge uko Mikocheni karibu na shule ya Fezza nyumbani kwa baba yake mzazi.

Alisema taarifa walizozipata ni kuwa Ruge alifariki jana saa moja jioni.

Jumatatu iliyopita, mdogo wa Ruge, Mbaki Mutahaba, akihojiwa kwenye kipindi cha 360 cha Clouds TV, alisema Ruge alianza kuumwa mwaka jana.

Akizungumza kwenye kipindi hicho Mbaki alisema gharama za matibabu Afrika Kusini ni kubwa kwa siku inaweza kufikia Sh. milioni tano hadi sita na hadi wakati huo zaidi ya Sh. milioni 600 zilikuwa zimeshatumika.

Kuhusu historia ya kuumwa kwake, Mbaki alisema Ruge alianza kuumwa mwaka jana na kabla ya kupelekwa Afrika Kusini alilazwa Hospitali ya Kairuki, Mikocheni jijini Dar es Salaam na baadaye alipelekwa nchini India.

"Jopo la madaktari kutoka hosptali ya Kairuki na Muhimbili wakasema apelekwe Afrika Kusini kwa sababu ni karibu ila matibabu ya huko yana gharama kubwa," alisema na kuongeza;

"Ila msaada ni kubwa ukianza na mheshimiwa Rais Magufuli, alishatoa msaada mkubwa sana na anakuwa akipiga simu kujua hali yake kila wakati ila kule gharama ya matibabu ni kubwa kwa siku inaweza kufika milioni tano mpaka sita." alibainisha.

Mbaki alisema mwezi Aprili mwaka jana, alianza kuumwa bila kujua ni tatizo la figo na mwezi uliofuata ndipo alipopata majibu ya hospitali kuwa anasumbuliwa na figo.

Alisema baada ya kufika India, walimwambia figo zake hazina ulazima wa kubadilishwa.

"India hakukaa muda mrefu alirejea Tanzania na kuendelea na matibabu, lakini baadaye hali ikabadilika mara ya pili akalazwa Kairuki, kutokana na hali yake ilivyokuwa ilipofika mwezi Septemba mwaka jana madaktari wakapendekeza apelekwe Afrika Kusini," alisema.

Alisema baada ya kufika Afrika Kusini mambo mengine yakaibuka yanayohusiana na figo, hivyo madaktari wakawa wanatibu siyo tu figo na mengine.

"Katika kipindi chote alichokwenda tangu Septemba hadi sasa madaktari wamekuwa wakitibu siyo tu masuala ya figo wakati mwingine presha," alisema.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (wa pili kulia), akizungumza na Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Phaustine Kasike (katikati), wakati alipotembelea ofisini kwake kwa mazungumzo juu ya kuangalia njia bora za kudumisha uhusiano baina ya NBC na jeshi hilo. Wengine ni maofisa wa NBC na Magereza. **MPIGAPICHA WETU**

# JPM akutana na bingwa wa upasuaji ubongo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, jana amekutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Idara ya Upasuaji wa Ubongo na Mishipa kutoka Hospitali ya Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Peking (PUIH), iliyopo Beijing nchini China Prof. Zhao Yuanil, ambaye ameongoza timu ya wataalamu wanaoshirikiana na Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu ya Muhimbili (MOI).

Taarifa iliyotolea na Kurugenzi wa Mawasiliano Ikulu jana, ilisema mazungumzo hayo yamefanyika Ikulu jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Balozi wa China hapa nchini Wang Ke, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Lawrence Mseru.

INAENDELEA UK 8

# Jafo aagiza ujenzi wa barabara zenye viwango

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameziagiza halmashauri za jiji la Dar es Salaam kujenga barabara zenye viwango vya hali ya juu, kufuatia kukamilika kwa maabara za kisasa za kupima udongo pamoja na malighafi katika wilaya tatu kupitia Mradi wa Uboreshaji wa jiji la Dar es Salaam (DMDP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Maabara hizo zipo ndani ya majengo ya kisasa yaliyojengwa katika wilaya za Kinondoni, Ilala na Temeke ambazo zitawezesha halmashauri kupima malighafi za kujenga barabara zenye viwango vinavyokubalika.

Jafo alitoa maagizo hayo juzi, wakati akizindua maabara hiyo wilayani Kinondoni na wawakilishi wa Benki ya Dunia ambao wamefadhili miradi ya DMDP kwa Sh. bilioni 660 katika ziara ya kuikagua jijini, Dar es Salaam.

Alisema uwapo wa maabara hizo utawezesha kupimwa kwa udongo wa kujengea barabara kama zinakidhi vigezo ili kusiwapo na zitakazojengwa chini ya viwango.

"Kutokana na maabara hii, sitaki kuona barabara zikijengwa chini ya kiwango, ninachotaka miradi ya DMDP ya barabara idumu kwa miaka 20 sio miwili kwa kuwa sitaraji kuona zikiwa na mashimo mashimo," Jafo alisema.

Aliwataka wasimamizi wa barabara kuwa makini na watu wa maabara wapatapo malighafi za barabara kama hazina ubora watoe taarifa.

"Kama maabara ipo na malighafi zinazoenda kujengewa barabara hazina ubora watawajibika na hatua zitachukuliwa dhidi yao," alisema.

Alisema matokeo makubwa ya ujenzi wa barabara, utengenezaji wa maeneo ya uhifadhi wa taka ngumu, utengenezaji wa mifereji ni matokeo ya ushirikiano baina ya benki hiyo na serikali.

Pia alisema mafanikio hayo ni kutokana na timu nzuri ya benki hiyo kufanya kazi vizuri na serikali kwa sababu barabara nyingi zinapitika, masoko yameimarika likiwamo la Kijichi, Daraja la Tuangoma na maeneo mengine.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa benki hiyo, Sameh Wahba, alisema benki hiyo itahakikisha inaendelea kushirikiana na serikali kwa sababu wameshuhudia miradi inayotekelezwa na kuridhishwa na maendeleo yake.

FSSP Field Support Services Project - Tanzania

**CONSULTANCY POSITION**

**PUBLIC FINANCIAL MANAGEMENT TECHNICAL SPECIALIST**

**TO SUPPORT GLOBAL AFFAIRS CANADA**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy services as **Public Financial Management (PFM) Technical Specialist** to support Global Affairs Canada under the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The Public Financial Management Technical Specialist will provide PFM-related strategic advice and technical support related to Canada's policies, strategies and programming in Tanzania.

**Candidates will be evaluated based on the following key qualifications and experience:**

i. Master's degree in a relevant field such as public administration (including accounting or auditing), economics, business administration, accounting, development economics, macroeconomics or public finance
ii. Minimum of five (5) years of experience in public policy, economic policy, or public financial management, at least three (3) years of which should have been gained in Tanzania
iii. Minimum of five (5) years of experience in international development policy and programs, preferably in a bilateral or multilateral development institution
iv. Minimum of five (5) years of experience with public sector accounting, financial management, and budget reviews
v. Knowledge of public sector policy priorities and processes in Tanzania, including planning, management and budgeting of public sector resources

In addition to the key qualifications above, the incumbent should also demonstrate the following skills and competencies:

- Advanced professional proficiency in English;
- General professional proficiency in Kiswahili;

Training or experience in gender-responsive, gender-based, and/or gender-sensitive public financial management would be a strong asset.

Interested candidates should obtain a detailed description of these services by sending request email to procurement@fssptz.org specifying in the requests as follows: "**Consultancy position for Public Financial Management Technical Specialist.**"

Requests for further information will be received up to three working days prior to the **last submission date, 8 March, 2019.**

**Any request received later than that may not be responded to.**

**FSSP Manager**

21507080Z

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SEKTA YA HIFADHI YA JAMII

SSRA

**TAARIFA KWA UMMA**

**KUHAMA OFISI**

Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) inawatangazia wadau wake wote na umma kwa ujumla kuwa, kuanzia tarehe 01 Machi, 2019 Ofisi za Kanda zilizokuwa katika Jengo la Alfa, Kitalu Namba 25, Barabara ya Bagamoyo sasa **zitahamia** katika Jengo la GEPF, Ghorofa ya 8, Kitalu Na. 37 Regent Estate, Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam.

Hivyo kuanzia tarehe 01 Machi 2019 huduma zote za Mamlaka zitapatikana katika jengo la GEPF, Ghorofa ya 8.

Aidha Mamlaka inapenda kufahamisha Umma kwamba Ofisi za Makao Makuu yake zinatakuwa katika , Jengo la NHIF, Barabara ya Makulu, Dodoma.

Mamlaka inaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza

**Imetolewa Na;**

**Kitengo cha Mawasiliano,**
**Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA),**
**Jengo la NHIF, Barabara ya Makulu, NCC Mtaa wa Link,**
**S.L.P.2929,**
**Dodoma.**
**Simu: +255 743 753204**
**Barua pepe: info@ssra.go.tz**
**Tovuti: www.ssra.go.tz**

21508280Z

# Watano mahakamani kwa kuingiza kemikali bila kibali

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA watano wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashtaka manne likiwamo la kuingiza nchini kemikali bila kuwa na vibali.

Washtakiwa hao ni, Jumanne Mazunde, Godfrey Kiwelu, Nsia Mbonika, Chankan Mhina na Joseph Omollo.

Walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Wankyo Simon, alidai kuwa washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka manne ya kuingiza nchini kemikali mbalimbali kutokea jijini Nairobi nchini Kenya.

Katika shtaka la kwanza linalomkabili Mazunde, anadaiwa kuwa Septemba 13, 2017, eneo la Ubungo aliingiza nchini kemikali aina ya Potassium Hydrochloride 12.5 kilogramu, Amonium Chloride kutoka Nairobi Kenya.

Shtaka la pili, Mbonika na Mhina walidaiwa Septemba 13, 2017, Ubungo jijini Dar es Salaam waliingiza kemikali aina ya Potassium Hydrochloride kilogramu 7.5 na Sodium Hydrogen Carbonate kilogramu 29 kutoka Nairobi, Kenya bila kuwa na kibali.

Shtaka la tatu, Mhina alidaiwa kuwa Septemba 13, 2017 Ubungo, jijini Dar es Salaam, aliingiza kemikali aina ya Polyester Resin kilogramu 100 bila kuwa na kibali cha mamlaka husika.

Katika shtaka la nne, Omollo alidaiwa kuwa Septemba 13, 2017, eneo la Ubungo aliingiza kemikali hizo kutokea Nairobi, Kenya bila kuwa na kibali.

Washtakiwa waliposomewa mashtaka yao walikana.

Upande was Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wake bado haujakamilika.

Hakimu aliwataka washtakiwa kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 10 kila mmoja.

Washtakiwa watatu kati ya hao wameachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ambao ni Kiwelu, Mbonika na Mhina.

Kesi hiyo itatajwa Machi 12, mwaka huu.



Mkazi wa jiji akiosha makopo ya rangi kwenye mtaro wa maji ya mvua, katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni uchafuzi wa mazingira. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# WB yafurahishwa miradi ya maendeleo

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais John Magufuli, Benki ya Dunia imeshatoa zaidi ya shilingi trilioni mbili kwa ajili ya kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

Fedha hizo zimetumika katika miradi mitatu ya uendelezaji wa majiji, miji na Jiji la Dar es Salaam katika ujenzi wa miundombinu ya barabara, vituo vya mabasi, madampo na masoko katika mikoa mbalimbali nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliyaeleza hayo jana alipoongozana na maofisa kutoka Benki ya Dunia, walipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa Miradi ya Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam inayotekelezwa na wizara yake katika manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke.

Akiwa katika Manispaa ya Temeke alipotembelea ujenzi wa kituo cha afya cha Buza, Jafo alisema Benki ya Dunia imesaidia utekelezaji wa miradi itakayowezesha kukuza uchumi wa wananchi na maendeleo ya taifa.

"Namshukuru Rais John Magufuli katika kipindi cha uongozi wake tangu aingie madarakani, Benki ya Dunia imeshafadhili miradi mbalimbali ya maendeleo kwa gharama za Dola za Marekani bilioni moja, sawa na zaidi ya shilingi trilioni mbili, ambazo zimesaidia kutatua changamoto mbalimbali za maendeleo katika nchi yetu," Jafo alisema.

Alisema utekelezaji wa miradi hiyo unasimamiwa kwa karibu na Rais Magufuli katika kuhakikisha anatekeleza ahadi alizotoa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na lengo ni kuwaletea wananchi maendeleo.

Alitaja baadhi ya majiji na miji ambayo miradi hiyo inatekelezwa kuwa ni Tanga, Arusha, Ujiji, Mikindani na Mbeya zinakojengwa barabara za kisasa.

Maeneo mengine alitaja kuwa ni katika miji na manispaa katika mikoa mbalimbali nchini kwa kujenga stendi za mabasi na miundombinu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Akikagua barabara ya Tuangoma iliyoko Mbagala wilayani humo, alimwagiza Mkuu wa Wilaya hiyo, Felix Lyaniva, kuhakikisha anasimamia usafi katika miradi hiyo, baada ya kuona takataka zimeshaanza kutupwa katika mitaro.

"Naagiza Mkuu wa Wilaya uhakikishe unaanzisha kampeni maalum ya kudhibiti uchafu katika miradi hii kwa sababu nimeshaona takataka zimeanza kutupwa kwenye mitaro hii. Suala la ujenzi ni jambo moja na jambo la msingi zaidi ni kuilinda miradi hii isiharibiwe," Jafo alisema.

Akiwa katika maeneo ya Mbagala Kuu na Kijichi, eneo la Tuangoma na Kijichi, Jafo alisema maeneo hayo yamebadilika kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na miaka mitatu iliyopita kufuatia ujenzi wa miradi inayoendelea.

Alisema changamoto iliyokuwa katika mto Mzinga ya kuwagawa wakazi wa maeneo hayo imetatuliwa baada ya kujengwa daraja la kisasa pamoja na soko la kisasa Mbagala na Kijichi yatakayowezesha wakazi wake kupata bidhaa na soko la Kijichi litaufanya kuongeza thamani ya maeneo hayo.

Kwa upande wake, Meya wa Manispaa ya Temeke, Abdallah Chaurembo, alisema wametekeleza vizuri miradi yote na kumwomba Rais Magufuli kuwapatia fedha za miradi mingine zaidi.

Alisema miradi hiyo inatekelezwa katika kata 13, lakini kuna kata nyingine ambazo zinahitaji fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Kwa upande wake Mwakilishi wa Benki ya Dunia kutoka Makao Makuu nchini Marekani, Sameh Wahba, alisema ameridhishwa na utekelezaji wa miradi hiyo katika Wilaya ya Temeke, inayotekelezwa kwa kushirikiana na viongozi wa serikali na watendaji wengine.

Pia alisema kwa kazi nzuri aliyoshuhudia hayupo katika nafasi ya kuahidi kuwa, Benki ya Dunia itaendelea kufadhili miradi mingine isipokuwa inaweza kuwa sehemu ya kuendelea kupata ufadhili.

## ATE yahamasisha wanawake kushika nafasi za juu

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE), kimesema iko haja ya kuwainua na kuwawezesha wanawake katika ngazi mbalimbali ili waweze kushika nafasi za juu katika uongozi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya kundi la nne la programu ya mwanamke wa wakati ujao (Female Future) inayolenga kuboresha ufanisi kwa wafanyakazi wa kike.

Alisema ushahidi unaonyesha kuwa wakipatiwa mafunzo na kuwezeshwa wanaweza kufanya mambo makubwa ikilinganishwa na wanaume.

Aidha, alisema mfumo dume ndio uliosababisha kuonekana mwanamke hawezi kupatiwa madaraka na ndio maana katika ngazi mbalimbali wanawake wanaachwa nyuma.

"Mfumo dume unamfanya mwanamke atizamwe kwa mambo mawili yaani akishindwa hatachukuliwa kama ni mfanyakazi matokeo yake atachukuliwa ameshindwa kwa vile ni mwanamke," alisema.

Dk. Mlimuka alisema kuna mtazamo hasi katika jamii kuhusu wanawake jambo ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi. Aidha, alitoa wito kwa waajiri kutoa fursa kwa wanawake na wasione kama mafunzo hayo ni gharama kubwa bali waone kama wanawekeza.

Alisema kuwekeza kwa mwanamke ni kuongeza tija kubwa na jambo hilo halina ubishi hata kwenye bodi ambazo zina wanawake zimefanya vizuri zaidi kuliko zenye wanaume.

"Kwa mwanamke anaongeza tija yaani ana uwezo wa kufanya vitu zaidi ya kimoja, mimi ni mwanaume na katika taasisi yangu wanawake ni wengi na wanafanya vizuri," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Chuo cha Biashara Esami, Prof. Michael Munkumba, alisema kuwapo kwa mafunzo hayo ni sehemu ya kumuinua mwanamke sehemu ya kazi.

Alisema ukiangalia kwenye bodi mbalimbali na hata za nje ya nchi zinaongozwa na wanaume na ndio maana wameamua kuja na mafunzo hayo ili mwanamke anapopata nafasi afanye vizuri zaidi.

"Tafiti imeonyesha kuwa ukiweka mwanamke mmoja kwenye bodi ufanisi wake unaongezeka kwa zaidi ya asilimia 50 na hii programu iko katika nchi tatu na itasaidia kupunguza umaskini maana hawa wanawake watakuwa wanasimamia majukumu yao vizuri hasa katika masuala ya uchumi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Benki ya Maendeleo (TIB), Frank Nyabundege, alisema huwa wanawaleta wafanyakazi wao kwa kuwa wanaamini mwanamke ni chachu katika maendeleo hasa wanapokuwa katika uongozi huwa wanafanya vizuri. Programu ya Mwanamke wa Wakati Ujao (Female Future) ilizinduliwa Februari, mwaka 2016 na Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu na inalenga zaidi kuongeza ufanisi kwa waajiriwa wa kike wenye kiu ya kukuza ufanisi kazini ili kuendeleza vipaji kwa waajiriwa wa kike mahali pa kazi.

Pamoja na mambo mengine, ilibainishwa kuwa wahusika watanda mtandao wa kubadilishana uzoefu katika fani mbalimbali.

## HABARI KITAIFA

# Kiama chaja kampuni za uwakala wa forodha

**Na Salome Kitomari**

CHAMA cha Mawakala wa Forodha Tanzania (Taffa), kimesema kinashangazwa na hatua ya msimamizi na mshindani wa biashara kuwa sehemu ya biashara anayosimamia.

Akizungumza na Nipashe jana, kuhusu utekelezaji wa sheria iliyoanzisha Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (Tasac), Makamu wa Rais wa Taffa, Edward Urio, alisema inashangaza kuona anayetunga kanuni na sheria, naye anafanya biashara husika.

Alisema wakiwa wadau, wamepokea kwa mikono miwili, lakini wameshangazwa na tangazo la hivi karibuni la Tasac kuanza kuondosha na kusafirisha mizigo bandarini kama wanavyofanya mawakala wa forodha.

"Wadau tumepokea kwa utii sheria hii, nasi tunawasiliana na wataalamu wetu juu ya jambo hili kwa kuwa tunashangazwa na jambo la mdhibiti naye kufanya biashara ya kishindani na watu anaowasimamia," alisema na kuongeza:

"Hatuelewi inakuwaje mdhibiti anakuwa mshindani, anayetakiwa akuangalie na kukutengenezea kanuni za kufanya biashara husika, naye anafanya biashara hiyo hiyo anakuwa mshindani wako."

Urio alisema ni vyema jambo hilo likaangaliwa kwa kina ili lisilete madhara ya kiuchumi kwa kampuni zenye mikataba ya kazi ambazo Tasac imetangaza kuanza kuzifanya.

"Kuna kampuni zenye mikataba na kampuni za madini katika kusafirisha mizigo yao na zimeajiri Watanzania na zinalipa kodi serikalini, kwa mabadiliko haya, maana yake wataathirika na hatujui hatima ya mikataba waliyoingia na wahusika," alisema.

"Katika hili, tunaomba sana busara kubwa itumike kuwe na utaratibu mzuri ambao hautaathiri mawakala binafsi na hata wateja kuhamia bandari nyingine kama ilivyotokea kwa mizigo inayopita."

Juzi, Katibu Mkuu, Tony Swai, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa, pamoja na kushiriki mchakato wa kutunga sheria, kuna mambo yalipitishwa bila kuwashirikisha, ikiwamo suala la mizigo iliyo safarini ambayo sheria haijataja nani aishughulikie.

Juzi, Tasac ilitoa tangazo kwenye vyombo vya habari kueleza kuwa kuanzia Machi 4, mwaka huu, itaanza kuondosha na kusafirisha mizigo bandarini.

Kazi hiyo itaanza ikiwa ni utekelezaji wa sheria iliyoanzisha shirika hilo ya mwaka 2017, inayolipa mamlaka ya usimamizi wa meli, huduma za uondoshaji shehena bandarini, mazingira ya meli na vyombo vya maji pamoja na ulinzi na usalama wa vyombo vya majini.

Katika tangazo hilo, ilielezwa kuwa kuanzia tarehe hiyo, shirika hilo litafanya kazi ya uondoshaji wa mizigo bandarini kwa inayosafirishwa nje na inayoingia nchini.

Mizigo iliyotajwa katika tangazo hilo ni pamoja na madini, mchanga wa madini (makinikia), mashine, vifaa, bidhaa mbalimbali, mafuta, silaha, wanyama hai na nyara za serikali.

"Kuanzia Machi 4, mwaka huu, Tasac itaanza kutekeleza jukumu lake la kisheria la kuondosha na kusafirisha mizigo bandarini katika maeneo ya madini, makinikia, mashine, vifaa, bidhaa na bidhaa nyingine zinahusu madini na mafuta," ilielezwa katika tangazo hilo.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, Tasac inawajulisha wadau na umma kwa ujumla kuwa, kuanzia tarehe hiyo hakuna msafirishaji au mpokea mizigo au taasisi yoyote itakayoruhusiwa kufanya tangazo lolote jipya kwa Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa lengo la kufanya kazi ya uondoshaji mizigo iliyotajwa kwenye kifunga cha saba cha sheria hiyo.

# DC aagiza kukamatwa mwekezaji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI wilayani Longido mkoani hapa, imeliagiza Jeshi la Polisi nchini, kumsaka na kumkamata mmiliki wa kitalu cha uwindaji cha Green Miles Safaris Ltd, Hawadhi Ally Abdallah, kwa kushindwa kulipa Sh. milioni 339 za vijiji 23. Licha ya fedha hizo, pia Halmashauri ya Wilaya ya Longido inamdai Sh. milioni 12 na malimbikizo mengine.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kutokana na mmiliki huyo kudaiwa kugoma kulipa fedha hizo za umma na kumwandikia barua yeye (Mkuu wa Wilaya) ya kumtaka amuombe radhi ndani ya siku saba, huku akitishia kumfikisha mahakamani kama hatatekeleza hilo.

Alisema mmiliki huyo amekuwa na vitisho na amefikia hatua ya kumwandikia barua Februari 16, mwaka huu, kupitia kampuni ya uwakili ya Law Associates ya Dare es Salaam ya kumtaka amwombe radhi ndani ya siku hizo kwa madai anachafua jina lake na asipofanya hivyo atamburuza mahakamani.

Mwaisumbe alisema anazo taarifa za kiintelijensia kwamba mwekezaji huyo amejificha nchini na amechukua fedha za kigogo mmoja toka Umoja wa Falme za Kiarabu aliyeingia nchini kufanya shughuli za uwindaji.

Alisema kwa kuwa amepigwa marufuku kuendesha shughuli za uwindaji wilayani humo, anataka kukimbilia mahakamani kufungua kesi, ili kuweka zuio aendelee shughuli za uwindaji hadi atakapoondoka kigogo huyo. Kwa mujibu wa Mwaisumbe, mwekezaji huyo aliingia mkataba wa makubaliano na wananchi wa vijiji hivyo Julai Mosi, 2013 wa kulipa Sh. milioni 5.5 kwa kila kijiji kwa vijiji 23 vilivyoko katika kitalu chake na Februari 29, 2014, alilipa vijiji 20 pekee na mpaka sasa hajalipa fedha zozote kwa vijiji hivyo.

"Mpaka sasa kila kijiji kati ya vijiji 20 kinadai Sh. milioni 14 na vijiji vitatu tangu aingie mkataba nao ambao hajawahi kuwalipa chochote, vinadai Sh. milioni 48. Cha ajabu katika barua yake aliyonipatia anadai kwamba hajawahi kuingia mkataba wowote na vijiji hivyo na hakuna fedha yoyote anayodaiwa kitu ambacho si kweli," alisema.

Aliongeza akiwa kiongozi wa wilaya hiyo ana ushahidi wa mikataba aliyoingia na vijiji vyote 23 na makubaliano ya vikao vya Baraza la Madiwani, ambavyo alishiriki lakini pia vikao alivyoshiriki ofisini kwa Mkuu wa Wilaya aliyepita.

Mwaisumbe alisema mikataba aliyoingia mwekezaji huyo na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (Tawa) pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii haihusiani na wananchi wa Longido na haitakuwa kigezo cha kufanya shughuli za uwindaji bila kuwa na uhusiano mzuri na wananchi, hivyo salama yake ni kulipa madeni aliyo nayo. Aidha, alionya vigogo walioko nyuma ya mwekezaji huyo na kuwataka kuacha mara moja kumkingia kifua kwa kumkataza kulipa fedha anazodaiwa.

Mkuu huyo wa wilaya alionya kuwa kwa kumkingia kifua watajikuta katika matatizo kwa kuwa kitendo alichofanya mwekezaji huyo ni sawa na uhujumu uchumi kwa sababu amekwamisha shughuli za maendeleo katika vijiji hivyo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Esupati Ngulupa, alisema tangu kuingia mkataba na mwekezaji huyo, vitendo vya ujangili na uchomaji mkaa vimeshamiri, ikiwamo kuuawa zaidi ya twiga 30 na majangili, sababu hafanyi doria kama ilivyo moja ya makubaliano ya mkataba.

**ewura**
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

**MAKAO MAKUU**
**Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole**
**S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni Taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea iliyoundwa na Sheria ya EWURA Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA inawajibu wa kuzidhibiti sekta hizi kiufundi na kiuchumi. Mamlaka ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili. Pia Mamlaka inadhibiti Umeme na Maji Safi na Usafi wa Mazingira kwa kuhakikisha huduma zinazodhibitiwa zinapatikana kwa viwango vya ubora wa kutosha; kwa bei halisi; salama na kwa uhakika; na kwamba watoa huduma wanapata faida ya halali na stahiki kwenye vitega uchumi vyao.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura Namba 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/No | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Fountain Petroleum Ltd – Nanhyanga Tandahimba S.L.P 826 Mtwara | Kijiji cha Nanhyanga, Wilaya ya Tandahimba, Mkoa wa Mtwara | Mehboob Osman (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 2. | Dua William Nkurua-Dua Service Station S.L.P. 246 Nanyumbu | Eneo la Mangaka, Wilaya ya Nanyumbu, Mkoa wa Mtwara | Meshack Osiah (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 3. | ATN Petroleum Ltd-Kibaha S.L.P 683 Morogoro | Kiwanja Na. 141, Eneo la Kibaha Mjini, Mkoa wa Pwani | Paulo Runyalula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 4. | Poly Petroleum Ltd S.L.P. 10117 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 107, Kitalu 'A', Eneo la Msongola, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam | Nassor Juma Said (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 5. | Neema Oil-Malinyi S.L.P Malinyi | Malinyi Mjini, Wilaya ya Malinyi, Mkoa wa Morogoro | Mabirika James Mabirika (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Chesco Madinga Petrol Station-Darajani S.L.P. 47 Ifakara | Eneo la Darajani, Wilaya ya Ulanga, Mkoa wa Morogoro | Chesco Madinga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 7. | Haider Muzafar Gulamali, S. L. P. 1986, Dodoma | Kiwanja Na. 154, Kitalu – Western Industrial Area, Jiji la Dodoma | Haider Muzafar Gulamali (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 8. | G.F.C General Supplies – GFC Petrol Station S.L.P 3 Makete | Kiwanja Na. 199, Kitalu "R.C", Makete Mjini, Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe | Francis L. Chaula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Camel Kapunga Filling Station S.L.P 26 Rujewa - Mbarali | Eneo la Kapunga, Kata ya Chimala, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya | Munif Ibrahim Khamis (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Kelvin D. Sanga – KDS Oil Filling Station S.L.P 14 Makete | Eneo la Tandala, Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe | Kevin Sanga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | Malongo I. James - Malongo Petrol Station S.L.P 34 Rujewa | Kijiji cha Ubaruku, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya | Malongo Isack James (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 12. | FAB International Limited – Samumba Petrol Station, S. L. P. 70419, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 1, Kitalu 'A', Samumba Area, Muungano Village, Ikungi District, Singida | Farid Ahmed Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**IMETOLEWA NA**
**Kaimu Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**
**Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole**
**S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania**
**Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

15081802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusicheze na kimeta kinaweza kutumaliza

**UWEZEKANO** wa kuenea maradhi ya kimeta ni mkubwa miongoni mwa wananchi wakiwamo walaji na wafanyabiashara wa nyama kama hatutabadilika.

Hadi sasa watu watano wamefariki na ng'ombe zaidi ya 21 wamekufa kutokana na kuenea kimeta mkoani Kilimanjaro.

Cha msingi tunawataka Watanzania kuchukua tahadhari na kula nyama zilizopimwa, kukaguliwa na kuchinjiwa machinjioni tena zinazouzwa buchani na si zile zinazopatikana mitaani.

Wakazi wa mijini na vijiji hula kitoweo kinachopatikana mitaani kwa kisingizio kuwa watu wengi ni maskini wasio na uwezo wa kununua nyama ghali zinazouzwa mabuchani.Tunaona kuwa hilo halina msingi kwani kimeta ni maradhi yanayoweza kuangamiza watu kwa muda mfupi hivyo tusiusingizie umaskini na kukimbilia kula nyama zisizopimwa.

Tunawahamasisha viongozi kuwahimiza wananchi kuepuka kula nyama zinazochinjwa mitaani pamoja na kukimbilia wanyama pori wanaokufa porini.Ni vyema kuepuka mizoga ya tembo, kiboko, nyati na nyumbu wanaookotwa na kuuzwa kwenye vijiji vilivyo jirani na mbuga za wanyama kwani huko nako kunaongeza uwezekano wa kueneza kimeta.

Tunatoa ushauri huo kwa sababu tunaimani kuwa watu wengi hawafahamu kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kula nyama zilizopimwa na kukaguliwa na wataalamu kwa kuwa nyama ni chanzo cha maradhi kuanzia kifua kikuu, minyoo ya tegu, kimeta na homa ya bonde la ufa na hata magonjwa ya ini.

Tunawahimiza wadau wa nyama na walaji wafahamu kwamba ukaguzi wa nyama unahusisha zaidi ya kuchunguza nyama machinjioni kwani kuna hatua nyingi mnyama anazopitia kama kumkagua akiwa hai na kuchunguza afya yake ili kuepusha uwezekano wa kusambaa zaidi magonjwa.

Walaji wafahamu kuwa mnyama anapochinjwa machinjioni huchunguzwa akiwa hai na anapokufa kuona iwapo anafaa kwa matumizi ya binadamu.Hapo ndipo magonjwa kama kimeta, homa ya bonde la ufa, kifua kikuu na maini yenye maradhi hugundulika.Tunatahadharisha kula nyama zilizochinjwa nyumbani, vichakani na hata maporini na wezi wa mifugo hakuna tofauti na kujitia kitanzi kwani ni kujiongezea uwezekano wa kupata maradhi hatari.

Ikumbukwe kuwa, kuna sheria na watalaamu na kinachotakiwa kufanyika ni kuhamasisha watu kuamka na kuachana na hatari za kula nyama zisizopimwa, kukaguliwa wala kuchinjwa kwa mujibu wa sheria.Lakini pia kuachana na kutumia kitoweo cha wanyamapori kisichokaguliwa na kuidhinishwa na wataalamu.

Tunatoa angalizo kuwa kuna idadi kubwa ya ng'ombe, mbuzi, nguruwe na kondoo wanaochinjwa bila kupimwa na kuuzwa mitaani iwe kwenye mabucha, migahawa na hata nyumbani kwa wafugaji.Ni jukumu la watu kutoa taarifa polisi na serikalini ili wahusika wakamatwe na hatua dhidi yao ichukuliwe ili kukomesha tabia hiyo inayoeneza magonjwa.

Maofisa afya wawahimize wananchi kutoa taarifa za wafanyabiashara wanaouza nyama za 'magendo au wizi' na kuzifikisha za wanaochinjia wanyama nyumbani bila kukaguliwa kwa mamlaka za juu ili kuwachukulia hatua kali.

Ni jambo la kusikitisha kuwa watu wengi nchini wanaishi na dhana kuwa nyama ya kuku haikaguliwi.Si kweli.Ni muhimu wananchi wakahimizwa na kuelimishwa kuwa kuku nao wachinjiwe machinjioni na si nyumbani na wakaguliwe ili kuepusha uwezekanao wa kusambaza magonjwa hatari kama mafua ya ndege.

Shime tubadilike kwani athari za kula nyama isiyokaguliwa ni kubwa kuanzia kuugua magonjwa kama taifodi, minyoo, kimeta na homa ya bonde la ufa lakini pia kuna uwezekano wa kupata matatizo makubwa kiafya kutokana na kusambaza maradhi hayo kwa wanyama wengine kama paka na mbwa ambao licha ya kwamba hawaliwi lakini wanaishi na binadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**KUB ADILISHA TAREHE YA KUZALIWA**

**KATIKA MIFUMO YA KULA HELA ZA UMMA, KUNA MCHEZO WA KUBADILISHA TAREHE YA KUZALIWA KABLA YA KUSTAAFU ILI KUENDELEA KUFANYA KAZI. WANAAPA MAHAKAMANI WAKIENDELEA KUBAKI KAZINI KULA JAMBO LA WENGINE. HOJA HIYO!**

**NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mashaka Mgeta

# Wigo wa kudhibiti ajali za barabarani utanulie

**TAIFA** limeshuhudia kwa huzuni kutokea kwa ajali iliyosababisha vifo vya wataalamu tisa wa Programu ya Kuwezesha Upimaji na Urasimishaji wa Ardhi (LTSP).

Katika ajali hiyo wataalamu wengine wanne walinusurika baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kutumbukia kwenye mto Kikwawila mkoani Morogoro.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa amekaririwa akisema gari hiyo aina ya Toyota Land Cruiser ni mali ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Tathmini iliyofanywa na gazeti hili imebaini kuwa katika kipindi cha miezi tisa sasa, taifa limeshuhudia ajali 7 zinazohusisha magari ya serikali zikisababisha vifo vya watu 25 na majeruhi kadhaa.Tathmini hiyo inayohusu magari ya serikali haiondoi maana na ukweli uliopo kwamba, licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na wadau wa usalama barabarani, tatizo la ajali katika sekta hiyo bado halijapata 'mwarobaini' wa kudumu.

Wapo wanaoamini kwamba si rahisi kumaliza ajali za barabarani. Fikra hiyo na nyingine za aina hiyo 'zinabeba' ukweli wenye mantiki hasa vyanzo vingine vya ajali vinapokuwa nje ya uwezo wa dereva aliye mshukiwa wa kwanza kila inapotokea ajali.

Lakini wapo wanaoamini kwamba kama jitihada thabiti zitafanywa kwa kuwahusisha wadau wengi kama si wote katika sekta hiyo, na kisha kila mmoja akatekeleza wajibu wake ipasavyo, basi ajali hizo zinaweza kuwa historia, ama zitatokea kwa nadra kuliko ilivyo sasa.

Mambo yote yanafikirika kwa sababu ajali za barabarani zina athari kubwa katika nyanja za uchumi, maendeleo, maisha na mali za watu.

Athari kubwa na yenye kuhuzunisha kutokana na ajali za barabarani ni vifo. Watu wanapopoteza maisha kwa sababu ya ajali za barabarani, inaweza kuchukuliwa kwa tafsiri rahisi kwamba 'Mungu alipenda', ingawa kwa sehemu kubwa inachangiwa na uzembe na kutofuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Na ukiukwaji huo wa sheria, kanuni na taratibu haupaswi kutazamwa kwa watumiaji wa barabara hasa madereva, bali wahusika wa mchakato wa kuanzia uagizaji wa magari na vipuri, mamlaka za upimaji ubora wa magari na vipuri, kadhalika wasimamizi wa sheria za usalama barabarani.

Serikali yenye dhamana ya kulinda mali na maisha ya watu lazima iisikilize sauti inayotoka kwa wadau mbalimbali wanaposhauri namna bora ya kukabiliana na ajali za barabarani.

Ninakumbuka kuna wakati kamati mojawapo ya Bunge iliwahi kufanya ziara kwenye nchi ambazo waagizaji wa magari wanazitumia kupata ama kupitishia bidhaa hizo.

Yapo 'madudu' kadhaa yaliyoibuliwa na wajumbe wa kamati hiyo akiwamo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ikiwamo biashara haramu ya vibali vya kuingiza magari pasipo kukaguliwa kwa mujibu wa sheria. Akichangia hoja kwenye moja ya vikao vya Bunge kwa wakati huo, Lugola alisema zipo mamlaka zilizobainika kutokuwa na ofisi kwenye nchi walizopaswa kufanya ukaguzi na badala yake vibali vya 'kuthibitisha' ubora wa magari vikawa vinanunuliwa mitaani.

Swali la kujiuliza ni, je, hali hiyo ilishashughulikiwa, ama taifa liliendelea 'kukaa kimya' baada ya 'kelele' za Lugola na wabunge wengine?

Huo ni mfano mmoja unaodhihirisha kwamba udhibiti wa ajali za barabarani haupaswi kuelekezwa kwa dereva pekee.

Kwa maana kama magari ama vipuri vinavyoingizwa nchini havitakuwa katika ubora wake, ni namna gani dereva anaweza kuzuia, mathalani breki kutofanya kazi ama tairi kupasuka wakati gari likiwa kwenye mwendo?

Wakati Taifa likiomboleza, ipo sababu ya Watanzania kuunganisha nguvu zetu dhidi ya adui huyu-ajali za barabarani.

Kila mdau ana nafasi yake katika kutekeleza wajibu wa udhibiti huo ili kwa pamoja, ufike wakati ambapo taarifa za kutokea kwa ajali za barabarani ziwe miongoni mwa matukio ya kihistoria nchini.

# MJADALA & BARUA

## *Kelele zimezidi Dar, serikali itusaidie sisi wakazi wake*

**Ndugu Mhariri wa Nipashe,**

*NAOMBA unichapishie yafuatayo katika gazeti lako kwa faida ya wananchi.*

*Leo hii katika jiji letu hili la Dar es Salaam kumeshamiri kelele nyingi na hali inaonekana itaendelea hivyo siku hadi siku.*

*Nyingi ya kelele hizi ni kutoka kwenye nyumba za starehe, baa, hoteli pia nyumba za ibada.*

*Na kwa bahati mbaya maeneo haya yameenea takribani katika sehemu zote za jiji letu, yaani kwenye makazi ya watu, hospitalini, katika zahanati, shule zetu na sehemu zingine za aina hii.*

*Aidha, kero zaidi ni kwamba mengi ya majengo haya yanatumia vipaza sauti ambavyo vinasababisha ukosefu wa starehe ya kupumzika kwetu sisi wananchi na mazonge mengine ambayo kwa ujumla wake yanasikitisha.*

*Wakati sasa umefika kwa serikali yetu na hasa Mheshimiwa January Makamba ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kuchukua hatua za makusudi za kudhibiti kero hiyo inayotutesa kwa hivi sasa.*

*Cha msingi, ni kwamba kelele hizi katika mazingira tunayoishi zinatuathiri kiafya, hivyo ni vyema taratibu, sheria na kanuni zikachukua mkondo wake.*

**Mwanamazingira-Dar**

## *Barua yetu ya wazi kwa Mwenyekiti CCM Taifa*

**Ndugu Mhariri pole na majukumu ya kikazi.**

*NINAYO heshima kwako kuomba nafasi katika gazeti lako tukufu ili uweze kutuchapishia barua yetu hii ya wazi kwa Mwenyekiti wetu wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).*

*Barua hii ya wazi kwa Mwenyekiti wetu Dk. John Magufuli ambaye pia ni Rais wa taifa letu hili inahusu suala la sisi wastaafu kunyang'anywa vibanda vyetu.*

*Kimsingi, sisi ni wazee wastaafu wa serikali na mashirika ya umma ambao tulijenga vibanda katika eneo la klabu la CCM, Uwanja wa Fisi kwa gharama zetu wenyewe.*

*Cha kushangaza viongozi wa kata wakatoa taarifa wilayani kwamba hatulipi kodi, kumbe tulikuwa tunalipa halafu viongozi hao hao wanakula kodi tunazolipa.*

*Kupitia kwako Mhariri tunamwomba Mwenyekiti wetu wa chama Taifa aingilie suala hili ili tuweze kurudishiwa vibanda vyetu hivyo.*

*Kwa kitendo hiki tulichofanyiwa, nimeamini kwamba kumbe kuna baadhi ya viongozi wa CCM ambao hawakitakii chama chetu hiki tawala mema na mafanikio katika jukumu lake la kutuongoza wananchi wa taifa hili.*

*Kwa kweli tunaomba haki itendeke katika suala hili.*

**Wazee wastaafu**
**Kijiji cha Mkamba 'A'**
**Kitongoji cha Mkamba,**
**Uwanja wa Fisi,**
**S. L. P. Kidatu.**

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# Serikali iangalie ustawi wa mtoto huyu

**Na Gaudensia Mngumi**

**MWAKA** huu umeanza na visa vya mateso ya mauaji ya watoto ambayo yameshuhudia watoto 10 wakiuawa mkoani Njombe na Simiyu. Baadhi ya watoto hao wamenyofolewa viungo vyao na ushirikina ndiyo unaotajwa kuwa ni chanzo cha uovu huo.

Safu hii ya Mjadala inashauri kuwa wakati wa kutafakari yanayowapata watoto hao ni vyema kuwapa kipaumbele watoto wenye ulemavu ambao wanasahaulika kila wakati.

Leo hii wadogo hawa wenye ulemavu wanateswa kupindukia kwenye mazingira ya siri mijini na vijijini na wengine wanageuzwa kuwa vitega uchumi wakitumiwa kuomba mijini.

Wapo watoto wamegeuzwa kuwa ombaomba wakiwekwa kwenye madaraja ya mabasi ya vituo vya mwendo kasi jijini Dar es Salaam eneo la Kimara na Morocco ili kutumiwa kuomba pesa kwa ajili ya familia zao ama walezi wanaowatunza.

Watoto hao wamekalishwa kwenye viti pembeni ya madaraja hayo ili wapita njia wawachangie tunajiuliza hivi hili linaruhusiwa? Wengine wapo njiani wakiwa wamefunikwa na miavuli na kuwekewa vikombe ili wachangiwe fedha hili nalo je? Wadau mnaliona?

Ukweli ni kwamba watoto wengi wanapitia katika hali ngumu, lakini wenye ulemavu wana hali mbaya zaidi.

Unavyoelekea watu wanasahau kuwa mtoto au watoto wenye ulemavu wanastahili msaada na upendo. Ikiwa ni pamoja na kutibiwa, kupewa nyenzo stahili kwa ajili ya kurekebisha ulemavu wake au wao. Kwa mfano kuwasaidia viti na baiskeli wasiotembea pia fimbo wasioona.

Mtoto mwenye ulemavu ana haki ya kupewa fursa sawa ya elimu na mafunzo pale inapohitajika. Ili kuendeleza vipaji vyake na uwezo wa kujitegemea.

Mtoto huyu ana haki ya kuishi kwa hadhi, heshima, uhuru, afya, kupumzika na kupatiwa elimu na malazi kutoka kwa wazazi au walezi wake.

Haki ya kupumzika na uhuru kwa mtoto vyote kwa pamoja vitategemea zaidi maelekezo na uwezo wa walezi au ndugu zake.

Kifungu cha 9(1)-(4) cha Sheria ya Mtoto kinaeleza kuwa mzazi ana wajibu na majukumu kwa mtoto wake ambayo yatatekelezwa, yawe yamewekwa na sheria au vinginevyo. Yatahusisha wajibu wa kumlinda dhidi ya kutelekezwa, kutengwa, kufanyiwa vurugu, kunyanyaswa, kutumiwa vibaya na kuwa katika mazingira mabaya kimwili na kimaadili.

Kutoa maelekezo, uangalizi, msaada na hifadhi kwa ajili ya mtoto pamoja na uhakika wa maisha na maendeleo ya mtoto kwa ujumla wake, pamoja na kuhakikisha kuwa wazazi na walezi wanapokuwa mbali na mtoto atapata uangalizi kutoka kwa mtu mwenye uwezo wa kutimiza majukumu hayo.

Mtoto atakuwa na haki ya kutoa maoni. Hakuna mtu atakayeruhusiwa kumnyima mtoto mwenye uwezo wa kutoa maoni haki ya kueleza maoni hayo kusikilizwa na kushiriki katika kufanya maamuzi yahusianayo na mustakabali mzima wa ustawi wa maisha yake.

Mtoto huyu aliyeko Morocco na Kimara ana maoni gani kuhusu sehemu hiyo anapowekwa ili kuomba hela?

Kifungu cha 13 (1)-(3) cha Sheria ya Mtoto, kinaeleza kuwa mtu yeyote hatoruhusiwa kumfanya mtoto apate mateso, au adhabu ya kikatili, ya kinyama au afanyiwe matendo yenye kumshushia hadhi kwa namna yoyote. Mbona kukaa kwenye sehemu hizo ni kama kuwapa watoto adhabu?

Sheria inaeleza kuwa anayevunja sheria hii, kwa mujibu wa kifungu cha 14, anatenda kosa. Na baada ya kutiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kisichozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

Ni vyema kufikiria njia bora za kuwatunza na kuimarisha usalama wa watoto hawa badala ya kuwatumia kama vitega uchumi kwenye mazingira mabaya yenye jua, mvua, vumbi na kejeli.

Ni wakati wa kufikiri na kudumisha mambo mema katika kuhakikisha wanalindwa na jamii pamoja na taifa kwa kuweka mazingira bora yakuzisaidia familia zenye watoto walemavu badala ya kuwaweka barabarani wakiomba kwenye mazingira ambayo huathiri afya zao.



# Tahadhari wakopaji benki

INATOKA UK 2

ya udalali ya Koti Brothers, kupitia gazeti la Mtanzania toleo namba 9191, ilielezwa kuwa, nyumba na viwanja vitauzwa kwa siku 14 na magari yatauzwa kwa siku saba.

Wiki iliyopita pia kulikuwa na matangazo ya taarifa za mnada kutoka ofisi za madalali tofauti kwenye vyombo mbalimbali vya habari likiwamo gazeti la Nipashe.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na kampuni ya udalali ya Maseto Auctioneer&Debt Collector, miongoni mwa vitu vilivyotajwa kuwa vitauzwa ni magari ya kifahari, nyumba na viwanja.

UCHUNGUZI WA NIPASHE

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe na kuchapishwa Desemba 20, mwaka 2017, kwa kuhusisha uchambuzi wa matangazo ya kunadiwa kwa mali za watu walioshindwa kulipa madeni yao kwenye taasisi mbalimbali za fedha, ulionyesha hali ya kufilisiwa mali kwa watu wa aina hiyo, imeongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka miwili kuanzia mwishoni mwa 2015 hadi Desemba 2017.

Magari, viwanja, mashamba na majengo mbalimbali yakiwamo ya nyumba za kuishi, hoteli na shule, ni miongoni mwa mali zilizotangazwa kupigwa mnada kwa bei poa katika nyakati tofauti baada ya baadhi ya wakopaji wake kushindwa kulipa madeni yao kwenye taasisi za fedha zikiwamo benki na hata taasisi za kuweka na kukopa (Saccos).

Katika uchambuzi huo, Nipashe ilitumia taarifa za matangazo ya minada zilizomo kwenye magazeti ya Nipashe, Mwananchi na HabariLeo ya kuanzia Novemba Mosi hadi Desemba 19, 2015 na kulinganisha na matangazo aina hiyo kwenye magazeti hayo matatu katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2017.

Matokeo ya uchambuzi huo yalionyesha kuwa mwaka 2015, ambao serikali ya awamu ya tano iliingia madarakani baada ya Rais John Magufuli kuapishwa Novemba 5, kulikuwa na nyumba 74, viwanja tisa na shule mbili zilizowahi kunadiwa na madalali mbalimbali kwa idhini ya taasisi za fedha baada ya wakopaji kushindwa kulipa, hivyo mali hizo kwa ujumla kuwa 85. Hakukuwa na tangazo la kunadiwa kwa magari katika kipindi hicho.

Idadi ya mali hizo zilizotangazwa kupigwa mnada iliongezeka maradufu katika kipindi cha Novemba Mosi hadi Desemba 19, 2017, baada ya matangazo ya madalali kwenye magazeti hayo kuonyesha jumla ya nyumba 256 zikinadiwa kwa idhini ya taasisi hizo za fedha, viwanja na mashamba 72, magari 76 na shule nne.

Kwa pamoja kulikuwa na jumla ya majengo, mashamba na viwanja 332 vilivyotangazwa kupigwa mnada kati ya Novemba Mosi na Desemba 19, mwaka huo.

Kwa hesabu hizo, tofauti ya idadi ya magari yaliyotangazwa kupigwa mnada baada ya wakopaji kushindwa kulipa marejesho yao kwa kipindi cha Novemba na Desemba mwaka 2015 na kipindi kama hicho mwaka 2017 ni 76 kutoka sifuri, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 100.

Pia tofauti ya nyumba, viwanja na mashamba vilivyotangazwa kupigwa mnada na madalali wa taasisi za fedha kwa Novemba Mosi na Desemba 19, 2015 na kipindi kama hicho mwaka 2017 ni 247, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 74.4.

***Taarifa hii imeandaliwa na Beatrice Moses na Mary Geofrey.***



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati) na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga, ofisini kwake, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

## Mume alilima Bunge barua kuhusu mkewe

INATOKA UK 2

ndipo Desemba, mwaka jana wakapeana talaka.

**BONNAH AFUNGUKA**

Akizungumza na Nipashe jana jijini Dar es Salaam, mbunge huyo alisema ni kweli ameachana na mume wake baada ya kupewa talaka kwa mujibu wa sheria za ndoa, kwa sasa anatambulika kama Bonnah Kamoli.

"Ni kweli nimeachana na mume wangu tangu mwaka 2018 baada ya kunipa talaka, lakini tangu mwaka 2017 tulikuwa tumeachana ingawa haikuwa rasmi mpaka ilipofika mwaka jana nilipopewa talaka kisheria," alisema.

Mbunge huyo alisema kwa sasa anatumia jina la Bonnah Kamoli na kwamba baadhi ya vitu vyake alivyokuwa akitumia jina la mume wake, ameanza kubadilisha.

Kadhalika, alikanusha taarifa iliyosambaa mtandaoni kuwa sababu ya kuachika kwake ni baada ya kufumaniwa na aliyekuwa mume wake jijini Dodoma.

"Tumepeana talaka kwa sababu za kifamilia, lakini naomba nikanushe kuachika kwangu si kwa sababu nilifumaniwa kama habari za mtandaoni zinavyodai. Kwanza tangu nimekuwa mbunge, mume wangu hajawahi kukanyaga Dodoma wala ile siku naapishwa kuwa mbunge hakuja, kwa hiyo si kweli kwamba nilifumaniwa,"

**"Ni kweli nimeachana na mume wangu tangu mwaka 2018 baada ya kunipa talaka, lakini tangu mwaka 2017 tulikuwa tumeachana ingawa haikuwa rasmi mpaka ilipofika mwaka jana nilipopewa talaka kisheria," alisema.**

# JPM akutana na bingwa wa upasuaji ubongo

INATOKA UK 3

Katika mazungumzo hayo, Rais Magufuli ameishukuru Hospitali ya Kimataifa ya Chuo Kikuu cha Peking kwa kukubali ombi lake la kuanzisha ushirikiano na MOI na amemhakikishia Prof. Yuanil kuwa Serikali ipo tayari kutoa ushirikiano zaidi utakaowezesha MOI kuongeza uwezo wake wa kutoa huduma za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa Watanzania ambao wamekuwa wakikosa huduma hiyo na kulazimika kutumia gharama kubwa kwenda nje ya nchi.

Rais Magufuli ameelezea kufurahishwa kwake na taarifa za kufanyika kwa mafanikio kwa upasuaji wa kwanza uliofanywa na Daktari Bingwa Prof. Yuanil hapo juzi na kwamba anaamini wataalamu zaidi wataendelea kuja nchini kutoka PUIH kwa ajili ya kutoa huduma na kuwafundisha madaktari wa Tanzania, na pia Watanzania wengi watakwenda nchini China kujifunza upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu.

Kwa upande wake Prof. Yuanil, alimpongeza Rais Magufuli kwa juhudi zake kubwa za kuhakikisha MOI inaimarishwa ikiwamo kufanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu na amemhakikishia kuwa PUIH itahakikisha makubaliano yaliyotiwa saini mwaka jana kati ya hospitali hiyo na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto yanatekelezwa kikamilifu.

"Tanzania kuna watu zaidi ya milioni 50 na kuna idadi kubwa ya watu wenye magonjwa ya ubongo, wanaopata majeraha kichwani, uvimbe wa ubongo, matatizo ya mishipa ya damu ya ubongo na magonjwa ya uti wa mgongo ambao wanahitaji kupata matibabu mazuri hapahapa, lakini naambiwa kuna wataalamu 10 tu ambao hawatoshelezi mahitaji, ndio maana tupo hapa kuangalia mnafanya nini na tuone namna ya kusaidia kuwaongezea uwezo," alisema Prof. Yuanil.

Naye Waziri Ummy amemshukuru Rais Magufuli kwa jitihada zake za kuwatafuta madaktari bingwa kutoka PUIH na kutoa maelekezo ya kuanzishwa kwa ushirikiano na MOI, pamoja na kuhakikisha Serikali inatoa zaidi ya Sh. bilioni 12.5 za kuimarisha miundombinu ya MOI ili itoe matibabu ya kibingwa ya upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa Watanzania wengi.

"Kwa kweli Watanzania wawe na matumaini makubwa kuwa huduma zile za kibobezi zitapatikana ndani ya nchi na hakuna kwenda nje, mambo yote ndani ya nchi, kwa hiyo tunashukuru sana kwa maono haya ya Rais Dk. John Magufuli, yeye ndio alipata taarifa kuwa kuna daktari bingwa huyu wa upasuaji wa ubongo na kisha akatupa maelekezo kuwa daktari huyo ameweza kutoa matibabu kwa wagonjwa walioshindikana katika nchi nyingi, kwa hiyo tukafanya mawasiliano kupitia Ubalozi wetu wa China na baadaye tukasaini mkataba Septemba 2018 nilipokwenda China na sasa tumeanza kutekeleza," alisema Ummy.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema kupitia ushirikiano huo Tanzania inatarajia kupata wataalamu wengi wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu na amebainisha kuwa pamoja na kufanya upasuaji wa mafanikio kwa mgonjwa mmoja hapo juzi, wagonjwa wengine wawili walitarajiwa kufanyiwa upasuaji jana na kwamba ushirikiano huo utaiwezesha MOI kuwa kituo bora cha upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu Barani Afrika.

HABARI KITAIFA

# Waomba gharama za gesi ya nyumbani ipunguzwe

**Na Halima Ikunji, TABORA**

WADAU wa mazingira mkoani Tabora wameshauri kupunguzwa kwa gharama ya gesi inayotumiwa nyumbani ili kudhibiti matumizi ya mkaa ambayo yanachochea uharibifu wa mazingira katika maeneo mengi nchini.

Ushauri huo ulitolewa jana katika kongamano maalumu la mazingira lililofanyika mjini hapo.

Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, alikuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo.

Walisema kuwa kuongezeka kwa vitendo vya uharibifu wa mazingira katika maeneo mengi nchini ikiwamo mkoa huo kunachochewa na shughuli za kibinadamu zisizofuata utaratibu ikiwamo gharama kubwa ya gesi.

Walitaja shughuli hizo kuwa ni kilimo, ufugaji, ukataji miti ovyo kwa ajili ya kuni na mkaa ambavyo huchochewa na ukosefu wa nishati mbadala iliyo na gharama nafuu ambayo ni rafiki mazingira.

Askofu Elias Chakupewa wa Kanisa la Anglikana Jimbo la Tabora, alishauri serikali kupunguza gharama za gesi ya majumbani ili wananchi wengi waweze kumudu bei yake hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya mkaa.

Mbunge wa Tabora Mjini, Emmanuel Mwakasaka, alisema kuwa kukata misitu ovyo bila utaratibu ni kujitakia laana kwa kuwa ukiharibu mazingira yatakuadhibu na wewe kwa kukukosesha mvua za kutosha, chakula na jamii kubaki maskini.

Askofu Ezekiel Yona wa Kanisa la Moravian mjini hapa alisema kutunza mazingira ni mpango wa Mungu ndio maana baada ya kumuumba Adamu alimweka kwenye bustani nzuri na kumwagiza kuitunza.

Naye Askofu mstaafu wa kanisa la Kitete Christian Center -TAG la mjini hapa, Paul Meivukie, alishauri mifugo yote idhibitiwe kisheria na kutengewa eneo maalumu la malisho ili kuepusha uharibifu mkubwa wa mazingira. Mratibu wa Kikundi cha Wajasiriamali wa Manispaa ya Tabora, Ashura Shaban, alisema kuwa jamii inapaswa kutunza mazingira yanayoizunguka kwa kuwa yakiharibika watakaoathirika zaidi ni kinamama na watoto kwa kukosa maji.

Mwenyekiti wa halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Said Ntahondi, alishauri agizo la Serikal la kupanda miti milioni 1.5 kila wilaya lisimamiwe ipasavyo na liwe na nguvu kisheria ili wilaya yoyote itakayozembea wahusika wachukuliwe hatua.

Ushauri huo ulipokelewa na Ofisi ya Makamu wa Rais waliahidi kuufanyia kazi.



Wakazi wa jiji wakipita kwa shida kutokana na bomba la maji kupasuka na kusababisha dimbwi kubwa barabarani, katika Mtaa wa Jitegemee Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wenye ulemavu watakiwa kujiunga CHF iliyoboreshwa

**Na Happy Severine. SIMIYU**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, Stella Ikupa, ametoa wito kwa viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu, kuwahamasisha wanachama wao kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), ulioboreshwa ili waweze kupata uhakika wa matibabu.

Ikupa alitoa wito huo jana wilayani Itilima, wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ikiwa ni pamoja na mradi wa Kitalu nyumba na masuala mbalimbali yahusuyo wenye walemavu.

Alisema, viongozi wa vyama na wenye ulemavu ni vema wakatoa taarifa na uhamasishaji wa kujiunga na CHF ulioboreshwa, ili kupatiwa matibabu kiurahisi.

Pia aliwaagiza Maofisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii kutoa elimu vijijini kwa watu wenye ulemavu kuhusu uundwaji wa vikundi na namna ya kutekeleza miradi mbalimbali.

Naye Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Festo Kiswaga, alisema mpaka sasa mkoa umeanza kutekeleza miradi ya vitalu na utatekelezwa kwa viwango na kwa malengo yaliyokusudiwa, huku akibainisha kuwa vitasaidia kuongeza kipato kwa wananchi katika mkoa na kuwa sehemu ya wananchi kujifunza kilimo bora.

Kwa upande wao viongozi pamoja na watu wenye ulemavu walioshiriki katika ziara hiyo walimwomba Naibu Waziri kushughulikia baadhi ya changamoto zinazowakabili katika maeneo yao.

"Ninaomba Serikali itusaidie tuweze kupata wakalimani wa lugha ya alama ili na sisi walemavu wa kusikia tuweze kupata ujumbe unaokuwa unawasilishwa na viongozi wetu kwenye mikutano na ziara kama hii ya leo hii itatusaidia sana," alisema Mhandi Ntobi, Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu wasiosikia Mkoa wa Simiyu.

# Wenye ualbino waomba asilimia mbili

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

WATU wenye ualbino Manispaa ya Bukoba wameomba Halmashauri ya manispaa hiyo kuwarahisishia gawio la asilimia mbili ili iwasaidie kwenye uzalishaji na kujikwamua katika mahitaji ya upatikanaji wa vifaa.

Hayo yamezungumzwa na Katibu wa watu wenye ualbino wa manispaa hiyo, Florence Felisian, wakati akiongea na Nipashe changamoto za ukosefu wa vifaa na madhara wanayoyapata kutokana na mionzi ya jua.

Felisian alisema, maalbino wengi wanahali ya kiwango cha chini katika uchumi na hutegemea misaada ya mashirika kuendesha maisha yao pia upataji wa vifaa vya kujikinga na madhara ya miili yao.

Alisema ni juhudi za viongozi kutafuta mashirika kama KCBRP ambalo linashugulikia wenye ulemavu kupeleka maombi ya misaada kupatiwa vifaa kama kofia za kukinga jua, miamvuli na mafuta.

Aidha alisema kuwa katika manispaa hiyo kuna jumla ya maalbino 90 kutokana hali ya jua, mionzi husumbua afya zao kwa kukosa mavazi ya kujikinga hivyo utafutaji wa kuingiza kipato sawa na watu wengine huwa kidogo.

Mkazi wa Kata Nshambya, Fausta Faustine, alisema anashukuru mashirika kuwapatia vifaa hivyo vinavyowakinga na jua wawapo kwenye mazingira ya ujasiriamali na humwepushia mionzi mikali kupenyeza ndani ya ngozi.

Faustine alisema endapo manispaa ikikamilisha utoaji wa asilimia mbili itaongeza kipato hasa kwa ambao tayari wanajishughulisha na itapunguza kuzungukia mashirika kutafuta vifaa kama mavazi.

"Sio kwamba kwa hali yetu ya ngozi hatuwezi kujishughulisha, tunafanya kile kinachowezekana, tatizo kubwa hapa ni mitaji ya kupata vifaa vya kuzuia jua ngozi zetu," alisema Faustine.

**Alisema ni juhudi za viongozi kutafuta mashirika kama KCBRP ambalo linashugulikia wenye ulemavu kupeleka maombi ya misaada kupatiwa vifaa kama kofia za kukinga jua, miamvuli na mafuta.**

# Naibu Waziri ataka sheria kuwadhibiti wakurugenzi

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameshauri itungwe sheria kuhakikisha kila Halmashauri nchini inapanda miti milioni 1.5 ili kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Alitoa ushauri huo baada ya agizo la Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alilolitoa alipokuwa akizindua kampeni ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani Desemba, mwaka jana kuwa kila halmashauri ihakikishe inapanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

Kanyasu alisema tangu agizo hilo lilipotolewa, hakuna halmashauri hata moja iliyotekeleza agizo hilo badala yake nyingi zimekuwa zikitaja takwimu za uongo.

Akizungumza mbele ya Makamu wa Rais, kwenye kongamano la kulinda mazingira lililofanyika kitaifa mkoani Tabora, Kanyasu alisema ili kuhakikisha agizo hilo linatekelezwa, itungwe sheria itakayowabana wakurugenzi kufanya hivyo.

**Endapo agizo hilo likapitishwa na bunge na baadaye kuwa sheria, wakurugenzi watapanda idadi hiyo ya miti badala ya ilivyo sasa kila mkurugenzi kutekeleza agizo hilo kama hiari.**

Alisema endapo agizo hilo likapitishwa na bunge na baadaye kuwa sheria, wakurugenzi watapanda idadi hiyo ya miti badala ya ilivyo sasa kila mkurugenzi kutekeleza agizo hilo kama hiari.

Kanyasu alisema halmashauri nyingi zimekuwa zikitaja takwimu kubwa za miti iliyopandwa lakini anapokwenda kuiona miti hiyo imekuwa haionikani na huku wengine wamekuwa wakiibuka na visingizio kwa vile hakuna idadi hiyo ya miti waliyoipanda.

Alisema idadi ya miti ambayo imekuwa ikitajwa na halmashauri kupandwa imekuwa ya vitabuni isiyo na uhalisia wowote.

Kwa mujibu wa Kanyasu, hata halmashauri ambazo zimekuwa zikijaribu kupanda, zimekuwa hazifikishi idadi hiyo na hata zikishapanda zimekuwa hazijishughulishi na kufuatia maendeleo yake.

Alisema hali hiyo imesababisha miti mingi kufa kwa kukosa uangalizi huku mingine ikiliwa na mifugo wakati halmashauri hizo zimekuwa zikibaki na takwimu zile zile za miti ziliyoipanda.

Makamu wa Rais kwa upande wake alisema agizo lake lililenga kila halmashauri ipande miti milioni 1.5 kwa mwaka ikiwa ni lazima na si hiari kama zinavyotekeleza.

Samia alisema agizo hilo lilikuwa wazi likitaka kila halmashauri ihakikishe inapanda miti ya aina yoyote ile akitolea mfano mizabibu na miti ya matunda ili mradi tu uwe mti bila kujali wa aina gani.

Aliongeza kuwa kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira unaoendelea nchini, Ofisi yake itahakikisha taratibu zinafuatwa za kulifanya agizo hilo liwe sheria.



Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (wa pili kushoto), akimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Reliance Group Ltd, Stephen Msaki, baada ya kuzindua matrekta aina ya Sonalika, yanayosambazwa na kampuni hiyo, katika hafla iliyofanyika, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkuu wa wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo na Meneja Mwandamizi wa kampuni ya International Tractors Ltd ya India, Sajal Bagga. **PICHA: JOHN BADI**

# Pombe zadaiwa kuchangia uhalifu

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MATUMIZI holela ya pombe za kienyeji katika mtaa wa Shunu mjini Kahama, yametajwa kuchangia matukio yanayogharimu uhai wa raia ikiwa ni pamoja na ajali za kila mara.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Shunu, Kube Shija, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema kuwapo kwa ajali za barabarani kunasababishwa na ulevi unaotokana na uuzwaji wa pombe hususani za kienyeji katika maeneo mengi ya mtaa huo pasi na kuzingatia taratibu elekezi.

Kube alisema suala hilo limekuwepo tangu kipindi anaingia madarakani na uongozi ulisimama kidete kuwashughulikia wale wanaovunja sheria ikiwamo uhalali wa matumizi ya pombe.

"Vilabu vya pombe kweli vipo maeneo haya, watu wanakunywa pombe na hiyo siwezi kukataa. Ajali zimekuwa zikitokea hata miezi miwili kuna mdada alipata ajali na hii ajali ya juzi wale vijana waliogongwa walikuwa wamelewa", alisema Kube.

Alisema Mtaa wa Shunu una vilabu 15 vya pombe ambavyo vinatambulika na hatua zinachukuliwa na uongozi wa mtaa kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ili kupunguza kama si kumaliza kabisa suala hilo ambalo linazalisha matukio mengi ya kihalifu.

"Kipindi naingia madarakani Shunu ilikuwa imechafuka kweli, hata tukienda polisi tulikuwa hatupewi nafasi ya kusikilizwa watu walikuwa wanachinjana sana. Watu waliokuwa wanafanya kazi machinjioni walikuwa wakikorofishana kidogo tu wanadhuriana. Nilijitahidi kutoa elimu kwa wananchi wote na walinielewa na sasa hali ni shwari," alisema.

Nipashe ilipita katika baadhi ya maeneo ya mtaa wa Shunu na kushuhudia pombe za Kienyeji zikitengenezwa na kuuzwa pamoja na kuzungumza na Neema John, ambaye ni muuzaji na kukiri kufanya biashara hiyo licha ya changamoto ya kuzingatia masharti ya biashara hiyo kama inavyoelekezwa na serikali.

Matukio yanayosababishwa na ulevi utokanao na pombe za kienyeji yametajwa kushamiri katika maeneo mengi ya wilaya ya Kahama hali ambayo inagharimu serikali

# Chenge apiga jeki ujenzi wa madarasa

**Na Happy Severine,** BARIADI

MBUNGE wa Bariadi Magharibi, Andrew Chenge, ametoa mabati 3,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 118 vinavyohitajika ili kunusuru wanafunzi 4,302 waliokosa nafasi ya kujiunga na elimu ya sekondari katika wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu.

Akikabidhi mabati hayo juzi, Chenge aliwataka watendaji wa serikali kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa hivyo ili vitumuke kwa malengo yaliyokusudiwa.

Chenge alisema baada ya kukaa kamati ya mfuko wa jimbo walikubaliana kununua mabati 2,000 ambayo baadaye yalionekana kuwa machache ndipo aliamua kutoa fedha zake binafsi kuongeza mengine 1,000 ili kukidhi mahitaji.


Alisema ana imani kuwa mabati hayo yataondoa changamoto ya maboma ambayo hayajaezekwa ili kuwawezesha wanafunzi waliokosa masomo kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa nao waende shuleni.

Wakipokea bati hizo, Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Wilaya Bariadi, Line Chanafi na Ofisa Mipango Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Emmanuel Mgongo, walipongeza hatua hiyo kwa kusema suala la maendeleo linahitaji kuungwa mkono na wadau mbalimbali, wakiwemo wananchi.

Mgongo alibainisha kuwa msaada huo utaongeza kasi ya kuezeka maboma ambayo yalikuwa hayajaezekwa kwenye halmashauri hiyo ili wanafunzi ambayo walikosa nafasi kutokana na upungufu wa madarasa waende shule.

Chanafi kwa upande wake alisema wilaya ya Bariadi inaendelea na ujenzi wa vyumba vya madarasa 118 vinavyohitajika ili kunusuru wanafunzi 4,302 waliokosa nafasi ya kujiunga na elimu ya sekondari.





## Watakiwa kujenga urafiki na watoto

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WAZAZI na walezi nchini wametakiwa kuwa karibu na watoto wao walioko katika kundi la kupevuka ili kupunguza ndoa za utotoni, mimba katika umri mdogo na magonjwa ya kuambukiza hususan Ukimwi.

Hayo yalisemwa jana na baadhi ya vijana walioshiriki tamasha la utoaji elimu rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana, iliyoandaliwa na shirika lisilo la kiserikali la JHPIEGO kupitia mradi wa Tupange Pamoja (TCI) kwa kushirikiana na watu wa afya mkoani hapa.

Mmoja wa vijana hao, John Steven, alisema endapo wazazi na walezi watabadilika na kuwapatia elimu sahihi ya masuala ya afya ya uzazi, changamoto hizo zitapungua kwa kiasi kikubwa.

"Lakini si kutupatia tu elimu bali tunahitaji wawe marafiki kwetu wanapotupatia elimu hii na wakifanya hivyo mimba za utotoni, ndoa katika umri mdogo na maambukizi ya Ukimwi na hasa maeneo ya pembezoni yatapungua kama si kwisha kabisa," alisema.

Naye Amina Hamza alisema baadhi ya wazazi na walezi wanachangia kuwapo kwa changamoto hizo kwa sababu wengi wao wanashindwa kuzungumza na watoto wao kuhusiana na hatua ya ukuaji.

Mratibu wa JHPIEGO kupitia mradi huo, Waziri Njau, alisema kujenga urafiki katika utoaji elimu ya afya ya uzazi kwa vijana muhimu, ili kuondoa woga kwao na kuwaweka karibu.

Alisema wamefanya tamasha hilo kwa ushirikiano na timu ya afya mkoani hapo, baada ya kubaini vijana wengi waoga kwenda vituo vya afya.

Njau alisema kabla ya tamasha hilo walitoa elimu kwa waandishi wa habari mkoani Arusha na kuwapatia elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ili kuwajengea uelewa katika nyanja hiyo na kuwawezesha kutoa elimu hiyo kwa vijana wengi zaidi, kupitia vyombo vyao.

**"Lakini si kutupatia tu elimu bali tunahitaji wawe marafiki kwetu wanapotupatia elimu hii na wakifanya hivyo mimba za utotoni, ndoa katika umri mdogo na maambukizi ya Ukimwi na hasa maeneo ya pembezoni yatapungua kama si kwisha kabisa," alisema.**

# Waziri ataka bajeti kubwa kilimo

Na Allan Isack, ARUSHA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema ni wakati mwafaka kwa nchi za Afrika, kutenga bajeti ya kutosha kwa wataalamu wanaofanya utafiti katika kilimo.

Hasunga alisema hayo jana katika mkutano wa kimataifa uliofanyika jijini hapa wa kuzindua mradi wa Avisa, uliolenga kueneza na kuhimiza teknolojia za mbegu bora za mazao ya jamii ya mikunde na nafaka.

Alisema nchi za Afrika zimetakiwa kutenga fedha nyingi, kwenye bajeti zao katika sekta ya kilimo ili kuwawezesha watafiti kuleta matokeo chanya na kwamba hatua hiyo itasaidia upatikanaji wa mbegu bora zitakazowasaidia wananchi kuongeza kipato na kuondokana na umaskini.

"Ni wakati mwafaka kwa nchi za Afrika kutenga fedha nyingi na kuwekeza zaidi katika sekta ya kilimo ili kuongeza tija na mapato sambamba na kukusanya kwa wingi fedha za kigeni zitokanazo na mazao ya kilimo," alisema Hasunga.

Alipongeza mkutano huo kufanyika nchini na kukutanisha watafiti, wataalamu na wasomi kutoka nchi saba za Afrika. Nchi hizo ni Tanzania, Mali, Burkina Faso, Nigeria, Ghana, Uganda na Ethiopia.

Hasunga alisema nchi nyingi za Afrika zinategemea kilimo na kwa Tanzania sekta hiyo inachangia pato la taifa kwa asilimia 29.1 na wananchi wanategemea kwa ajili ya kukidhi mahitaji mbalimbali yakiwamo chakula na biashara.

Aliongeza kuwa kilimo kinachangia maendeleo ya viwanda na kuwezesha upatikanaji wa malighafi zaidi ya asilimia 65. Pia alisema sekta ya kilimo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo ukame, upungufu wa rutuba, uwapo wa wadudu na magonjwa, miundombinu hafifu, kipato kidogo kwa wakulima, matumizi madogo ya pembejeo za kilimo na uhaba wa masoko ya uhakika na bei ndogo za mazao.

Alitaja changamoto zingine zinazozikabili nchi za Afrika ni kuwa na kundi kubwa la wakulima wadogo wanaolima kilimo cha kujikimu, matumizi ya pembejeo kama vile mbegu bora na mbolea, na matumizi ya jembe la mkono, hivyo kusababisha uzalishaji duni na umaskini kwa wakulima wengi. Alisema utafiti mbalimbali uliofanyika, umeshauri mambo ya msingi kufanyika ili kukabiliana na changamoto hizo, ikiwamo kuongeza uzalishaji na uhamasishaji wa matumizi ya mbegu bora na elimu kuhusu kanuni bora za uzalishaji.

Pia kuhusisha jinsia katika uzalishaji wa mazao ya jamii ya mikunde na nafaka, pamoja na kushirikisha wadau na serikali kuchukua matokeo ya utafiti na kuyafanyia kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqaro, alisema mkutano huo, umelenga na kutazama malengo ya millenia hadi kufikia mwaka 2020/25, kuondoa na kupunguza umaskini na njaa kwa Watanzania na kwa nchi za Afrika kwa ujumla.

Naye Mkurugenzi wa mazao na mbegu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Geofrey Mkamilo, alisema mradi huo utazisaidia kuleta mabadiliko makubwa katika kilimo cha nchi za Afrika kwa kuzalisha mbegu bora na watatoa elimu bora ya kilimo kwa wakulima .



Wakazi wa Kijiji cha Kimotorok wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakimpungia mkono Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James Ole Millya (hayupo pichani), wakati akizungumza nao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wakimbia nyumba kukwepa kukamatwa

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WANAUME wa Kata ya Olturument katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, wamezikimbia familia zao, kukwepa kukamatwa au kuchukuliwa mali zao, baada ya kushindwa kulipa mchango wa lazima wa Sh. 15,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya sekondari ya kata hiyo.

Hatua hiyo inadaiwa kuchukuliwa kutokana na Mtendaji wa Kata hiyo, Goodluck Chilya, kuwakamata baadhi ya wananchi wasiolipa michango hiyo.

Baadhi ya wananchi walidai kuwa mtendaji huyo anapita nyumba hadi nyumba akiwa ameambatana na balozi wa nyumba 10 na mgambo kadhaa kuwakamata baada ya kushindwa kulipa kiasi hicho cha fedha.

Mmoja ya wananchi hao ambaye aliomba jina lake kuhifadhiwa, alisema mtendaji huyo na kikosi chake, amekuwa na tabia ya kuwakamata wake zao au wasichana wa kazi na kuondoka nao hadi ofisini kwake ili kushinikiza baba mwenye nyumba aende kumkomboa kwa kutoa kiasi hicho cha fedha.

"Mtendaji huyu pindi anapofika kwenye kaya na kumkosa baba mwenye nyumba, huamrisha kuondoka na mtu yeyote akiwamo msichana wa kazi au mke ili baba atakaporejea aende ofisini kwake kumkomboa kwa kulipa mchango huo," alisema.

Mwananchi mwingine aliyelalamikia hilo, Anna Mollel, alisema mtendaji huyo na kikosi chake katika baadhi ya nyumba wanachukua mali kama vile magodoro, televisheni, redio, na samani ndani na kuondoka nazo.

"Tunashangaa wanafanya hivi kwa madai kwamba baba mwenye nyumba atakaporejea atakwenda kukomboa mali hizo kwa kulipa mchango huo, jambo ambalo linakwenda kinyume cha agizo la Rais John Magufuli la kutaka wananchi wasinyanyaswe kwa kuchangishwa michango.

"Hali hii imewalazimu wanaume wengi kuzikimbia familia zao kwa kuogopa kukamatwa au kuchukuliwa mali zao za ndani, sasa tunaomba kusaidiwa maana watakimbia hadi lini," alisema.


Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Dk. Wilson Mahela, alikiri kupokea malalamiko hayo juu na kwamba amemwagiza mtendaji wa kata hiyo kumpatia maelezo juu ya tuhuma hizo.

Alisema wananchi hao kupitia mikutano yao ya hadhara, walikubaliana kuchangishana fedha ili kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili ya shule ya sekondari.

Hata hivyo, alisema hakubaliani na namna ya uendeshaji wa jambo hilo kwa kuwa limekuwa na dosari nyingi, ikiwamo wananchi kulalamikia kukamatwa au kuchukuliwa kwa mali zao na kusema linawachafua viongozi wa halmashauri hiyo.

Chilya alipoulizwa juu ya madai hayo, alisema ni kweli amekuwa akifanya hivyo ikiwa njia mojawapo ya kukusanya fedha kutoka kwa wananchi, kwa ajili ya ujenzi wa madarasa.

Alisema walilazimika kufanya msako wa nyumba kwa nyumba katika kitongoji cha Kishori baada ya wananchi wa vitongoji vingine katika kata hiyo, kulalamikia wenzao kwa kukwepa kuchangia chochote.



## ‘Same ya kijani’ yaleta matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu, SAME**

MPANGO wa kuifanya Wilaya ya Same kuwa ukanda wa kijani, kwa kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira na uharibifu wa misitu unaochangiwa na ukataji miti kwa ajili ya ujenzi na nishati ya kuni na mkaa, umeanza kutoa matokeo chanya.

Mafanikio hayo yanatokana na wadau wa mazingira kuzijengea uwezo kaya, kufanya shughuli mbadala zinazowapunguza kasi ya matumizi ya rasilimali za misitu.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema mpango huo unawashirikisha wadau wote zikiwamo taasisi za serikali, sekta binafsi, mashirika ya dini na asasi za kiraia ili kubaini shughuli inayofanywa na kila mmoja na kuona pale panapohitaji ushiriki wa pamoja ili kufikia lengo.

Alisema mpango huo uliozinduliwa Julai mwaka jana, unalenga kuirejesha wilaya hiyo ya Same kwenye uoto wake wa asili na kuiondoa kwenye orodha ya wilaya zinazokabiliwa na changamoto kubwa ya ukame unaochangiwa na uharibifu wa mazingira.

Wananchi hao wanajengewa uwezo kuhusu uhifadhi wa mazingira na Shirika la SMECAO linalofanya kazi zake katika Wilaya za Mwanga na Same.

Alisema baada ya kuanza utekelezaji na kila mdau kufanya wajibu wake, tayari yapo matokeo chanya yaliyoanza kuonekana hususani kwenye suala la uchomaji mkaa na ukataji kuni baada ya wananchi walio wengi kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutumia majiko banifu yanayotumia kuni chache. “Licha ya kutumia majiko banifu, hamasa ya upandaji miti majumbani pia imesaidia upatikanaji wa kuni ambazo wanazipata kwa kupunguza matawi huku miti ikiendelea kustawi,” alisema.

Mkurugenzi wa SMECAO, Ezekiel Masawa, alisema kuwa mpaka sasa, wananchi wamepata fursa ya kujifunza shughuli mbalimbali za ujasiriamali utakaowawezesha kufanya shughuli mbadala zitakazowasaidia kuepuka kuharibu mazingira yao ikiwamo misitu.

“Sisi SMECAO tuanaamini kuwa wananchi wakiwekeza kwenye ufugaji wa samaki, kuku na nguruwe wataweza kupata mahitaji yao ya muhimu na wataongeza kipato na hivyo hawatakua tena na shauku ya kuingia msituni kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa au kukata miti kwa ajili ya kupasua mbao,”alisema Masawa. Matumizi ya majiko banifu pia yameelekezwa kwenye taasisi za serikali zenye matumizi makubwa ya kuni zikiwamo shule za msingi na sekondari.

Katika Shule ya Msingi Mvuleni iliyoko katika Kijiji cha Kisiwani, Mkuu wa shule hiyo, Nambosye Mduma, alisema kuwa baada ya kuanza kutumia majiko banifu, matumizi ya kuni yamepungua na kwa sasa shule inaweza kutumia sio zaidi ya mizigo mitatu ya kuni kwa chakula cha watoto 270.

Kwa upande wao wakulima na wafugaji wadogo walioanza kunufaika na mafunzo yanayotolewa kwenye kituo hicho na huduma za ugani zinazoendelea kutolewa na shirika la SMECAO wanakiri kubadili mfumo wa maisha na kuongeza kipato kwa asilimia kubwa.

# Ndugu wawili wafariki dunia kwa kunaswa na umeme

**Na Paul William, MOSHI**

WATU wawili wa familia moja, Zulfa Chami na Zuhura Chami, wamepoteza maisha baada ya kupigwa shoti ya umeme kwenye kamba ya kuanikia nguo katika eneo la Pasua, Manispaa ya Moshi.

Zulfa (24) na Zuhura (28) walifikwa na mauti hayo jana wakati wakianika nguo.

Habari zilizopatikana kutoka eneo la tukio na baadaye kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Hamisi Issah, zinaeleza kuwa ndugu hao wa familia moja walifariki dunia papo hapo baada ya kupigwa shoti ya umeme.

“Ni kweli ni mtu na dada yake wamefariki dunia jana (leo) saa kati ya 3:00 na 3:30 asubuhi katika eneo la Pasua Manispaa ya Moshi.

“Zuhura ambaye ni dada wa Zulfa alitoka eneo la Mailisita, Wilaya ya Hai na kuja Pasua anapoishi mdogo wake kumtembelea, ndipo wakati mdogo wake huyo aliyekuwa akifua nguo alipoanika katika kamba ya waya na kunaswa na umeme uliokuwa ukipita katika kamba hiyo.”

Kwa mujibu wa Kamanda Issah, dada huyo baada ya kuona mdogo wake amenaswa na umeme alimkimbilia kwa lengo la kumtoa, ndipo na yeye aliponaswa.

Alisema kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa kamba hiyo ya kuanikia nguo ambayo ni ya waya iligusana na waya uliokuwa ukipitisha umeme.

Kamanda Issah alisema baada ya tukio hilo, miili ya watu hao ilipelekwa kuhifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi.

Alipotafutwa Meneja wa Tanesco Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Mhawa Mkaka, kuzungumzia tukio hilo alisema Tanesco baada ya kwenda kufanya uchunguzi wa awali walibaini mfumo wa umeme katika nyumba hiyo ulikuwa una tatizo.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Kilimanjaro, Patrick Boisafi (kulia), akisalimiana na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa chama hicho (UWT) taifa, Gaudensia Kabaka, alipofanya ziara ya kikazi mkoani humo. Katikati ni Katibu wa CCM Kilimanjaro, Jonathan Mabihya. **PICHA: JMES LANKA**

# Daktari bingwa, wanafunzi watunukiwa kwa kumwokoa mtoto

**Na Mary Mosha, MOSHI**

DAKTARI bingwa wa upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi), Dk. Lobulu Molleli na wanafunzi watano wa mafunzo ya vitendo waliookoa maisha ya mtoto Sophia Massawe, aliyechanwa chanwa na panga lenye makali, wamepewa tuzo maalum na serikali ya utendaji uliotukuka.

Mtoto Sophia (2), alianguka darini siku chache zilizopita na kupoteza damu nyingi, baada ya mwili wake kujeruhiwa na panga lililokuwa limechomekwa ukutani na bibi yake.

Akikabidhi tuzo hiyo ya utendaji uliotukuka, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema serikali imeridhishwa na kufurahishwa na kitendo hicho ambacho kinatoa taswira ya kuheshimiwa kwa weledi wa watаalamu wa kada hiyo wanavyojitoa kuokoa maisha ya watu wakati wowote.

“Kwa namna mtoto huyu alivyookolewa maisha yake, sisi kama serikali tumeona jambo hili na tumeamua tuwatunuku vyeti vya kutambua mchango wenu. Huu ni utendaji uliotukuka ambao tunapaswa kuwashukuru.

“Natoa wito kwa watumishi wote kwenye idara ya afya kuhakikisha wanajituma katika kuokoa maisha ya watu wenye huitaji, kutumia lugha za faraja kwa kuwa serikali haitawaacha bila kutambua jitihada zao.” Madaktari wa mafunzo kwa vitendo waliotunukiwa tuzo hiyo wanatoka katika Hospitali ya Rufani ya mikoa ya Kanda ya Kaskazini na baadhi ya mikoa ya Kanda ya Kati ya KCMC.

Akizungumza kabla ya kupokea tuzo hiyo, Dk. Mollel alimweleza Mkuu huyo wa mkoa kwamba walimpokea mtoto huyo akiwa mahututi na katika hatari ya kupoteza maisha kutokana na kupoteza damu nyingi kutokana na majeraha aliyoyapata na walifanikiwa kuokoa maisha yake baada ya kutumia takribani saa tatu kumfanyia upasuaji.

Mmoja wa wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo ambaye alimpokea mtoto huyo, Godfrey Laswai, alisema hali aliyofikishwa nayo mtoto hospitalini hapo ilikuwa mbaya na walihangaika katika saa tatu katika kuokoa maisha yake.

“Tunamshukuru Mungu tumeweza kuokoa maisha ya mtoto huyo ambaye kila aliyemuona alikata tamaa ya kumuona tena akiwa hai, lakini kwa sasa anacheza na kuendelea na maisha yake,” alisema Laswai.

Naye mama mzazi wa mtoto huyo, Juliana Prosper, akielezea hali ya mtoto wake alisema kuwa baada ya kupewa taarifa za mtoto aliyekuwa amemuacha nyumbani dakika 30 zilizopita na kwenda kwenye biashara zake za kumpatia kipato, alipokea simu ikimtaarifu kuhusu tukio hilo na kufanikiwa kumkimbiza katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi.

Alisema alipofika alikuwa amekata tamaa ya kumuona mwanawe akiwa hai kutokana na kuvuja damu nyingi na kupoteza fahamu.

“Nilipoteza fahamu nilipofika Mawenzi sikujua kilichoendelea mpaka daktari alipokuja kuniamsha nikamuone mtoto anacheza, ilikuwa ngumu kuamini, lakini ni kweli mwanangu yupo hai na anaendelea na mazoezi. Nawashukuru wote waliojitahidi kuokoa uhai wa mwanangu,” alisema.

Ukurasa 18



**KASAKA ABAINISHA CHIMBUKO LA G55**

**MAKALA:**

Wanasiasa wanaopandikiza siasa za chuki wazingatie somo la Mangula



Ukurasa 14

**KIMATAIFA:**



**Ugaidi wazifikisha Pakistan, India ukingoni, ila hofu ya vita si kubwa**

Ukurasa 20


# siasa

JUMATANO FEBRUARI 27, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




**Afrika Kusini yamkamata waziri wa Msumbiji, kwa amri ya Marekani**

Ukurasa 15

# UHURU ampunguzia kazi Ruto, aweka msaidizi mkuu Baraza la Mawaziri

**Na Michael Eneza**

SIASA za Kenya kwa jumla na hasa mbio za kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2022 zimechukua sura mpya baada ya Rais Uhuru Kenyatta kufanya mabadiliko ya mbinu kama siyo ya mkakati, kwa kumteua Waziri wa Mambo ya Ndani Dk. Fred Matiang'i kuwa mwenyekiti wa Kamati Maalum za Baraza la Mawaziri.

Kamati hizo ambazo ingefaa kwa kawaida rais ahudhurie lakini anahitaji mtu wa kuzisimamia badala yake ahudhurie tu kikao cha Baraza la Mawaziri, huwa zinaendeshwa na Naibu Rais William Ruto.

Tatizo ni kuwa akili yote ya Dk. Ruto (aliyetunukiwa shahada ya uzamivu mahafali za mwaka jana) iko kwenye

ENDELEA UK 16



Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya.

UCHAMBUZI

# Wanasiasa wanaopandikiza siasa za chuki wazingatie somo la Mangula



Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa, Philip Mangula.



Mbunge wa Iramba Magharibi, Dk. Mwigulu Nchemba.

**Na Sabato Kasika**

SIASA inaelezwa kuwa ni shughuli ya kimaadili inayohusiana na ujenzi wa jamii yenye usawa.

Kwa maana hiyo, binadamu ni mtu wa kisiasa anayeishi kwenye jamii ya kisiasa, hivyo kila kitu ni siasa.

Aidha, inafafanuliwa kuwa, siasa ni utekelezaji wa mkataba kati ya watawala na watawaliwa, ambao msingi wake ni katiba na demokrasia ambayo ni serikali ya watu, iliyochaguliwa na watu, ikiongozwa na watu kwa manufaa ya watu.

Nchi hii iliingia katika mfumo wa siasa za vyama vingi mwaka 1992 na tangu wakati huo, Watanzania wamekuwa wakishuhudia, jinsi ambavyo baadhi ya wanasiasa wanafanya shughuli zao za kisiasa.

Wapo ambao wamekuwa wakiendesha siasa za chuki ili kugawa Watanzania kwa itikadi za kisiasa, hali ambayo ilisababisha Makamu wa Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Philip Mangula kutoa neno.

Septemba mwaka 2014, alionya kuhusu siasa za chuki wakati akitoa salamu za chama chake kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), jijini Dar es Salaam.

Alisema siasa siyo chuki bali ni tofauti za kisera, itikadi, ilani na falsafa

> Lakini inapofikia kuombeana mabaya eti kwasababu tu za kisiasa, basi hizo ni dalili tosha kwamba mihemko ya kisiasa inaipeleka nchi kubaya... wanasiasa warudi kwenye siasa za kushindana kwa hoja.

na kwamba pamoja na utofauti huo, jukumu la vyama vya siasa ni kuwa wamoja, kuwahudumia wananchi na kwamba kuna umuhimu wa vyama vya siasa kukutana mara kwa mara ili kujenga umoja wa kitaifa.

Anaviasa vyama vya siasa kutogeuza tofauti za kiitikadi na ilani za vyama kuwa chanzo cha chuki baina ya vyama na wafuasi wao na badala yake kuwa na umoja wenye kuwa na maslahi ya wananchi.

"Wanasiasa wanaochochea chuki na kusababisha vurugu waache kwa kuwa siasa ni uvumilivu na kuvumiliana...mbegu ya chuki inayotokana na itikadi za kisiasa inaweza kusababisha mgawanyiko kwa jamii yetu kutokana na siasa na hatimaye chuki," anasema Mangula.

Sasa ni kama miaka mitano imepita tangu Mangula atoe onyo hilo, ambalo ni kama baadhi ya watu halijawaingia na wamekuwa wakiendeleza siasa za chuki ambazo ninaamini mwisho wake si mzuri.

Kuna mifano mingi inaoonyesha kuwapo kwa siasa za chuki na hasa kwenye mitandao ya kijamii, jinsi ambavyo watu wamekuwa wakiwatakia wenzao mabaya na ukifuatilia utabaini kuwa ni kwasababu za kisiasa.

Ni hivi karibuni tu mbunge wa Iramba Magharibi mkoani Singida, Dk. Mwigulu Nchemba alipata ajali ya gari na kuwataka Watanzania wamuombee apone.

Lakini cha kushangaza, baadhi ya watu walimkejeli wakidai kuwa ni bora wamuombee punda aliyesababisha ajali hiyo apone kuliko kumuombea Dk. Mwigulu.

Lakini kwa nini? Watu hao wanadai kuwa wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, alizuia Tundu Lissu kuombewa, hivyo na yeye hakuna haja ya kumuombea, hivyo ajiombee mwenyewe.

Tukio hilo halikuanzia wa Dk. Nchemba tu bali hata Dk. Hamis Kigwangala naye aliwahi kukumbana na hali kama hiyo baada ya kupata ajali.

Kuombeana mabaya ni dalili tosha zinazoonyesha ni kwa jinsi gani siasa za chuki zinawapeleka mbali baadhi ya Watanzania na kusababisha watakiane mabaya.

Kimsingi vyama vya siasa havipaswi kugeuza tofauti za kiitikadi na ilani za vyama kuwa chanzo cha chuki baina ya vyama na wafuasi wao kama ambavyo aliwahi kuasa Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mzee Mangula.

Badala yake tofauti hizo za kiitikadi na ilani zinapaswa kujenga umoja wenye malengo ya kuimarisha maslahi ya wananchi.

Kwa mtindo huu wa kutakiana mabaya ni wazi kwamba Watanzania wanatakiwa kutafakari ni wapi siasa zinawapeleka na kisha warudi kwenye mstari na kuishi kwa kupendana bila kubaguana kwa itikadi za kisiasa.

Chuki za aina hii zikiachwa ziendelee zinaweza kuwa na madhara makubwa hivyo ni muhimu zizimwe mapema ili zisiendelee kupenya miongoni mwa Watanzania.

Mwenendo huu wa siasa za chuki au kujaza mbegu za chuki na kubaguana kwasababu ya itikadi za kisiasa miongoni mwa Watanzania ni hatari kwa Tanzania ijayo kama utaendelea.

Inasikitisha kusikia baadhi ya wanasiasa kuzungunmzia mambo ambayo ukiyatafakari utabaini kwamba yanalenga kujaza chuki wafuasi wa vyama vyao dhidi ya wale wa vyama vingine.

Ikumbukwe kuwa Watanzania wanaunganishwa kwa Utanzania wao, huyu akiwa wa chama fulani na yule wa chama fulani wanatakiwa kushirikiana katika mazingira yote.

Lakini inapofikia kuombeana mabaya eti kwasababu tu za kisiasa, basi hizo ni dalili tosha kwamba mihemko ya kisiasa inaipeleka nchi kubaya... wanasiasa warudi kwenye siasa za kushindana kwa hoja.

Wote ni Watanzania ingawa kila mmoja ana chama chake na pia wapo wengine siyo wanachama wa vyama vya siasa wote hao wanaunganishwa kwa Utanzania wao, hivyo wanaoendekeza siasa za chuki wasiwavurugie wengine.



Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini. **PICHA: MTANDAO**

# Afrika Kusini yamkamata waziri wa Msumbiji, kwa amri ya Marekani

**Na Nimi Mweta**

SERIKALI ya Msumbiji imeshangaza dunia kwa kuchukua wiki takriban tatu kuanzia wakati waziri wake wa zamani wa Fedha, Manuel Chang, kukamatwa uwanja wa ndege wa kimataifa wa Oliver Tambo jijini Johannesburg kwa hati ya kukamatwa iliyotolewa na Marekani na kuzuiliwa katika uwanja wa ndege hadi kutaka arejeshwe nchini humo.

Baadaye hakimu wa Mahakama ya Johannesburg akatoa idhini ya kukamatwa kwa waziri huyo wa zamani ambaye Marekani inataka apelekwe humo ili akajibu mashtaka ya kupokea rushwa kubwa katika mradi wa uvuvi uliopata mkopo kutoka nje.

Tayari mvutano umeanza kati ya Msumbiji na Marekani kuhusu waziri huyo, Msumbiji ikitaka arudishwe afunguliwe mashtaka huko, huku Marekani ikitumia sheria yake yenyewe.

Mradi husika ulichangia katika deni la taifa na kuisukuma Msumbiji kutafuta misaada Benki ya Dunia (WB) na kwenye Fuko la Fedha la Kimataifa (IMF).

Ni mradi uliogubikwa na rushwa ambako deni la taifa la dola bilioni mbili liliongezeka kwa nguvu Chang akiwa waziri.

Deni liliingizwa miaka ya 2013 hadi 2014 kupitia udhamini wa mradi wa uvuvi ambao ulipaji wake wa madeni na hata kazi ya uvuvi ilikwama, Msumbiji ikatoa taarifa za deni hilo kwa IMF baada ya miaka mitatu.

Waziri huyo wa zamani alikamatwa katika mtiririko wa mkasa ambao hivi karibuni umemkumba Nambia Guebuza, mwanae rais wa zamani Armando Guebuza kwa kuhusika na kuandaa mikopo ya mradi wa uvunaji wa tuna katika eneo la kiuchumi la bahari nchini humo mwaka 2012.

Haikuchukua muda mrefu kwa udhaifu wa mradi huo kuonekana, na tatizo la msingi lilikuwa ni kuhusishwa kampuni za serikali kama wabia na huku waendeshaji ni kampuni za nje, na deni likiwa limedhaminiwa na serikali.

Kulikuwa na sehemu kubwa ya deni ambayo haikuwa ya kununulia vifaa vya uvuvi, na badala yake ikaelekezwa katika 'usalama wa ufukwe.'

Mradi huo ulipoanza ulionekana kama hatua kubwa ya ukombozi wa kiuchumi, kuvuna samaki hao kutoka baharini, kuingiza fedha za kigeni na kuwezesha nchi hiyo na za jirani kupata samaki waliosindikwa kwa kiwango cha juu, tena kwa bei ndogo.

Zilinunuliwa meli 24 za kuendesha mradi huo, lakini miaka mitatu baadaye meli hizo zilikuwa zimepata kutu katika bandari ya Maputo.

Mkopo wa dola milioni 850 wa kibiashara wenye riba kubwa uliandaliwa na benki ya Credit Suisse ya Uswisi na benki ya VTB ya Russia kwa ajili ya kile kilichoitwa 'miundombinu ya uvuvi,' kwa kutumia hati fungani ya serikali ya Msumbiji kwa kampuni yake ya uvuvi, Ematum.

Mkopo huo ambao kimsingi ulikuwa ni wa muda mfupi ulionekana mwanzoni kuwa utalipika kutokana na mradi huo kuwa wenye uwezo wa kujitegemea, lakini mwenendo wake haukuwa hivyo.

Kutokana na riba ambayo inaongeza deni kila mwaka, wakati dola milioni 500 hazikuwa katika mpango halisi wa uvuvi bali kuelekezwa katika taasisi za usalama wa baharini na ufukwe, kampuni hiyo kwanza haikufikia malengo yake ya uvuvi na mapato, na uwezo wa kulipa deni hilo ukaingia katika changamoto za wazi.

Wataalamu wa fedha wanasema ukubwa wake katika kulipa ni kiasi cha asilimia 80 ya pato la taifa ikiongezewa na madeni mengine yanayoikabili serikali ya Msumbiji, hivyo kufanya mpangilio wake wa matumizi kuwa tabu, na utegemezi kuzidi.

> "Wapo watu wengine 18 wamekamatwa Msumbiji, na maofisa watatu wa Credit Suisse pia walikamatwa jijini London nchini Uingereza kwa hati iliyotolewa pia na Marekani kuhusiana na kashfa hiyo ya mkopo wa uvuvi.

Ni katika juhudi hizo za kutafuta misaada ya kifedha katika taasisi kama WB na IMF ambako shinikizo la kuwapeleka mbele ye mahakama waliohusika na mkopo huo lilipoanza, na kuwa sehemu siyo tu ya makubaliano na nchi kama Marekani, bali matazamio ya nchi wafadhili kwa jumla.

Jinsi ambavyo dola milioni 500 zilielekezwa katika kampuni za serikali ya Msumbiji kwa shughuli za usalama ndiyo eneo lililoleta utata zaidi, na mifumo ya rushwa iliyosukwa kuanza kujionyesha.

Kampuni hiyo ilikuwa inapata kiasi cha dola 450,000 kwa mwaka kutokana na tuna, na siyo dola milioni 18 kwa mwaka zilizotarajiwa.

Serikali ya Msumbiji ilianza kujisikia huru kuhusu suala hilo baada ya Marekani kuchukua hatua, ilipotoa hati ya kukamatwa kwa waziri Chang kwa madai kuwa Chang alipokea dola milioni 12 kukubali kutia saini mkataba huo wa mkopo.

Hati ya mashtaka ya Marekani inasema kuwa jumla ya dola milioni 200 zilitumika kutoa rushwa maeneo tofauti, na kufunguliwa kwa kesi hiyo kutaleta vurumai ya aina yake nchini humo hasa baada ya kukamatwa kwa mwanae rais mstaafu.

Walioko madarakani hivi sasa hawako salama kwani Rais Filipe Nyusi ndiye alikuwa waziri wa Ulinzi wakati huo, na hati ya Marekani ilisema alitia saini baadhi ya kandarasi muhimu.

Wachunguzi wa habari wa kimataifa mjini Maputo walionyesha mshangao kwa hatua ya Msumbiji ya kutaka Manuel Chang apelekwe huko, kwani walilazimika tu kufanya hivyo baada ya Afrika Kusini kutii amri ya Marekani (hati ya kisheria) kwa suala hilo.

Ndipo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali nchini Msumbiji alipeleka hati ya kuomba kurudishwa Msumbiji kwa waziri huyo, baada ya Mahakama ya Afrika Kusini kutoa hati ya kukamatwa kwake na polisi ili kufunguliwa mashtaka, baada ya kuzuiliwa uwanja wa OR Tambo kwa hati hiyo ya Marekani.

Wapo watu wengine 18 wamekamatwa Msumbiji, na maofisa watatu wa Credit Suisse pia walikamatwa jijini London nchini Uingereza kwa hati iliyotolewa pia na Marekani kuhusiana na kashfa hiyo ya mkopo wa uvuvi.

Zenaida Machado, mtaalamu wa shirika la Human Rights Watch huko Msumbiji alisema kuwa kabla ya kukamatwa waziri Chang kwa hati ya Marekani huko Afrika Kusini, watawala walikuwa wameridhika kuwa asiwepo nchini, lakini baada ya kukamatwa wanatoa tangazo kuwa wanamhitaji.

Ndambi Guebuza alitajwa kuhusika na kificho cha dola bilioni mbili za mkopo zilizofichwa, kama sehemu ya mkopo huo ambao hati ya Marekani inasema ulifichwa kwa Bunge la Msumbiji na IMF hadi kukwama kwa mradi huo na kulipa deni kulipoanza.

Baadhi wanahisi kuwa kukamatwa kwa mwanae Guebuza ambaye ni mfanyabiashara kuna chembe ya kutafuta kinga kwa Rais Nyusi mwenyewe, lakini inahofiwa kutakuwa na shinikizo la ziada kutoka Marekani kuhusu kesi hiyo inavyoendeshwa, mradi Msumbiji bado inahitaji mikopo kutoka kwa wafadhili.

Wako wanaoamini kuwa kukamatwa kwa wahusika wote hao ni danganya toto kwa ajili ya mahakama hiyo ya Afrika Kusini, ambayo sasa iko katika mvutano wa serikali ya Marekani na ya Msumbiji kuhusu waziri Chang, kwani Msumbiji inataka arudishwe nyumbani, si kushtakiwa Marekani.

Kuna uwezekano kuwa suala hilo liamuliwe na Rais Cyril Ramaphosa, kama ilivyokuwa wakati wa kukamatwa kulikoshindikana kwa Rais Omar el Bashir wa Sudan akiwa amehudhuria mkutano wa Umoja wa Afrika, ikatoka hati ya mahakama ya Afrika Kusini akamatwe apelekwe kujibu mashtaka Uholanzi (The Hague) kwa uharamia wa kivita. Serikali ilifuta hati.

MAKALA

Inatoka Uk.13

kampeni za kujiandaa 2022.

Kabla ya uteuzi huo Rais Kenyatta alinukuliwa akisema kuwa mivutano kuhusu uteuzi wa mgombea wa Jubilee, mkusanyiko wa vyama vya siasa ulioko madarakani, unadhoofisha utendaji serikalini, na isitoshe yako maeneo mengi ambako tofauti zake na naibu rais ni za wazi na hazina mjadala.

Naibu rais huyo amekuwa akizunguka maeneo tofauti nchini akitumia wadhifa huo wa kusimamia shughuli za maendeleo, kwani mfumo wa serikali Kenya hauna waziri mkuu.

Ina maana kuwa Dk. Matiang'i sasa anakuwa kama naibu rais wa pili, kwa nafasi yake hiyo ya waziri kiongozi, hali ambayo inampa Ruto uhuru zaidi wa kusafiri, makali yakipungua.

Wachambuzi wa siasa nchini Kenya wanaona kuwa mabadiliko hayo ni mwendelezo tu wa athari za 'kupeana mikono' kati ya Rais Kenyatta na kiongozi wa upinzani Raila Odinga ambako zilikubaliwa ajenda tano za mazungumzo na kufanyia kazi baada ya hapo.

Ni pamoja na 'madudu' ya uchaguzi mkuu wa 2017, rushwa, ukabila, madaraka mikoani na usalama wa taifa - hasa kutokana na mtafaruku ulioenea nchini baada ya upinzani kususia uchaguzi wa marudio, na kumwapisha Raila kama 'rais mbadala wa watu wa Kenya.'

Ajenda hizi zilivyotekelezwa ni mwiba kwa naibu rais, akisimamia uhafidhina, kukandamiza upinzani na maeneo yao.

Wakati ambapo Raila alielezea kufikiwa kwa makubaliano na Rais Kenyatta kuwa ni kutaka kuwaletea maendeleo watu wake, wasiwekwe nje ya maendeleo hadi uchaguzi mkuu unaofuata 2022, suala muhimu zaidi ni kumaliza mtafaruku uliokuwepo.

Sasa katika kutatua masuala ya ajenda hizo, ni wazi msingi wa muafaka wa kubadili dira ya chama tawala kuhusu nani awe kiongozi, au uchaguzi ufanyike kwa njia gani kuondoa nafasi ya kurudiwa kwa mtafaruku wa 2017 ilibidi ufikiwe, na ni katika mazingira hayo ambako naibu rais amejikuta akitengwa.

Wafuasi wake katika maeneo tofauti wanaonekana kutajwa zaidi kwa masuala ya rushwa, 2018.


Kufikia mabadiliko hayo serikalini, yako maeneo mawili ambayo inaelekea yalimtatiza Rais Kenyatta, moja ni wazi linahusu matumizi ya muda katika ratiba za naibu rais Ruto, kwani mikutano yake mingi na maongezi yake binafsi ni ya kisiasa.

Anatafuta kwa udi na uvumba kuhakikishiwa utii na viongozi wa Jubilee katika ngazi tofauti, wakati mwelekeo wake wa kisiasa siyo kujumuisha bali kubakiza kambi hizo mbili za kisiasa, za 'wao' na 'sisi' wakati undani wa kupeana mikono hasa ulikuwa ni kuondoa uhasama huo na kuweka mbele maslahi ya taifa kwa misingi ya ukweli na maadili katika kusimamia maendeleo. Ruto alionekana mzito kufuatilia hilo.

Ina maana kwa kiwango fulani naibu rais hakuwa mtu wa kutegemewa kusukuma mbele miradi ya maendeleo na kufanya maamuzi maeneo tofauti katika kubuni na kufuatilia juhudi za maendeleo katika majimbo au wilaya tofauti.

# Uhuru ampunguzia kazi Ruto, aweka msaidizi mkuu Baraza la Mawaziri

> Imekuwa ndiyo 'sekretariati' ya kutekeleza ajenda za utawala wa muhula wa pili wa Rais Kenyatta, hali ambayo kimsingi ni kubadili mwelekeo wa serikali kutoka ule wa uchaguzi mkuu uliozua mtafaruku, na kuchukua sura ya serikali sikivu.



Rais Uhuru Kenyatta (kushoto), akiwa na Naibu Rais William Ruto. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Kinara wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga (aliyenyoosha mikono).

Dhamira yake ni kuwavuta wanaounga mkono kuendelea na Jubilee mwaka 2022 kama ilivyo sasa na kwa vile Rais Kenyatta anamaliza muhula wa pili ni wazi ni yeye anayefuata, hali inayomaanisha kuwa tatizo la ajenda ya kwanza, madudu ya uchaguzi 2017 lisifanyiwe kazi, mvutano uendelee hadi 2022.

Ni wazi Rais Kenyatta alihitaji kupata njia nyingine ya kufuatilia ajenda zake na siyo kumwelekeza naibu asiyezitaka.

Wakati Rais Kenyatta akiwaelekeza mawaziri kushirikiana kwa karibu na Waziri wa Mambo ya Ndani Fred Matiang'i katika kutekeleza ajenda za urais wake, naibu rais alijitahidi kuwatuliza wafuasi wake kuwa Matiang'i katika nafasi hiyo mpya anaripoti kwake.

Ina maana kuwa kuna mtiririko ule ule wa kazi za Baraza la Mawaziri ambako Matiang'i ni waziri kiongozi chini ya naibu rais na ndipo afikiwe rais jambo ambalo Ruto anajua si kweli, kwani Dk. Matiang'i amepewa mamlaka mapana ya kufanya maamuzi, kwa vile amejadiliana kirefu na rais kujua nini kinatakiwa kufanyika katika kila eneo.

Ni mjumbe maalum mwenye mamlaka ya kutosha, aina ya waziri mkuu, na naibu rais anafahamu kabisa kuwa rais hatamwuliza yeye kuhusu anachofanya Matiang'i.

Dk. Matiang'i alisema hivyo yeye mwenyewe katika mkutano wake wa kwanza akisimamia nafasi hiyo mpya ambako aliungana na kamati ya wataalamu kutoka wizara tofauti kuzungumzia kile kinachoitwa 'Big Four' nchini humo, yaani ajenda nne muhimu zaidi za utawala.

Ajenda hizo ni uhakika wa chakula, nyumba bora wanazoweza kununua au kupanga walio wengi, kukuza viwanda na afya bora, ambako waziri Matiang'i alisema baada ya kikao hicho kuwa kamati imeorodhesha maeneo kadhaa ya changamoto katika utekelezaji wa ajenda hizo:

"Kamati itakuwa inatoa ripoti za kila wiki na mapendekezo ya jinsi ya kutatua changamoto hizo, kwa rais."

Kuainisha kuwa ana nafasi muhimu, waziri Matiang'i hakutoa taarifa hiyo yeye mwenyewe bali ilitolewa na Katibu Mkuu Karanja Kibicho, hali inayodhihirisha kuwa siyo tu kuwa Matiang'i amepewa majukumu ya ziada katika Baraza la Mawaziri pamoja na hili la kuwa waziri wa Mambo ya Ndani, ila wizara hiyo pia imeinuliwa.

Imekuwa ndiyo 'sekretariati' ya kutekeleza ajenda za utawala wa muhula wa pili wa Rais Kenyatta, hali ambayo kimsingi ni kubadili mwelekeo wa serikali kutoka ule wa uchaguzi mkuu uliozua mtafaruku, na kuchukua sura ya serikali sikivu.

Bado siyo shirikishi kwa sababu wapinzani hawakujumuishwa, ila ajenda zimeunganishwa.

Kamati anayoiongoza Matiang'i ilizinduliwa na Rais Kenyatta ikiitwa Kamati ya Baraza la Mawaziri ya Utekelezaji wa Maendeleo ya Taifa na Mawasiliano, ambako wajumbe wake muhimu zaidi ni Matiang'i kama mwenyekiti na Waziri wa Fedha Henry Rotich.

Kuacha wajumbe wa Baraza la Mawaziri ambao kwa nafasi zao ni wajumbe wa kamati hiyo, inawahusisha pia Mwanasheria Mkuu Paul Kihara na Mkuu wa Utumishi Serikalini Paul Kinyua na hakuna ubishi wowote kuwa kazi zake zinasimamiwa au kuripotiwa moja kwa moja kwa rais, na si naibu rais.

Dk. Ruto sasa ni naibu rais kivuli zaidi, muda wote ni mwenyekiti DP, chama chake.



Maboksi ya kupigia kura yalitelekezwa katika Wilaya ya Isolo huko Lagos.. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Zijue sababu Marekani kuwawekea vikwazo vya usafiri viongozi wa DRC

HATUA ya Marekani kuwawekea vikwazo vya usafiri maafisa wakuu wa Tume ya Uchaguzi pamoja na viongozi wengine nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, (DRC) imeendelea kuzua hisia mbalimbali.

Serikali ya Marekani ilichukua hatua hiyo mwishoni mwa wiki kwa madai kwamba viongozi hao walijipatia utajiri kwa njia za rushwa.

Msemaji wa Tume Huru ya Uchaguzi, Jean Pierre Kalamba, kupitia barua iliyotiwa saini na tume hiyo, amekanusha tuhuma hizo za rushwa na kuongeza kuwa ilifanya kazi nzuri ya kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa njia ya amani. Hali ambayo anasema ilisaidia marais wawili wa Congo kupokezana madaraka kwa njia ya amani.

Bw. Kalamba ameahidi kutoa ripoti ya maandalizi ya uchaguzi kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka huu.

Naye Lambert Mende, ambaye alikuwa msemaji wa serikali ya Joseph Kabila, amesema vikwazo hivyo havitakuwa na mafanikio yoyote.

''Marekani inasimama na watu wa Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo, kufuatia historia waliyoweka kwa kufanikisha mchakato wa viongozi kupokezana madaraka kwa amani. Uchaguzi ulionyesha ari ya wakongo ya kutaka mabadiliko ya serikali na taasisi zinazowajibika. Hata hivyo, kuna madai kwamba hapakuwa na uwazi katika machakato wa uchaguzi.'' Ilisema taarifa iliyotolewa na Marekani.

Viongozi waliowekewa vikwazo ni pamoja na Mwenyekiti wa Tume ya Huru ya Uchaguzi ya Congo DRC (CENI), Corneille Nangaa, naibu wake Norbert Basengezi Katintima.

Wengine ni mshauri wa mkuu wa CENI, Marcellin Mukolo Basengezi, kiongozi wa Bunge la Kitaifa, Aubin Minaku Ndjalandjoko pamoja na rais wa mahakama ya kikatiba Bw. Benoit Lwamba Bindu.

Marekani pia imewawekea vikwazo vya usafiri maafisa wa kijeshi na maafisa wa serikali wanaoaminika kuhusika na ukiukwaji wa haki za binadamu na kuhujumu mchakato wa uchaguzi nchini DRC.

''Maafisa hawa walinufaika kutokana na ufisadi, au kuwazuia watu kuandamana na kuwanyima uhuru wa kujieleza'', iliongeza taarifa hiyo.

## UCHAGUZI WA DESEMBA 30 ULIKUWAJE?

Tume ya Uchaguzi awali ilikuwa imetangaza kwamba felix Tshisekedi alikuwa amepata asilimia 38.5 ya kura, huku Fayulu akijipatia asilimia 34.7.

Mgombea wa chama tawala Emmanuel Shadary alipata asilimia 23.8.

Hata hivyo, Fayulu alihoji kwamba Bw. Tshisekedi alifanya makubaliano na Bw. Kabila ambaye amekuwa uongozini kwa miaka 18. Kabila alikuwa haruhusiwi kuwania muhula mwingine kikatiba.

Kabla ya uchaguzi, kulitokea utata baada ya uchaguzi kuahirishwa katika maeneo yaliyoathiriwa na Ebola yakiwamo miji ya Beni na Butembo Mashariki mwa nchi hiyo, na pia katika jiji la Yumbi Magharibi mwa nchi hiyo.

Hatua hiyo iliathiri takriban wapiga kura 1.26 milioni kati ya jumla ya wapiga kura 40 milioni.

Uchaguzi katika maeneo hayo uliahirishwa hadi mwezi Machi mwaka huu.

## KURA ZAHESABIWA UCHAGUZI ULIOAHIRISHWA


Kura zinaendelea kuhesabiwa nchini Nigeria kufuatia uchaguzi mkuu wa nchi hiyo. Hata hivyo, upigaji kura ulisogezwa kufikia siku ya pili katika maeneo machache.

Kutokana na hitilafu ya mambo, kutokukamilika kwa mipango na vurugu katika baadhi ya maeneo uchaguzi umesogezwa mpaka hapo baadaye.

Wanigeria wanasubiri kwa hamu kumjua rais wao mpya.

**CHINI:** Karatasi ya majina ilikuwa ndefu ili kuweka wagombea wote 73 nafasi ya urais.





Rais Muhamadu Buhari mwenye miaka 76 anatetea kiti chake kwa awamu ya pili. Mpinzani wake mkuu ni Makamu wa Rais wa zamani Atiku Abubakar, 72.

Uchaguzi ulitakiwa kufanyika juma moja lililopita na baadaye kuahirishwa katika dakika za lala salama.

Kwa yeyote atakayeshinda na kukikalia kiti hicho katika taifa hilo lenye watu wengi zaidi Barani Afrika na uchumi mkubwa, atakabiliwa na suala la ukosefu wa nishati ya uhakika, rushwa, tishio la kiusalama na kuporomoka kwa uchumi.

Rais Buhari alipiga kura yake katika mji wa Daura Kaskazini mwa mkoa wa Katsina. Alipoulizwa kama atampongeza mpinzani wake pale atakapoangushwa kwenye uchaguzi huo alisema, ''Nitajipongeza mwenyewe''.

Bw. Abubakar, mfanyabiashara mkubwa, amesema ana imani ya kushinda uchaguzi.

## UCHAGUZI ULIKUWA WA AMANI?

Sehemu kubwa ya nchi hiyo ilionekana kuwa katika utulivu lakini kumekua na taarifa za uwapo wa Kundi la wapiganaji la Boko Haram eneo la Kaskazini. Wapiga kura walitishwa huku wakijaribu kutaka kuiba masanduku ya kura katika sehemu ya vituo, hasa katika mikoa ya Kaskazini, Lagos na Anambra.

Muungano wa makundi ya asasi za kiraia umeripoti kuwa jumla ya watu 16 waliuawa -Idadi mbayo ni ndogo ikilinganiswa na uchaguzi uliopita.

Watu wawili walitiwa kizuizini katika mkoa wa Surulere eneo la mji mkubwa wa kibiashara Lagos, baada ya wapiga kura kuvamiwa na kundi la vijana wadogo wakiwa na silaha kama jambia, shoka na vitu vyenye ncha kali, shuhuda mmoja aliiambia BBC.

Tume ya Uchaguzi yenyewe inasema kuwa uchaguzi haukuwezekana katika vituo 8,500 kati ya vile 120,000 katika eneo lote la nchi, Shirika la Habari la AFP limeripoti.

Mgombea atakayepata kura nyingi atatangazwa kuwa mshindi katika duru ya kwanza ya uchaguzi, na hiyo ni ikiwa atapata asilimia 25 ya kura katika theluthi mbili ya majimbo 36.

Wagombea wa nafasi ya uraisi walikuwa 73, lakini ushindani mzito zaidi ulishuhudiwa kati ya raisi wa sasa Muhamadu Buhari na mfanyabiashara mkubwa nchini humo, Atiku Aboubakar.

Takwimu za Uchaguzi zinaonyesha kuwa waliojiandikisha kupiga kura walikuwa watu milioni 73, idadi ya wagombea nafasi ya urais walikuwa 73 na vituo vya kupigia kura vilikuwa 120,000.

**BBC**

# Kasaka abainisha chimbuko la G55

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 1993 wakati wa Mkutano wa Bunge la Bajeti, liliibuka vuguvugu la kudai kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano. Hatua hiyo ingewezesha kuwapo kwa serikali tatu- Tanzania Bara (Tanganyika), Zanzibar na ile ya Muungano tofauti na serikali mbili ilivyokuwa wakati huo na sasa.

Katika harakati hizo za kudai serikali ya Tanganyika liliibuka kundi la wabunge 55, maarufu kama G55, wote kutoka CCM, chama pekee ambacho kilikuwa na wabunge ndani ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Miongoni mwa wabunge hao alikuwa Njelu Kasaka (Chunya) ambaye alionekana kinara wa jambo hilo kutokana na kuliweka wazi tangu alipokuwa akichangia hotuba ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Wengine miongoni mwao walikuwa Philip Marmo (Mbulu), Jenerali Ulimwengu na Venance Ngula (Taifa), Tuntemeke Sanga (Makete), William Mpiluka (Mufundi), Patrick Qorro (Karatu) na Nassoro Malocho (Newala).

Kwa ujumla, wabunge waliounda kundi hilo walikuwa na uwakilishi mpana kutoka takribani mikoa yote ya Tanzania, jambo ambalo lilionekana kuwa na sura pana ya kitaifa. Hakuna mkoa uliokosa mbunge katika kundi hilo.

Katika kitabu chake cha 'Njelu Kasaka Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika-G55, Kasaka ambaye ndiye alikuwa mstari wa mbele kuwasilisha hoja hiyo ndani ya Bunge, anaweka bayana kwamba kundi hilo kwa moyo mmoja na kwa ari kubwa, walijitoa mhanga kuhakikisha jambo hilo linafanyika.

Kasaka ndani ya kitabu hicho kinachobeba kumbukumbu mbalimbali juu ya vuguvugu hilo, anasema kila mmoja ndani ya G55 alionyesha wazi kuwa alikuwa na dhamira ya dhati kutokana na mambo yalivyokuwa yalitendeka ndani ya serikali.

Wakati akichangia hotuba ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Juni 29, 1993, Kasaka pamoja na mambo mengine alisema katika wakati uliokuwapo muundo wa Muungano ulikuwa haufai na umepitwa na wakati hivyo kuna kila sababu ya kuubadili na kuwa na serikali tatu badala ya mbili.

Katika kujenga hoja hiyo ili kuleta ushawishi, aliweka kwa kinagaubaga mambo au sababu mbalimbali zilizofanya kuwa na ulazima wa kuwa na Muungano wenye sura tofauti na uliokuwapo wakati huo. Mambo hayo, kama yalivyoandikwa ndani ya kitabu hicho. yaliainishwa katika makala iliyopita.

**HOJA YA TANGANYIKA**

Baada ya kuvuma kwa kasi suala la Tanganyika lililohanikizwa na wabunge wa kundi la G55 na vyombo vingi vya habari kulibeba kwa kiwango cha juu, hatimaye Agosti 23, 1993 iliwasilishwa Hoja Binafsi Bungeni.

Akiwasilisha hoja hiyo, Kasaka alianza kwa kusema: "Madhumini ya hoja hii si kuvunja Mungano kama ambavyo baadhi ya watu wangependa ieleweke. Lengo ni kuiwezesha Tanzania Bara iwe na serikali yake kama ilivyo uoande wa Zanzibar.

"Hatua hii tunaamini italeta haki na usawa kwa pande zote zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuondoa manung'uniko kwa wananchi wa Tanzania Bara ambao wanafikiri wamenyimwa haki yao ya kushughulikia masuala ya ndani ya nchi yao bila kuingiliwa na Wazanzibari na pia serikali ya Muungano yenyewe."

> "Haikuchukua muda wabunge 44 walijiorodhesha na kutia saini. Idadi hii ya wabunge ilichukuliwa kuwa ni kubwa ya kutosha kumjulisha Naibu Spika kuhusu kusudio letu la kuwasilisha hoja binafsi,"

Kasaka katika hoja hiyo alibainisha kuwa hali iliyokuwapo ilisababisha wananchi kutoka Tanzania Bara kutopewa nafasi za uongozi katika ofisi za Muungano zilizoko Zanzibar na wakati mwingine Serikali za Mapinduzi Zanzibar kuzuia watumishi wa Muungano kutoka Bara kuhamishiwa Zanzibar.

"Wakati huo huo Wazanzibari wameendelea kuteuliwa kushika nafasi katika serikali ya Muungano kwenye ofisi zake zilizoko Tanzania Bara hata wizara zisizokuwa za Muungano. Wananchi wa Zanzibar na serikali ya Muungano wana uhuru wa kufanya jambo lolote Tanzania Bara bila kuulizwa na wananchi wa Tanzania Bara lakini wananchi wa Tanzania Bara na serikali ya Muungano hawana fursa kama hiyo ndani ya Zanzibar," alisema.

Jambo lingine lililobeba uzito ndani ya hoja hiyo ni wananchi na viongozi kutoka Tanzania Bara kuonekana kama wageni wanapoingia Zanzibar. Wakati huo ilikuwa marufuku kwa mtu kutoka Tanzania Bara kuingia Zanzibar bila kibali lakini wale wa Zanzibar walikuwa huru kuingia Tanzania Bara na hili lilisababisha doa ndani ya Muungano.

"Ni dhahiri kwamba kitendo cha kuwataka (wananchi kutoka Tanzania Bara) waonyeshe pasipoti au kitambulisho cha uraia wa Tanzania Bara hakionyeshi usawa kwa nchi shiriki ndani ya Muungano na kupingana na Ibara ya 17 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema katika hoja hiyo.

Ibara hiyo inabainisha kuwa: "Kila raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo haki ya kwenda kokote ndani ya Jamhuri ya Muungano na kuishi sehemu yoyote; kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano."

Aidha, Kasaka alipinga maoni ya watu, aliyoyaita potofu, kwamba kuundwa kwa serikali ya Tanganyika kungesababisha Muungano kuvunjika na kusisitiza kuwa hayana msingi kwa sababu kuwapo au kutokuwapo kwa serikali ya Tanganyika hakikuwa kigezo muhimu cha kuufanya Muungano uendelee kuimarika.

**KIINI CHA HOJA**

Baada ya kuwapo kwa msisimko ndani na nje ya Bunge juu ya vuguvugu la serikali ya Tanganyika, kundi la kwanza la Wabunge wanane walikutana nyumbani kwa Mateo Qaresi, Upanga jijini Dar es Salaam. Wabunge hao ni Kasaka, Qaresi mwenyewe (Babati), Qorro, Arcado Ntagazwa (Kibondo), Mpiluka, Lumuli Alipipi Kasyupa (Kyela) na Jared Gachocha (Ngara).

Lengo la kikao cha wabunge hao wanane kilikuwa kutengeneza mkakati wa namna ya kutekeleza wazo la kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano.

Kasaka anabainisha kuwa katika majadiliano yao, wabunge walikubaliana wajiunge kuwa kamati ya majadiliano ya kusukuma mbele ajenda ya kuundwa kwa serikali ya Tanganyika na yeye alipewa jukumu la katibu na mratibu wa mchakato huo na Qaresi kuwa mwenyekiti. Moja ya mambo waliyokubaliana ni kuhakikisha suala hilo linawasilishwa bungeni na kujadiliwa.



Anasema kuundwa kwa kamati hiyo ilikuwa hatua ya kwanza ya utekelezaji wa hoja ya Tanganyika huku ya pili ikiwa kushawishi wabunge wengine waunge mkono kwa vitendo.

Hatua ya tatu ilikuwa kufikisha pendekezo hilo kwa Naibu Spika (wakati huo), Pius Msekwa, juu ya kuwasilisha hoja binafsi Bungeni. Msekwa ndiye aliyekuwa akiongoza vikao vya Bunge kutokana na aliyekuwa Spika, Chifu Adam Sapi Mkwawa, kuwa na matatizo ya kiafya. Sapi kwa sasa ni marehemu.

**KUNDI LA G55**

Baada ua mkutano wa wabunge wanane Upanga, nyumbani kwa Qaresi, Kasaka anasema akiwa katibu na mratibu wa mchakato, aliandaa karatasi ambayo ilizungushwa kwa wabunge kuwataka wale wanaounga mkono jambo hilo waandike majina yao na kutia saini.

"Haikuchukua muda wabunge 44 walijiorodhesha na kutia saini. Idadi hii ya wabunge ilichukuliwa kuwa ni kubwa ya kutosha kumjulisha Naibu Spika kuhusu kusudio letu la kuwasilisha hoja binafsi," anasema.

Awali, Kasaka anasema Naibu Spika aliwaeleza kuwa hoja binafsi ingewezekana mradi tu izingatie matakwa ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya hapo, anasema alitekeleza hilo kwa kutayarisha hoja na kuambatanisha na majina ya wabunge waliojiandikisha na kutia saini.

Baada ya hapo, anasema Naibu Spika alitangaza hoja kwa waandishi wa habari na kuijulisha serikali na vyombo vya habari vilipotangaza, umma ilipata taarifa na ari ya wananchi juu ya kufufuliwa kwa hoja ya Tanganyika ilikuwa kubwa sana.

"Mahudhurio ya wananchi katika viwanja vya Karimjee ambako vikao vya Bunge vilikuwa vikifanyika, yaliongezeka siku hadi siku. Hatukujua kwamba suala la Muungano, hasa kurudishwa kwa serikali ya Tanganyika, lilikuwa na mvuto wa kiasi hicho," anabainisha.

- **Nini kilitokea baada ya Naibu Spika kutangaza kuwapo kwa Hoja ya Tanganyika? Fuatilia makala ijayo upate undani wake na yote yaliyomo ndani ya kitabu chake.**

# Korea Kusini na somo kwenye ubunifu Tanzania ya Viwanda

Na Mashaka Mgeta

KOREA Kusini imeendelea kushika nafasi ya kwanza ya ubunifu unaokuza uchumi na maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo, kwa mujibu wa tathmini ya ubunifu inayofanywa na taasisi ya Bloomberg ya Marekani.

Ripoti ya tathmini hiyo iliyofanyika mwaka jana na kuchapishwa Januari 22, mwaka huu, imetumia takwimu zilizokusanywa kutoka mashirika ya kimataifa yakiwamo Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD).

Kampuni 'iliyoibeba', Korea Kusini katika tathmini hiyo ni Samsung, inayojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali hususani za kielektroniki zinazotumia sayansi na teknolojia bunifu.

Tathmini ya Bloomberg, inaonyesha kuwa tangu kuanza kwa kipindi cha millennia, nembo ya biashara ya kampuni hiyo, imetumika kwa makubaliano ya kibiashara kwenye mataifa makubwa hasa Marekani kuliko ilivyo kwa kampuni nyingine, isipokuwa IBM.

Tathmini ya Bloomberg iligusia maeneo saba yakiwamo utafiti na maendeleo, utengenezaji bidhaa, kampuni zinazojihusisha na vifaa vya teknolojia ya juu, kiwango cha usaili katika sekta ya elimu na watafiti na shughuli zinazohusiana na hatimiliki.

Katika tathmini hiyo, Korea Kusini imeshika nafasi ya kwanza katika kundi la hatimiliki na nafasi ya pili katika utafiti na maendeleo na ongezeko la thamani katika uzalishaji wa bidhaa.

Pia imeshika nafasi ya 21 katika uzalishaji, ikitoka nafasi ya 32 iliyokuwapo katika taarifa iliyotolewa mwaka jana.

"Serikali ya Korea Kusini itajitahidi kufanikisha huduma za uzalishaji wa ndani ya nchi ambao ni mdogo kuliko wa sekta ya viwanda ili iweze kuboresha ndani ya kipindi mahususi," taarifa ya Wizara ya Fedha ya nchi hiyo imesema baada ya kuchapishwa taarifa ya Bloomberg.

Tathmini hiyo inaonyesha kuwa Korea Kusini imefuatiwa na Sweden iliyopata alama 84.7, Singapore ikisogea kutoka nafasi ya sita hadi ya tatu kwa kuwa na alama 83.05 wakati Japan ikishika nafasi ya sita kwa alama 81.9.

Marekani ambapo taasisi hiyo ya Bloomberg ina Makao Makuu yake, imeshika nafasi ya 11 kwa kuwa na alama 80.42 na China inaonekana kushika nafasi ya 19 kwa kuwa na alama 73.36.

Ubunifu kwa asili yake unaweza kutafsiriwa kwa namna tofauti lakini zaidi ukihusu utengenezaji wa bidhaa na huduma kwa namna inayoyafanya maisha kuwa bora, na kwa kuhusisha sekta mtambuka.

Kwa hali hiyo, nchi yoyote inayotaka kupiga hatua za maendeleo katika sekta na nyanja tofauti ni vema ikawekeza na kuendeleza utamaduni wa ubunifu, ingawa si jambo rahisi hivyo ushirikiano na uhusiano mwema kati ya nchi zilizo nyuma kwa ubunifu wa teknolojia na zile zilizopiga hatua ni jambo lenye maana pana.

### MCHAMBUZI

Mchambuzi wa masuala ya sera, Kasmir Thomas, anasema hali kama hiyo inapaswa kufanyika hapa nchini kwa kuanzia na uboreshaji zaidi wa sera ili zitambue nafasi ya ubunifu katika mchakato wa uchumi na maendeleo.

"Sera zinazotuongoza katika maeneo tofauti yakiwamo ya uzalishaji, viwanda na kwingineko, zitamke bayana namna ubunifu unavyochukua nafasi katika kuleta mabadiliko na mageuzi," anasema.

Pia anasema, kwa kadri ya ripoti hiyo, ipo haja kwa Tanzania kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na mataifa mbalimbali, lakini zaidi kuwa na mkakati mahususi na Korea Kusini inayoonyesha mafanikio katika nyanja kwenye sekta tofauti.

Kasmir anasema taarifa ya Bloomberg imechapishwa wakati ambapo serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, ipo katika utekelezaji wa azma ya kuingia uchumi unaotegemea ama kutokana na sekta ya viwanda, hivyo suala la teknolojia bunifu si la kupuuzwa.

"Ndio, tunaweza kwenda haraka na kupata mafanikio makubwa kwa kipindi kifupi kuhama kutoka uchumi unaotegemea kilimo kwenda ule wa viwanda, lakini hili halitawezekana kwa urahisi kama nchi haitawekeza kwenye ubunifu hasa kwa utafiti na maendeleo katika ngazi na nyanja tofauti," anasema.

### WAJASIRIAMALI

Kiongozi wa kikundi cha wajasiriamali wanaokuza mitaji yao, Milembe Lameck anasema uwekezaji katika teknolojia bunifu unapaswa kuelekezwa katika bidhaa zinazohusika katika sekta ya kilimo yenye kuzalisha malighafi nyingi zinazohitajika kwenye soko la ndani na nje ya nchi.

"Ubunifu una nafasi kubwa katika mchakato wa mageuzi ya kiuchumi na maendeleo, kuanzia uboreshaji wa thamani za bidhaa na huduma na kuongeza fursa za usambazaji kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi," anasema Milembe.

Ni kwa hali hiyo, anashauri kwamba Tanzania inapaswa kuchukua hatua na jitihada muhimu kuhakikisha kwamba ushirikiano na uhusiano dhidi ya Korea Kusini unatumika kufanikisha ubunifu hasa wa kiteknolojia kwa nchi na watu wake.

Mathalani, hapa nchini kuna taasisi kama Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) yenye dira inayoelezea kuwa mwongozaji ama mtoaji wa ubunifu katika sayansi na teknolojia kwa ajili ya maendeleo endelevu.

COSTECH ina jukumu, pamoja na mengine, kueneza, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utafiti wa kisayansi na maendeleo ya teknolojia na kuwezesha ushirikiano katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kadri ya maeneo husika.

Kwa mujibu wa taarifa inayopatikana kwenye mtandao wake, COSTECH mamlaka ya kupata, kuhifadhi, kusambaza na kuzieneza taarifa za kisayansi na teknolojia kwa umma.

Ni kwa mukhtadha huo, COSTECH inakuwa moja ya taasisi muhimu katika ubunifu wa teknolojia na katika masuala mengine ya maendeleo.

Ni mwendo wenye azma njema ingawa bado kunahitajika kuzidi kujifunza kwa waliopiga hatua kama Korea Kusini.

Kwa maana mafanikio ya Korea Kusini, nchi ambayo takwimu zinaonyesha kuwa katika miaka ya mwanzoni mwa 1960, uchumi wake ulikuwa sawa na baadhi ya nchi zinazoendelea kama Tanzania, na wakati huo ilitoka kwenye vita ya muda mrefu dhidi ya Korea Kaskazini yanapaswa kuwa 'darasa' katika kuyafikia maendeleo.

Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na namna ilivyofanikiwa kutumia mbinu bunifu ikiwamo kuwekeza katika utafiti na maendeleo, hivyo kuchangia kuendelea kushika nafasi ya kwanza katika tathimini ya Bloomberg.

### PROFESA WA UCHUMI

Profesa wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha California nchini Marekani, Bronwyn Hall, amekaririwa akisema kwenye nchi ambazo wanasayansi wengi ni watumishi wa umma serikalini, wana nafasi ndogo ya kutoa matunda ya kazi zao (utafiti) hivyo kuifanya jamii isinufaike.

Profesa Hall anasema kwamba kwa nchi kama Korea Kusini, kampuni zinazowekeza kwa tija katika utafiti zikiongozwa na Samsung, zimechangia kuboresha uchumi wa taifa hilo.

Akitoa mfano katika kipindi cha 2014, kampuni hiyo ilitenga Dola bilioni 14 za Marekani kwa matumizi ya utafiti na maendeleo kwa mwaka mzima.

Hivyo wakati Tanzania ikichagiza kasi ya mageuzi ya kiuchumi kuelekea uchumi wa viwanda na kuibuliwa kwa miradi mikubwa ya maendeleo, ipo haja ya 'kutupia jicho' nyanja ya ubunifu na kwa hali hiyo, Korea Kusini inapaswa kuwa mshirika wa karibu.

Lakini lipo somo linalotokana na mafanikio ya Korea Kusini, kwamba ushirikiano wa karibu kati ya serikali na sekta binafsi, umechagiza kuendelea kupatikana kwa mafanikio hayo.

Kuibuka kwa kampuni ya Samsung kulikoifanya Korea Kusini iongoze katika tathmini ya Bloomberg kwa mwaka jana, kunaweza kutoa ishara ya umuhimu wa ushirikiano usiotiliwa shaka kati ya serikali na sekta binafsi, na mwisho wa siku, taifa litapiga hatua hasa katika maendeleo ya kiuchumi na kwa kutegemea zaidi ubunifu kwenye sayansi na teknolojia.



Rais wa Korea Kusini, Moon Jae-In. **PICHA: MTANDAO**

MAKALA

# Ugaidi wazifikisha Pakistan, India ukingoni, ila hofu ya vita si kubwa

**Na Ani Jozeni**



Waziri Mkuu wa India, Narendra Modi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KUNDI la kigaidi la Jaesh e-Mohammad la Pakistan, ambalo kinadharia limepigwa marufuku lakini ni moja ya makundi ya siasa kali yenye nguvu nchini humo limeifikisha nchi hiyo kukaribia kuingia vitani na India, baada ya shambulio la kujitolea mhanga jimbo la Kashmir, ambako zaidi ya wanajeshi 40 wa India walikufa.

Ni hali ya uchokozi wa kudhamiria wa kundi hilo la kigaidi linalojua kuwa lina maeneo linayoshika nchini humo, sawa na makundi mengine kama Taliban iliyo na nguvu Afghanistan na Pakistan, na hivyo serikali haiwezi kuchukua hatua yoyote.

Isitoshe, kuiingiza Pakistan vitani na India, hata kwa kiasi tu, kutasaidia ugaidi kupata nguvu zaidi.

Pamoja na kuwa demokrasia inashamiri India na kwa kiasi kikubwa nchini Pakistan vile vile, nchi zote mbili zina makundi ya kigaidi yenye sura tofauti, huku vyama vya kisiasa na makuhani wengi wakiwa na mahusiano ya wazi na makundi hayo.

Pakistan kwa mfano ni nchi iliyoundwa kwa kuigawa Himaya ya India ya wakati wa ukoloni ili Waislamu wawe na nchi yao na Wahindu watawale India, licha ya kuwa katika miaka iliyofuata, India ilibaki kuwa taifa lenye idadi kubwa zaidi ya Waislamu kuliko kwingine, hata Indonesia.

Tangu iundwe Pakistan wakati India ikifikia uhuru mwaka 1947, mzozo wa mpaka haujaisha, kwani eneo la Jammu na Kashmir Kaskazini ya India limegawanyika kidini, likagawanywa kwa tabu nchi hizo zikivutana liwe la nchi ipi.

Wakati nchi zote mbili zinatishiwa na ugaidi na zina makundi tofauti, India ina makundi maridhawa ya kigaidi ambayo yanashambulia taasisi za nchi au za usalama nchini humo, wakati makundi ya Pakistan yanapenda zaidi kushambulia India ili kurudisha maeneo Pakistan inayotaka.

Wachunguzi wa habari wanasema serikali ya Pakistan kwa miaka mingi, licha ya kuwa na mawaziri wakuu tofauti, kwa jumla haipendi kuchukua hatua kwa vikundi vya kigaidi vinavyofanya mashambulio nchini India kwani nchi hizo ni maadui wa jadi.

Wakati India inatafuta njia ya kujibu shambulio hilo, Pakistan ilionya kuhusu kuchukua hatua za kijeshi, ikataka majadiliano.

Maofisa wa kijasusi na kidiplomasia wa Marekani wanasema kuwa kitengo cha ujasusi cha jeshi la Pakistan (ISI - Inter-Services Intelligence) ambacho kinafahamika kwa ukaribu wake na vikundi vya kigaidi nchini humo, kilihusika katika shambulio hilo.

ISI walilaumiwa sana na Marekani mwaka 2011 wakati Marekani ilipofanya shambulio la makomandoo walioshuka kwa helikopta katika nyumba alikokuwa amejificha gaidi nambari moja, Osama bin Laden huku opereshseni hiyo ikiangaliwa na Rais Barack Obama na mawaziri, wasaidizi wakuu wa masuala ya ulinzi na usalama Ikulu.

Nyumba hiyo ilikuwa kando kando ya kambi ya chuo kikubwa cha kijeshi.

Wakati siku 10 zilikuwa zimeshapita bila hatua kuchukuliwa dhidi ya kundi hilo au Pakistan kama nchi, wachunguzi wa habari walisema kuwa ni lazima Pakistan iadhibiwe kwa shambulio hilo.

Ingekuwa ni kundi hilo limefanya shambulio kivyake na hakuna ushahidi kuwa jeshi au taasisi tanzu zilihusika, India ingeangalia kama inaweza kufanya shambulio la anga dhidi ya maskani ya vikundi vya kigaidi karibu na mpaka wa Jammu na Kashmir, kama ilivyopata kufanya awali.

> Ndiyo maana India inapendelea zaidi kuleta mazingira mapana ya kutengwa kwa Pakistan kimataifa, huku ikigwaya kuchukua hatua za wazi za kijeshi dhidi ya jeshi la Pakistan au kambi yoyote ya kigaidi.



Waziri Mkuu wa Pakistani, Imran Khan.

Inaweza pia kuchukua hatua kama hiyo lakini kuna uwezekano wa kulishambulia jeshi la Pakistan ili serikali ya nchi hiyo itambue kuwa kuunga mkono ugaidi pia kuna gharama.

Shambulio hilo linaonekana kuingilia kati ratiba za kisiasa za nchi hizo mbili kwa njia tofauti, kwani kwa upande wa Pakistan inaonekana shambulio hilo ni njama za ISI na Jaesh e-Mohamad za kuihujumu serikali ya mcheza kriketi mstaafu Imran Khan.

Ingawa aliungwa mkono na jeshi baada ya Mahakama kumtia hatiani waziri mkuu aliyepita Nawaz Shariff ambaye amewahi kutawala miaka ya nyuma akaondolewa madarakani na jeshi, makundi ya siasa kali ikiwemo ISI hawapendi serikali za kiliberali zinazosikiliza nchi za Magharibi.

ISI imekuwa mwiba katika uhusiano wa Marekani na Pakistan kwani ina nguvu sana jeshini na ni swahiba mkubwa wa magaidi.

Serikali ya Imran Khan inajua kuwa haina ubavu wa kuliingilia jeshi na kutafuta wafuasi wa makundi ya kigaidi kwani hatua kama hiyo inaweza kumfikisha waziri mkuu huyo kupigwa risasi kama alivyouawa waziri mkuu Benazir Bhutto akiwa katika vita ya wazi na jeshi, kuhusu ugaidi, rushwa, n.k.

Matamshi yake baada ya tukio hilo yameonyesha kutochukulia maanani kwa kiwango kikubwa uzito wa suala hilo, kuuawa kwa askari 40 na zaidi wa India kwa shambulio la kukusudia likiungwa mkono na jeshi la Pakistan, au taasisi yake mojawapo.

Lugha ya kufanya majadiliano nini cha kufanya maana yake ni kuwa mzozo wa msingi wa Jammu na Kashmir ndiyo tatizo halisi, msimamo unaomaanisha kuwa mradi tatizo hilo lipo lolote linaweza kutokea kati ya nchi hizo mbili.

India kwa upande wake iko katika kipindi cha maandalizi ya uchaguzi mkuu, na kama Waziri Mkuu Narendra Modi hachukui hatua stahiki dhidi ya Pakistan inaweza kutumiwa na wapinzani, hasa vikundi vya uzalendo wa kupania kuwa ni dhaifu, n.k.

Tatizo kwa upande wa serikali ya India ni kubuni au kufikia tamati ni aina gani ya mashambulio yanaweza kufikia lengo lake, kwani adui ametawanyika na hakuna uhakika India inataka kutoa somo kwa kundi gani hasa.

Kama ni Jaesh e-Mohamad hawahitaji somo kwani watafurahi kama hali ya utulivu itapungua, mtafaruku uongezeke na uzalendo uinuliwe zaidi Pakistan, kwani kwa hali hiyo ugaidi utafuzu zaidi.

Kwa upande wa pili India ingependa serikali ya Imran Khan nchini Pakistan iweze kuwa na nguvu kuleta mabadiliko jeshini na kwingineko, hivyo hatua ya kuanza mashambulizi ya kijeshi itailazimisha serikali hiyo kuvielemea vyombo na taasisi za ulinzi na usalama.

Katika hali kama hiyo hakuna mipango yoyote ya mageuzi inayowezekana hata kama Imran Khan siyo mwanamageuzi kivile na alitegemea pia kuungwa mkono na jeshi kuingia madarakani.

Ndiyo maana India inapendelea zaidi kuleta mazingira mapana ya kutengwa kwa Pakistan kimataifa, huku ikigwaya kuchukua hatua za wazi za kijeshi dhidi ya jeshi la Pakistan au kambi yoyote ya kigaidi.

Katika juhudi za kuitenga Pakistan ni wazi Marekani pekee ndiyo inayounga mkono mapendekezo hayo, kwani utawala wa Rais Donald Trump umeondoa sehemu kubwa ya ushirikiano wa kijeshi na Pakistan kutokana na undumila kuwili wa jeshi la Pakistan, kupambana na ugaidi na kuusaidia.

China iliwahi kuzuia juhudi za kutangaza kundi la Jaesh e-Mohamad kama kundi la kigaidi katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, wakati Russia inachukia ugaidi lakini uhusiano kati ya nchi hizo mbili una mashaka hasa kutokana na ukaribu wa serikali ya kiliberali ya Modi yenye uhusiano mzuri na Marekani.

Isitoshe Russia ni mshindani wa China katika maeneo kadhaa na China imekuza kwa haraka uhusiano wake na India, wakati ambapo Russia imeshindwa kukuza biashara na India kama China na hasa nchi za Magharibi, Ghuba au Asia ya Mbali.

Jumla ya biashara kati ya India na Russia ni dola bilioni 10 wakati ni zaidi ya dola bilioni 100 biashara na Marekani kwa upande mwingine.



## RC aibua mkakati ujenzi madarasa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewaagiza watendaji wa vijiji na kata mkoani Mbeya, kushirikiana na viongozi wa shule kuandaa kanzi data za wanafunzi waliowahi kusoma kwenye kila shule ili wasaidie kwenye ujenzi wa miundombinu ya shule hizo.

Alitoa agizo hilo jana wilayani Chunya wakati wa ziara ya kukagua shughuli za maendeleo ikiwemo ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa vituo vya afya na zahanati pamoja na kutembelea baadhi ya migodi ya dhahabu ili kujua shughuli zinazofanyika.

Chalamila alisema shule zote za msingi na sekondari zinatakiwa kuwa na orodha ya wanafunzi waliowahi kusoma kwenye shule husika na kujua waliko ili wakati wa ujenzi au uboreshaji wa miundombinu ya shule husika wawe wanahusishwa.

Alisema baada ya kukamilisha orodha ya wahitimu wa shule hizo ni lazima bodi na kamati za shule zifanye kazi ya kuwasiliana nao ili kuwashirikisha kwenye shughuli za ujenzi.

"Tunataka bodi na kamati za shule ambazo zinajua majukumu yao, hatutaki bodi za watu ambao wanakuja kukaa na kudai posho tu, hawa wanafunzi tukichukua Sh. 5,000 zao au kila mmoja akatuchangia mfuko wa sementi tutajikuta tunajenga vyumba vingi vya madarasa," alisema Chalamila.

Aidha aliwataka wazazi na walezi kushirikiana na viongozi wa shule pamoja na serikali katika kuboresha mazingira ya shule kwa ajili ya watoto wao ili kuinua kiwango cha ufauru.

Alisema mwaka huu mkoa wa Mbeya ulikuwa unakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa 143 kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza na kwamba kuchelewa kukamilika kwa vyumba hivyo pia kulipelekea wanafunzi 6,225 kuchelewa kuanza masomo.

Akisoma taarifa ya maendeleo ya elimu ya wilaya hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, alisema mwaka huu wilaya yake ilikuwa na uhaba wa vyumba vya madarasa vinne kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Alisema kwa sasa tayari vyumba hivyo vilishakamilika na wanafunzi tayari wameshaanza kusoma na kwamba kwa sasa wanaendelea kufuatilia ili kuhakikisha wanafunzi wote waliofauru mitihani wanaendelea na masomo.

Alisema kwa upande wa shule za msingi wameandikisha wanafunzi wa darasa la kwanza zaidi ya 6,000 sawa na asilimia 112 ya malengo waliyokuwa wamejiwekea ya kuandikisha wanafunzi 5,000.

"Wananchi wengi wana mwamko wa kuandikisha watoto wao shule kwa sababu ya utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo, mwaka huu tumeandikisha watoto wengi kuliko tulivyokuwa tunatarajia," alisema Mahundi.

Aidha kuhusu usimamizi wa rasilimali madini za wilaya hiyo alisema, wao kama serikali watahakikisha wanasimamia na kuhakikisha hakuna utoroshaji unaofanywa.

# Mwili wazikwa baada ya miezi tisa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWILI wa kijana Frank Kapange (22) ambao ulikuwa umetelekezwa kwa miezi minane na siku 26 katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na wanafamilia kutokana na mvutano wao na Jeshi la Polisi, umechukuliwa na kwenda kuzikwa.

Wanafamilia wa kijana huyo waligoma kuchukua mwili huo baada ya kufariki dunia katika mazingira ya kutatanisha wakidai Jeshi la Polisi linahusika na kifo chake hali iliyofanya wapeleke kesi mahakamani kwa ajili ya kusaka haki.

Akizungumza hosptalini hapo jana, msemaji wa familia ya Kapange, Julius Kapange, alisema wameamua kuchukua hatua kutokana na uamuzi wa mahakama uliowataka wazike ndani ya wiki moja kabla ya kufanyika uamuzi mwingine.

Kapange alisema mahakama iliamua kuwa endapo wangeendelea kugoma kuuchukua mwili huo, ingeamuliwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kutekeleza jukumu la kuuzika, hivyo wakaona haitakuwa vyema.

"Tunaenda kuzika kijijini kwetu Syukula, Rungwe. Tumefanya hivi kutokana na amri ya mahakama ambayo ilitutaka tuzike ndani ya wiki moja. Lakini pia tumeona si vyema kuendelea kuutesa mwili wa kijana wetu," alisema Kapange.

Hata hivyo, alisema familia haikuridhishwa na uamuzi wa mahakama kwa madai kuwa haikuwatendea haki kwenye uamuzi wa kesi hiyo ambayo imechukua miezi minane.

Aidha, alisisitiza kuwa kijana wao katika historia ya maisha yake hakuwahi kuwa na matukio ya ovyo na alikuwa mtafutaji hali inayowafanya wanafamilia kuona kuondoka kwake ni pigo kubwa.

Vilevile alisema wanafamilia wanaushukuru uongozi wa hospitali ya Kanda ya Rufan ya Mbeya chini ya Mkurugenzi wake, Dk. Godlove Mbwanji, kwa upendo walioonyesha wakati wote wa tatizo hilo.

Alisema mwishoni mwa wiki iliyopita waliitwa na Dk. Mbwanji na kukaa nao kwa ajili ya mazungumzo kisha akawataka wachukue mwili wakazike huku akiwasamehe gharama zote za kuhifadhi mwili huo tangu mwanzo.

"Sisi tulienda mahakamani kuomba mwili wa mtoto wetu uchunguzwe kutokana na mazingira ya kifo chake kuwa ya utata na wala hatukuususa mwili huo kama inavyotafsiriwa na baadhi ya watu ambao hawatutakii mema," alisema Kapange.

Alisema kwa sasa wataendelea na shuguli zao za kawaida baada ya mazishi na kwamba suala hilo wanaachana nalo kutokana na walivyohangaika kwa muda mrefu.

Akizungumza kwa njia simu, Dk. Mbwanji alisema wameamua kusamehe gharama za kutunzia mwili kwa muda wote ili kuwasaidia wanafamilia hao kupunguza baadhi ya machungu yanayowakabili.

Alisema uongozi wa hospitali umeona usamehe gharama hizo ili kama wanafamilia hao waliandaa malipo hayo wakazitumie fedha hizo kwa ajili ya kuendeshea msiba.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi (kushoto), akipokea madarasa mawili yaliyojengwa na benki ya CRDB na madawati 40 kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Musa Nsekela, katika hafla iliyofanyika mkoani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba kurudishiwa eneo la hifadhi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Kata ya Matundasi, Chunya mkoani Mbeya, wameomba kurudishiwa eneo lililochukuliwa na serikali kuwa Hifadhi ya Mbiwe maarufu kwa jina la Kung'utasi.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero mbalimbali ulioitishwa na Diwani wa Kata hiyo, Kimo Choga, walisema watu wameongezeka, hivyo eneo wanaloishi halitoshi.

Mmoja wa wananchi hao ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Matundasi A, Masaga Kaloli, alisema wanatamani kwenda kumwona Rais John Magufuli kuomba wapewe eneo linalodaiwa kuwa la Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) akidai kuwa eneo hilo halina wanyama.

Alisema katika hifadhi hiyo hata kumkuta sungura ni vigumu lakini wananchi wakifanya shughuli za kilimo wanachapwa bakora na maofisa wa TFS hali ambayo ni unyanyasaji.

"Eneo hilo tunalolitaka kwa sasa ndilo eneo ambalo miaka ya nyuma tulikuwa tunaishi na wakati wa Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere alitangaza Ujamaa, wazazi walijikusanya sehemu moja na baada ya hapo serikali ikalichukua kama hifadhi," alisema Kaloli. Naye Anyimike Sakalavi alisema eneo hilo linaloombwa lipo umbali wa mita 200 kutoka barabara kuu na ni rahisi wananchi kufanya shughuli zao lakini wakithubutu wanakamatwa.

Alisema kutokana na ongezeko kubwa la watu ndani ya kata hiyo, wameshindwa hata kutekeleza sera ya viwanda kwa kuwa hakuna meneo ambayo wanaweza kuwekeza kwa kujenga viwanda na kutii agizo la Rais Magufuli.

"Kila siku tunaambiwa tuanzishe viwanda sasa kwa hapa wananchi wa Matundasi hatuwezi kwani eneo ni dogo sana, hivyo tunaiomba serikali, eneo lililochukuliwa liachiwe kwa wananchi tuendeleze shughuli za uzalishaji," alisema Sakalavi.

Diwani wa Kata hiyo, Choga alisema suala hilo limekuwa ni kero pia kwake japo amekuwa akilizungumza kila siku kwenye vikao vya baraza la madiwani ili kusaidiwa.

Alisema amejitahidi kuonana na maofisa wa mistu kuzungumza nao juu ya eneo hilo kutwaliwa kwa wananchi lakini imekuwa vigumu kwa kuwa toka Rais Magufuli atoe kauli hiyo ya kuzifuta hifadhi zisizokuwa na maana bado haujatolewa.

Choga alisema eneo linaloombwa na wananchi awali lilikuwa likitumika kama makazi na hadi sasa bado kuna misingi ya nyumba, makaburi, mbaki ya nyumba na mashamba ambayo wananchi walikuwa wakilima kabla hawajahamishwa.

"Ukweli kwa sasa eneo hili la Matundasi ni dogo sana kwani kuna ongezeko kubwa sana la watu na mifugo hivyo kwa sasa wakulima wamekuwa wakigombana kila siku na wafugaji huu ya maeneo ya kulima na kufugia na hata wachimbaji wamekuwa wakifanya shughuri zao katika maeneo ya makazi," alisema Choga





# Watuhumiwa wa kughushi risiti za EFD mahakamani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATUHUMIWA watano wa kesi ya uhujumu uchumi wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Dodoma na kusomewa mashtaka 19 yanayowakabili likiwamo la kughushi risiti za mashine za kielektroniki (EFD) na kuisababishia serikali harasa ya zaidi ya Sh. milioni 700.

Akisoma maelezo ya kesi hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Anord Kirekiano, Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Mkoa wa Dodoma, Salome Mgesani, aliwataja washtakiwa katika kesi hiyo kuwa ni Baldi Mushi, Jerome Mushi, Arif Said, Kasiki Mtiso na Kelvin Mbando.

Alidai Septemba 8, 2018 na Februari 4, 2019, washtakiwa namba moja hadi tatu wote kwa pamoja walifanikiwa kufanya mpango wa uhalifu kwa kughushi risiti bandia za EFD zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 700.

Aidha, alisema washtakiwa hao pia mnamo Februari 3, 2019, katika maeneo ya kisasa walikutwa wakifanya udanganyifu kwa kughushi risiti bandia za mashine za kielektroniki.

Katika kesi hiyo washtakiwa wawili ambao ni Kasiki Mtiso pamoja na Kelvin Mbando, walikuwa wakitetewa na Wakili wa Utetezi Godfrey Wasonga ambaye aliimwomba hakimu wateja wake wapatiwe dhamana kutokana na makosa yao kutohusisha na uhujumu uchumi.

Wasonga alisema wateja wake walikuwa ni mawakala wa mashine hizo kutoka kampuni ya Complynx Supply na katika makosa hayo 19 hakuna sehemu ambayo imeonyesha mtuhumiwa namba nne na tano wanakabiliwa na kosa la uhujumu uchumi.

Katika majadiliano hayo, mwendesha mashtaka wa serikali alimweleza hakimu huyo kuwa kutokana na kesi hiyo kuletwa mahakamani hapo kwa kosa la uhujumu uchumi, washtakiwa wote hawapaswi kupatiwa dhamana.

Hata hivyo, Hakimu Kirekiano, akijibu hoja hizo alisema kuwa pamoja na kuwa mahakama hiyo bado haijapata kibali cha kusikiliza kesi hiyo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, Mahakama haiwezi kuzuia haki zingine kuendelea kutolewa.

"Kama inaonekana kuwa kuna mtu anayo haki ya kupata dhamana basi taratibu zifuatwe, lakini kwa suala la dhamana kwa washtakiwa hawa wawili inabidi mfanye utaratibu Mahakama Kuu muone jaji sio katika mahakama hii," alisema.

Hakimu huyo aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 8, mwaka huu.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhandisi Joseph Nyamhanga, akifungua mkutano wa maboresho ya programu ya usimamizi wa fedha za umma, ulifanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ma-RAS watakiwa kusimamia makusanyo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAKATIBU Tawala wa mikoa nchini (RAS), wametakiwa kusimamia kwa karibu makusanyo kwenye mamlaka zao za serikali za mitaa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamhanga, wakati wa kufungua mkutano wa siku moja wa wasimamizi wa programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma nchini, uliofanyika jijini hapo.

Nyamhanga alisema pamoja na kusimamia, lakini wanatakiwa kudhibiti matumizi yote.

"Tumeona maeneo mengi kuna upungufu kwenye ukusanyaji wa mapato ya fedha za ndani, hivyo ninawataka makatibu tawala wote wa mikoa kuhakikisha mnasimamia ukusanyaji wa mapato yote ya fedha za serikali kwenye maeneo yenu," alisema.

Nyamhanga alisema mpango huo ni wa miaka mitano na ulianza kwenye bajeti ya 2014/2015, unatarajiwa kufikia mwisho mwaka 2022.

Alisema lengo la serikali kuanzisha mpango huo ilikuwa ni kudhibiti mapato yote ya serikali yanayokusanywa kwenye maeneo mbalimbali nchini na matumizi yake.

Naye, mwenyekiti mwenza wa wadau wa maendeleo wanaochangia mpango huo kutoka DFID, Oliver Blake, alisema wanaishukuru serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na John Magufuli kwa kufuatilia mapato na matumizi ya fedha za serikali.

Blake alisema wadau wanaridhishwa na matumizi ya fedha zinazotolewa na wadau, hivyo watumishi wengine wanatakiwa kuunga mkono serikali kwa kudhibiti mapato yote.

Aidha, alisema mikutano hiyo ina lengo la kukaa pamoja na kujadiliana ili kubaini changamoto zilizojitokeza na mafanikio ya mpango huo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia fedha za Serikali za Mitaa, Shomari Mukhandi, alisema tangu kuanzishwa kwa mpango huo wa makusanyo serikali kwa njia ya kielektroniki umesaidia kuongeza mapato.

Alisema makusanyo ya serikali yamekuwa yakipanda mwaka hadi mwaka kutoka mifumo hiyo na mwaka jana mapato ya halmashauri nchini yalikuwa Sh. bilioni 687 yamepanda hadi kufikia zaidi ya Sh. bilioni 735 katika bajeti ya mwaka 2018/19.

Alitaja faida nyingine ya mfumo huo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki umewezesha asilimia 90 ya halmashauri nchini kupata hati safi kwenye ukaguzi wa mahesabu.

# Changamoto za mazingira ya biashara zatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI Msaidizi, Idara ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Uwekezaji Ofisi ya Waziri Mkuu, Christopher Mramba, amesema utitiri wa kodi, leseni, vibali na ada ni miongoni mwa maeneo yenye changamoto katika uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini.

Hata hivyo, alisema serikali imeanza kuboresha mazingira hayo kwa kuondoa na kufuta tozo mbalimbali.

Mramba alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika Mkutano wa Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu wa taasisi zinazotekeleza mpango kazi jumuishi wa kuboresha mazingira hayo uliofanyika jijini hapo.

Mpango huo ni wa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21 na umeandaliwa na wizara, taasisi za serikali na sekta binafsi kwa kushirikiana na mtaalamu mwelekezi ambaye ni Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF).

Akizungumza katika mkutano huo ambao utekelezaji wa mpango kazi huo unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mramba alisema eneo hilo ndio linaloiangusha serikali.

"Hili ndio eneo linalotuangusha sana hata katika taarifa ya mwaka huu ya wepesi kwenye ufanyaji biashara mtaona ni eneo linalohitaji kufanyiwa kazi sana," alisema.

"Kwasababu sheria na kanuni zinazoweka kodi, leseni, vibali, na tozo mbalimbali zote pengine zimepitwa na wakati na bado tunazishikilia kwa wale ambao tupo upande wa serikali," alisema.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya tano imeendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni nyenzo muhimu ya kufikia malengo ya kujenga uchumi wa viwanda na kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, alisema watapokea taarifa kutoka kwa mtaalamu mwelekezi na kujadili.

"Tujadili kwa uhalisia wake, tuna tatizo kubwa sana siogopi kusema na wala simung'unyi maneno, kwamba kuna tatizo la kufunika funika huu ni mpango kazi utaenda kutekelezwa," alisema.

Mwaluko aliongeza: "Usije ukafurahia umeweka malengo ya kutufurahisha wakati kiuhalisia hilo lengo hutakaa utimize, jiangalie sana katika nyumba yako una uwezo wa kutekeleza kitu gani kiuhalisia, tusipende kukuza mambo wakati hatuna uwezo, tuende mdogo mdogo safari ni ndefu."

Alibainisha kuwa suala la kuweka mambo makubwa halafu mwisho hayaendi sawa hatarajii litokee kwenye mkutano huo.

"Tusipende kukuza mambo tufanye mambo kwa uhalisia wetu kuhakikisha kunakuwa na mazingira wezeshi ya kufanya biashara," alisema.



## HABARI ZANZIBAR

# SMZ yaziondoa hofu asasi zisizo za kiserikali

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema ina imani na asasi za kiraia kutokana na mchango wao mkubwa wa kuleta maendeleo.

Akifungua kongamano la tatu la asasi za kiraia, Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, alizitaka asasi hizo kuwa na imani na serikali kwa kuwa na imani ya dhati ya kuweka mazingira mazuri kwa asasi hizo katika kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

"Ni matarajio ya serikali kuwa asasi za kiraia pamoja na wadau wengine wataitumia fursa hii ya kukutana katika kongamano hili kutoa michango na maoni mazuri yatakayoleta mabadiliko chanya ya nchi yetu," alisema Balozi Iddi.

Alieleza kuwa hivi sasa ushirikiano uliopo baina ya asasi za kiraia na serikali uko katika hali nzuri, kwa kuwa asasi hizo zimekuwa zikishiriki katika utengenezaji wa sera mbalimbali za kitaifa.

Alisema ni vyema asasi za kiraia zikajipanga na kushiriki

kikamilifu katika kufanikisha suala la ugatuzi wa madaraka mikoani.

"Naelewa kwamba baadhi ya asasi za kiraia ni wajumbe wa mabaraza ya wadi na kamati za mashauriano za shehia, kuwamo kwenu katika vyombo hivi kutasaidia kuwasilisha mawazo ya wananchi katika maamuzi yenye manufaa kwa taifa," alisema.

Akitoa mada katika kongamano hilo, mwanaharakati Salma Maulid, alisema asasi za kiraia sio kazi yake kushirikiana na serikali bali zinapaswa kufanya kazi zaidi na jamii kulingana na lengo la asasi hizo.

Alieleza kuwa kazi za asasi ni kukosoa na kusaidia jamii katika

kuelekea kwenye maendeleo ambayo wananchi wanahitaji kupewa elimu juu ya majukumu ya asasi za kiraia na namna ya utendaji wa kazi zake.

Alisema bado inaonekana uelewa ni mdogo katika jamii na ndio maana wanashindwa kuzitumia asasi za kiraia katika kazi zake.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Mwamvuli wa asasi za kiraia Zanzibar (ANGOZA), Hassan Khamis Juma, alieleza kuwa asasi hiyo itashirikiana na asasi za kiraia katika kuihamasisha jamii kuwapa nafasi wanawake kugombea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Alisema kuwa wanawake nao wana fursa sawa hivyo wasinyimwe haki zao ikiwamo ya kijinsia.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi (katikati), akiangalia moja ya bidhaa ziunazouzwa katika moja ya maduka ya Mr Discount, lililoko Veta, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni mkurugenzi wa maduka hayo, Mohamed Mansool. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi watakiwa kufuata sheria za utumishi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Tawala Mkoa Mjini Magharibi Unguja, Hamida Mussa Khamis, amewataka watendaji wa Baraza la Manispaa na Wilaya ya Magharibi "A" kufuata sheria na kanuni za utumishi wa umma katika kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na watendaji wa wilaya hiyo katika kikao kilichowashirikisha masheha, makatibu tawala na wakurugenzi wa manispaa.

Aliwataka watendaji hao kubadilika katika kufanikisha majukumu yao kwa maendeleo ya nchi sio kwa maslahi yao binafsi.

Alisema kuwa kumejitokeza kwa baadhi ya watumishi wa taasisi hizo kukosa uzalendo wa kutekeleza kazi zao ipasavyo na kusababisha kurudisha nyuma jitihada za serikali katika utoaji huduma na kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Alisema serikali za wilaya na mkoa hazitawavumilia watendaji wa aina hiyo na kama hawawezi kutekeleza majukumu yao ni bora kukaa pembeni.

Akizungumzia suala la nidhamu katika sehemu za kazi katibu tawala huyo, alisema suala la mahudhurio hususani muda wa kufika kazini hauridhishi kwa watendaji wa wilaya na manispaa zote za mkoa huo.

Aliwataka wafanyakazi hao kuwahi kazini kwa wakati na kuondoka kwa wakati kama sheria za utumishi wa umma zinavyoelekeza.

"Limekuwa ni jambo la kawaida kwa watendaji wetu kufika kazini wakati wanaotaka na kuondoka kabla ya muda ulioelekezwa kama kwamba hawana majukumu ya msingi ya kufanya," alisema.

Hamida aliwaagiza wakuu wa sekta wa wilaya na manispaa hiyo

kuwasilisha ripoti za utekelezaji wa majukumu ya wafanyakazi

wanaowasimamia kwa kila wiki kwa makatibu tawala na wakurugenzi wao ili kuona kila mtendaji anatekeleza vyema shughuli zake za kila siku.

Naye Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "A", Amour Ali Mussa, aliwasisitiza wafanyakazi hao kuendelea kufanya kazi kwa pamoja ili kuleta mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi wa manispaa hiyo.

"Kimsingi muda wa majungu, kusemana katika maeneo yetu ya kazi hayaleti tija yoyote wala ufanisi katika utoaji wa huduma na hiyo siyo dhamira ya kuwa mtumishi wa umma utumishi wa umma ni kuwa na nidhamu, ushirikiano na utekelezaji mzuri wa kazi ulizopangiwa," alisema.

Kwa upande wao Makatibu Tawala Wilaya ya Magharibi "A" Mohammed Ahmed na Katibu Tawala wa Wilaya ya Magharibi "B" Hamza Ibrahim, waliwataka

masheha kuendelea kuwahudumia wananchi kwa ufanisi na kutotumia lugha zisizofaa ili kuepusha malalamiko yasiyokuwa ya lazima.

Walisema kumekuwa na malalamiko yanayoripotiwa kwa baadhi ya viongozi hao kutokuwa na lugha nzuri kwa wananchi wanaowaongoza jambo ambalo halileti sura nzuri kwa viongozi hao, kwa kuwa wao ni wawakilishi wa serikali katika maeneo yao.

# Uwanja wa ndege wa kisasa kujengwa Pemba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, inatarajia kujenga uwanja wa ndege wa kisasa kisiwani Pemba utakaoruhusu kutua ndege kubwa.

Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, aliyasema hayo Wawi Chake Chake Pemba, wakati wa majumuisho ya ziara yake kisiwani humo.

Alisema kuwa uwanja huo utakuwa wa kisasa na mkubwa utakaoruhusu ndege za aina zote kubwa kutua katika kiwanja hicho na kusaidia usafiri wa anga.

Alisema tayari mchakato wake umeanza na ameshatuma

mawaziri 10 kwenda kwa wananchi wanaoishi katika maeneo ya pembezoni mwa uwanja huo wakiwamo wananchi wa Mfikiwa, Furaha na Mvumoni ili wakae tayari ujenzi utakapoanza waweze kuondoka katika eneo hilo na kupewa fedha kwa ajili ya mali zao. Dk. Shein alisema kuwa tayari upembuzi yakinifu umeshafanywa kwa ajili ya uwanja huo mpya wa ndege na karibu Sh. milioni 500 zimetumika

na hivi sasa serikali iko katika hatua za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

"Niwaombe wananchi kuwa na subira hasa wale wanaoishi pembezoni mwa uwanja huo kwa kuwa mtapewa fidia mara tu ujenzi utakapoanza," alisema.

Aidha, Dk. Shein aliwataka wawakilishi wa majimbo yaliyoko katika Wilaya ya Chake Chake, Pemba kuongeza kasi ya kushirikiana kwa kwenda kufanya kazi ili kuwashughulikia wananchi kwa azma ya kutatua changamoto walizonazo.

Dk. Shein pia alieleza kuwa ujenzi wa barabara ya Chake Chake-Mkoani pamoja na barabara ya Chake Chake-Wete, azima ya ujenzi huo iko pale pale kwa kuwa mchakato wake umeanza. Alisisitiza haja kwa viongozi wote wa serikali wakiwamo maofisa wa vikosi kufanya kazi zao kwa uadilifu kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria zilizopo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa kazi zao na kuleta ufanisi zaidi.

Alisema kuwa ziara yake hiyo imekuwa na mafanikio kuliko changamoto, huku akisisitiza haja ya kutekelezwa kwa maagizo yote aliyoyaelekeza na kuahidi kufanya ziara nyengine baada ya miezi minane.

HABARI KIMATAIFA

## Waziri wa Mambo ya Nje Iran ajiuzulu

**TEHRAN,** Iran

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Iran, Mohammad Javad Zarif, aliyeongoza mazungumzo ya kufikiwa kwa makubaliano ya kinyuklia ya mwaka 2015 kati ya Iran na mataifa mengine matano yenye nguvu duniani amejiuzulu ghafla.

Zarif ambaye kwa sehemu kubwa alifanikisha mazungumzo ya nchi yake kufikia mwafaka na nchi za magharibi kuhusu mpango wake wa nyuklia, hakuweka wazi sababu zilizomsababisha kuchukua uamuzi huo.

Zarif alitangaza kujiuzulu na kuliomba radhi taifa kwa kuchukua hatua hiyo ghafla. Kupitia kwenye ukurasa wake wa kijamii wa Instagram, Zarif amewashukuru wananchi wa taifa hilo na nchi washirika kwa kumwamini huku akiomba radhi kwa kushindwa kuendelea na kazi aliyoaminiwa na taifa.

Uamuzi wa kujiuzulu umekuja saa chache baada ya ziara ya kushtukiza ya Rais wa Syria, Bashar Al-Assad, mjini Tehran, ambapo inaripotiwa kuwa hakuwapo hata katika mkutano kati yake na kiongozi wa juu wa kidini wa taifa hilo, Ayatollah Ali Khamanei pamoja na Rais Rouhani.

Hata hivyo, wabunge wa Iran na wenye ushawishi mkubwa wameonyesha kulikataa ombi hilo la Zarif.

Taarifa iliyoandikwa kwenye ukurasa rasmi wa Instagram wa ofisi ya rais ilisema "Zarif hatakuwa peke yake, serikali itamuunga mkono".

Zarif mwenye miaka 59, ameitumikia Wizara hiyo ya Mambo ya Nje tangu Agosti 2013, na katika kipindi hicho amekuwa akikabiliwa na shinikizo la mara kwa mara kutoka kwa wanasiasa wenye mrengo mkali wanaoipinga sera yake ya msimamo wa kimahusiano na mataifa ya Magharibi.

Sababu ya kujiuzulu kwake imeibua mjadala kwenye majukwaa ya kijamii, huku baadhi wakidai amechoshwa na ukosoaji kuhusiana na mkataba huo wa nyuklia pamoja na sera yake kuelekea mataifa ya magharibi.

Wengine wanadai amekasirishwa na namna alivyowekwa pembeni katika mkutano na Rais wa Syria, Bashar al-Assad. **RFI**

# Buhari aongoza mbio za urais Nigeria

**LAGOS,** Nigeria

MATOKEO ya mwanzo yaliotolewa na Tume ya Uchaguzi Nigeria (INEC), kutoka majimbo mawili kati ya 36, kusini magharibi mwa nchi, yameonyesha Buhari anaongoza kwa kiwango kikubwa.

Matokeo hayo yameonyesha kuwa katika Jimbo la Ekiti, Buhari anaongoza kwa asilimia 58 dhidi ya 40 za mpinzani wake Atiku Abubakar, na Jimbo la Osun ameongoza kuwa asilimia 49 dhidi ya 47.

Ushindi wa kwanza wa Abubakar ulikuwa katika mji mkuu wa shirikisho Abuja, ambako alimshinda Buhari kwa tofauti ya kura 108,000.

Buhari mwenye umri wa miaka 76 na mtawala wa zamani wa kijeshi, anawania muhula wa pili kwa ahadi ya akupambana na rushwa, huku Atiku, mwenye umri wa miaka 72, ameahidi kupanua sekta binafsi.

Matokeo yanaonekana kutegemea zaidi yupi kati ya wagombea hao anaaminiwa na wapigakura kufufua uchumi wa taifa hilo unaoendelea kupambana na athari za mdororo wa mwaka 2016.

**Ujumbe wa waangalizi wa Umoja wa Afrika (AU) katika ripoti yake imeeleza kuwa uchaguzi ulifanyika kwa amani kwa sehemu kubwa licha ya matukio kadhaa ya vurugu na udanganyifu.**

Waangalizi wa uchaguzi huo wanakosoa kuchelewesha ufunguaji wa vituo katika maeneo mengi, wakisema ucheleweshaji huo na kuahirishwa kwa uchaguzi huo kwa wiki nzima viliwakatisha tamaa watu wengi kupiga kura.

Ujumbe wa waangalizi wa Umoja wa Afrika (AU) katika ripoti yake imeeleza kuwa uchaguzi ulifanyika kwa amani kwa sehemu kubwa licha ya matukio kadhaa ya vurugu na udanganyifu.

Kundi la Situation Room, ambalo ni muungano wa mashirika ya kiraia yaliosimamia uchaguzi huo kwa pamoja limeeleza watu zaidi ya 39 waliuawa nchini humo siku ya kupiga kura.

Mwenyekiti wa kundi la waangalizi wa Jumuiya ya Madola, Rais mstaafu Jakaya Kikwete, alisema kuwa vurugu zilizotokea kwenye uchaguzi huo ni suala linalohuzunisha.

"Kumekuwa na ugumu wa kimaandalizi, kilojistiki na kiufundi katika uchaguzi huu ambavyo tunajua na kuamini kuwa INEC na wadau wote nchini Nigeria watahitaji kuvishughulikia, vurugu zinazohusiana na uchaguzi na upotevu wa maisha vilivyotokea katika maeneo kadhaa vinasikitisha. Naamini Nigeria inaweza kufanya vizuri zaidi. Vurugu hazina nafasi katika demokrasia ya kisasa," alisema Kikwete.

Naye, Mkuu wa Ujumbe wa Waangalizi wa Umoja wa Ulaya (EU), Maria Arena, alisema kura hiyo ilitatizwa na kosoro za kiutendaji zilizosababisha ugumu kwa wapigakura.

Nalo kundi la waangalizi kutoka Marekani limesema ucheleweshaji wa uchaguzi huo kwa wiki nzima umeharibu imani ya umma katika mchakato huo na imepunguza uitikiaji wa wapigakura. **DW**



Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari (kulia), akiwa na makamu wake Yemi Osibanjo. **PICHA: NOVO**

# Kardinali Katoliki hatiani kwa unyanyasaji kingono

**CANBERRA,** Australia

KARDINALI George Pell wa Kanisa Katoliki nchini Australia amekutwa na hatia za unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto.

Imeelezwa kuwa Pell aliwafanyia unyanyasaji vijana wawili mwaka 1996, lakini amekana kuhusika na tuhuma hizo.

Mashtaka dhidi ya Pell yalifunguliwa tangu Desemba, lakini hayakuwekwa wazi kutokana na sababu za kisheria.

Pell mwenye umri wa miaka 77 anatarajiwa kuhukumiwa leo, lakini mawakili wake wanasema kuwa watakata rufani hatia hiyo.

Kiongozi huyo wa kanisa aliyekuwa anashikilia nafasi ya mweka hazina, ni miongoni mwa viongozi wenye nguvu zaidi kanisani.

Pell amekutwa na hatia ikiwamo ya kumwingilia mtoto chini ya miaka 16, na hatia zingine nne za kuwafanyia vitendo visivyo vya kawaida watoto wa chini ya miaka 16.

Kanisa Katoliki duniani kote kwa miaka ya hivi karibuni, limekumbwa na kashfa ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto, na kudaiwa kuwa wamekua wakificha masuala hayo.



Hata hivyo, Kadinali Pell amekanusha kuhusika na matukio yote, na kwa sasa yupo katika mapumziko marefu wakati kesi ikiendelea.

Pell alikuwa katika mwaka wake wa kwanza katika kanisa huko Melbourne mwaka 1996, alipowafanyia unyanyasaji watoto, baada ya kuwaambia kuwa walikunywa mvinyo wa kanisa.

Inaelezwa kuwa Pell aliwalazimisha kuwafanyia vitendo visivyofaa kama adhabu yao.

Kanisa Katoliki lilipata fursa ya kusikia ushahidi kutoka kwa mmoja wa wahanga wa unyanyasaji huo, na kwamba mwathiriwa mmojawapo alishafariki.

Kukutwa na hatia kwa Pell kumevutia umakini wa watu wengi ikizingatiwa, Papa Francis ameanza jitihada za kupambana na tatizo hilo ikiwamo mkutano uliofanyika wiki iliyopita.

Kwenye mkutano huo, Papa Francis, alisema "Unyama unaotendeka kote ulimwenguni unaweza kuja kuwa wa hali ya juu na kulikashifu kanisa, kwa sababu tu ya kulinganishwa na mamlaka ya kimaadili na uaminifu"

Alipochaguliwa mwaka 2013, Papa Francis alifanya maamuzi ya kuhusiana na unyanyasaji wa kingono unaohusisha watawa, ambapo alisema bado hatua za kutosha hazijachukuliwa kuwashikilia watawa watakaohusishwa na unyanyasaji.

Idadi kubwa ya watu huenda wakawa wamefanyiwa unyanyasaji wa kingono na watawa na wakati wote kanisa limekuwa likishutumiwa kuficha uhalifu huo. **BBC**

# Bosi wa JICA kuwasili Tanzania kukagua miradi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais na Mtendaji Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Kazuhiko Koshikawa, anatarajiwa kufanya ziara ya kikazi nchini kuanzia leo hadi Machi 3, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana na shirika hilo, ilisema kuwa katika ziara hiyo, Koshikawa atatembelea baadhi ya miradi inayofadhiliwa na JICA, jijini Dar es Salaam na Mkoa wa Kilimanjaro.

Akiwa jijini Dar es Salaam, taarifa ilisema anatarajiwa kushuhudia utiaji saini wa mradi wa upanuzi wa Barabara ya Bagamoyo (kituo cha Mwenge - Morocco), utakaofanyika kesho (Feb. 28) na mkoani Kilimanjaro anatarajiwa kushuhudia shughuli mbalimbali za miradi ya umwagiliaji na viwanda vya uzalishaji mchele (TANRICE), uliopo Moshi Chini, Machi Mosi.

JICA ni shirika kubwa duniani linalofanya shughuli zake katika zaidi ya nchi 150 na kuwa na ofisi zaidi ya 100 duniani, Tanzania ikiwa kati ya nchi hizo.

Ofisi ya JICA nchini, ilifunguliwa rasmi mwaka 1980, japokuwa misaada ya shirika hilo kwa Tanzania ilianza kutolewa tangu mwaka 1962 kwa makubaliano ya washiriki wa mafunzo ya ufundi.

Ushirikiano wa karibu kati ya JICA na Serikali ya Tanzania umeendelea kukua na kupanuka kwa miaka kadhaa sio tu kwenye masuala ya ufundi bali pia misaada mikubwa na mikopo.

Aidha, JICA imetoa kipaumbele katika sekta za kilimo, viwanda, maendeleo ya miundombinu na uboreshaji wa huduma za kijamii.

Kati ya miradi mikubwa iliyofadhiliwa na JICA ni pamoja na daraja la Selander (1980) na daraja la Mfugale Flyover (2018).

Miradi inayotekelezwa kwa sasa ni pamoja na miundombinu, afya, maji na nishati na miradi ya kilimo na elimu.




Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (katikati), akiwa na Meneja Mwandamizi Biashara ya Kilimo wa Benki ya NMB, Carol Nyangaro, wakati wa kongamano la wadau wa sekta ya maziwa nchini, lililoanza jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau wa Maziwa Duniani (GDP), Dk. Margrethe Jonkman. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Anayedaiwa kunajisi mtoto kizimbani

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKAZI wa kitongoji cha Kinyo kilichoko katika Kijiji cha Msebehi wilayani Uvinza, Mathayo Juma (28), amepandishwa kizimbani kwa kosa la kumnajisi mtoto wa kike.

Halikadhalika, amedaiwa kumlawiti na kumbaka mtoto huyo mdogo katika matukio matatu tofauti yaliyotokea kati ya Desemba na Januari mwaka huu.

Mshtakiwa huyo alisomewa maelezo ya awali jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma.

Juma anakabiliwa na mashtaka matano ya kubaka na kulawiti mtoto huyo msichana mwenye umri wa miaka nane na kumsababishia maumivu makali, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Flora Mtarania na kukana mashtaka .

Hata hivyo aliwekwa mahabusu katika gereza la Bangwe baada ya kukosa wadhamini.

Akisoma maelezo ya awali Mwendesha Mashtaka, Wakili wa Serikali Raymond Kimbe, alidai kuwa, Desemba 31 mwaka 2018, Januari 4 mwaka 2019 na Januari 7 mwaka huu majira ya usiku katika Kitongoji cha Kinyo Kijiji cha Msebehi Wilaya ya Uvinza, Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa huyo alimbaka na kumlawiti mtoto msichana mwenye umri wa miaka nane na kumsababishia maumivu makali.

Kimbe aliendelea kueleza kuwa, upande wa mashtaka unatarajia kupeleka mahakamani mashahidi 10 na vielelezo viwili na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Mtarania alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Machi 5 mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Aidha, mshtakiwa huyo ataendelea kuhifadhiwa mahabusu katika gereza la Bangwe.

ITV

**IJUE SHERIA: SAA 12:30 JIONI**

**JE, UNAIFAHAMU SHERIA YA DAWA NA CHAKULA INASEMAJE, ULINZI WA SHERIA HII NI KWA WATU WA AINA GANI HASA, MAMLAKA GANI INA UWEZO WA KUSIKILIZA MASHAURI YAHUSUYO SUALA ZIMA LA DAWA NA CHAKULA, NINI NAFASI YA MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA TFDA KATIKA SHERIA YA CHAKULA NA DAWA?. MWANASHERIA LEONARD MANYAMA ATAFAFANUA KIUNDANI IKIWA NI SEHEMU YA KWANZA.**

# Serikali yataka walemavu CHF

**Na Happy Severine,** SIMIYU

KATIKA jitihada za kuhakikisha kuwa wanaoishi na ulemavu wanapatiwa huduma za afya kikamilifu, serikali imewataka kujiunga na mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa (CHF).

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu, Stella Ikupa, ametoa wito huo akiwataka viongozi wa vyama vya watu wenye ulemavu, kuwahamasisha wanachama wao kujiunga na mfuko huo.

Ikupa (pichani chini) alitoa wito huo jana wilayani Itilima mkoani Simiyu, wakati wa ziara yake ya kukagua utekelezaji wa maelekezo ya serikali yakiwamo yanayowahusu walemavu.

Aliwataka viongozi wa vyama hivyo kuwapa taarifa na uhamasishaji wa kujiunga na mfuko wa CHF ulioboreshwa ili kutunza na kulinda afya zao.

Aidha, Naibu Waziri, aliwaagiza maofisa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii kutoa elimu vijijini kwa watu wenye ulemavu kuhusiana na uundwaji wa vikundi vya ushirika na namna ya kutekeleza miradi ya miradi ya kujitegemea.

Kwa upande wake, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Festo Kiswaga, alieleza kuwa Simuyu imeanza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwamo ya kuboresha hali za walemavu.

Kwa upande wao viongozi pamoja na watu wenye ulemavu walioshiriki katika ziara hiyo walimwomba Naibu Waziri kushughulikia baadhi ya changamoto zinazowakabili katika maeneo yao.

"Ninaomba serikali itusaidie tuweze kupata wakalimani wa lugha ya alama ili na sisi walemavu tuweze kusikia na kupata ujumbe unaokuwa unawasilishwa na viongozi wetu kwenye mikutano na ziara kama hii ya leo hii."

Ombi hilo lilitolewa na Mhandi Ntobi, Mwenyekiti wa Chama cha Walemavu wasiosikia Mkoa wa Simiyu.



## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Kisongo Arusha jirani na Braebun School Kina upana wa 43,urefu 93 . Bei Milioni 40 kimepimwa. Maji, barabara na umeme vipo. Mawasiliano:-0755 907 520.

**ENEO LINAUZWA,** NAUZA ENEO LIKO MPIJI MAGOE YANAPOGEUKIA MAGARI YA KUTOKA MBEZI NI UNATEMBEA MITA 200 HADI KWENYE ENEO UKUBWA NI MITA 20@40. BEI NI NAFUU KABISA SIMU NAMBA: 0621 607825.

### NAFASI ZA KAZI

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LAMWEL ELIA MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 130 CQY** TOYOTA RAV 4.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MAG/RB/562/2019.

115089202

### CHETI KIMEPOTEA



**CONSTANTINA KIZWALO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0380-003** kilichotolewa na UCHAMA SEKONDARI mwaka 1988. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MS/RB/7472/2018.**

115082202

### KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**EDWARD JONAH KAMWELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina LANDCRUISER yenye namba za usajili **T381CDR.** Chassis **JTERB71J00016347,** Engine Namba **1HZ0413605.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/TR/RB/206/2019.**

115082602

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENARD HEZRON MUNUBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 509 AZG VITS.** Engine namba **1820379577.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/B.I/I/VOL VIII/81.**

115081102

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Abdillah Said Mtaswa** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yeye namba ya usajili **T602 DFK** aina ya TOYOTA RACTIS yenye engine namba **INZEAA7232** na chasis namba **NCP105007232.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **KJN/RB/621/2019**

115080702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 70. 2019**
**Mdai: HADIJA MOSES SADIKI**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: MAJALIWA JOHN MKOMBOZI**

**Kwa:**
**MAJALIWA JOHN MKOMBOZI**
**WA KIHONDA MBUYUNI**
**MOROGORO**

**Ombi la Mdai: HADIJA MOSES SADIKI**
**Madai ya: PESA SHILINGI 7,705,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 28 mwezi 02 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25 mwezi 02 mwaka 2019.

215081302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No; 37/2019**
**Ombi la MOHAMED S.MATIKULA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MAGRETH FRANK**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 12/02/2019.

215081202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No; 48/2019**
**Ombi la SARAH HAMIS NDUI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu WILSON JONAS MSENGI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 22/02/2019.

215081502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA – MWANZA**
**SHAURI NA 151 LA 2013**
**BENARD PETER.....................MUOMBAJI**

DHIDI YA

1. DIAMOND TRUST BANK (T) LIMITED
2. FLAVIA MTATINA (THE ADMINISTRATIX OF THE ESTATE OF THE LATE JAMES JUSTINE JOACHIM@JONAS JAMES KAIJAGE................................WADAIWA

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

KWA: FLAVIAN MTATINA (THE ADMINISTRATIX OF THE ESTATE OF THE LATE JAMES JOACHM@JONAS JAMES KAIJAGE)
Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 18/03/2019 katika chumba cha baraza, barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania.

Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria.

KAA – Ukijua kwamba kushindwa kufika, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo.

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya Baraza leo tarehe 25/02/2019.

115082402

**RE;THE LAND ACT NO 4 OF 1999**
**LOSS OF ORIGINAL LETTER OF OFFER OF REF NO;MMC/LD/3738**

**REGISTERED OWNER; PHILIP WILLIUM KABUGA**

**LAND; PLOT NO.232 BLOCK "V"SABASABA MOROGORO MUNICIPALITY**

**APLICANT; PHILIP WILLIUM KABUGA**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGINAL LETTER OF OFFER** to the land described above is said to be lost and that I intend to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty days(30) from the date of this pubication.

**THE ORIGINAL LETTER OF OFFER** is found,should be delivered to the office of the ;Municipal Director,Morogoro Municipal Council,P.o box 166 Morogoro.

**Issued by:**

215082102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No; 47/2019**
**Ombi la SALMA RAMADHANI KIGWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PILI ATHUMANI KIENGE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/03/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 22/02/2019.

215082002

**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**Katika Mahakama ya wilaya ya Dodoma**
**Usimamizi wa mirathi No. 06/2019**
**Ombi la PATRICK JANUARY MSUNGU kuteuliwa Msimamiliz wa mirathi ya marehemu JANUARY MWAPENDA MSUNGU**

Watu wotew anaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo na wan nia ya kupinga uteuzi wa mwombaji huyo. wanalikwa kufika mahakamani kuhudhuria kesi mnano 20/3/2019 ili kuwasilisha mapingamizi yao kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

115082502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No; 51/2019**
**Ombi la RAJABU SAID MRAHAGWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SAID ISSA MRAHAGWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 27/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 25/02/2019.

215081402

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KYAW MYINT AUNG** anatangaza kupotelewa n akadi ya gari TOYOTA RAV 4 yenye namba za usajili **T 210 GD 450.** Engine namba **1ZZ-0616974**, chasis namba ZCA26-007687,

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifayapolisi: **OB/RB/1936/2019.**


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la The Guardian kila siku*



NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KEPA APIGWA FAINI CHELSEA



**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, ametozwa faini ya mshahara wake wa wiki moja na ameomba msamaha kwa kukataa kuondolewa uwanjani wakati wa mechi ya fainali ya Kombe la Ligi (EFL Cup) dhidi ya Manchester City Jumapili.

Chelsea ilifungwa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-3 na Man City wakalitwaa taji hilo.

Kipa huyo raia wa Hispania alikataa kuondolewa uwanjani ili kipa wa ziada Willy Caballero kuchukua nafasi yake katika Uwanja wa Wembley.

"Licha ya kwamba hatukuelewana, kwa kujitathamini, nilifanya makosa kwa namna nilivyoshughulikia hali hiyo," Kepa amesema katika taarifa rasmi ya Chelsea.

Kocha Maurizio Sarri alisema kwamba yeye na Kepa wamekuwa na mazungumzo mazuri.

Sarri, aliyeondoka kwa hasira wakati Kepa alipokataa kutoka uwanjani dakika za mwisho za muda wa ziada, pia amebaini kwamba 'hawakuelewana'.

Lakini aliongeza: "Kepa ametambua alifanya makosa makubwa katika namna alivyofanya.

"Ameniomba msamaha, amewaomba wachezaji wenzake na timu nzima kwa jumla msamaha. Ni uamuzi wa klabu hiyo kumuadhibu kwa mujibu wa sheria za klabu, lakini binafsi, suala hili limemalizika.

"Uchezaji wa timu nzima kwa jumla, ulikuwa ni matumaini makubwa na ni aibu kuona namna tukio hili limegubika mchezo na jitihada za timu katika fainali iliyokuwa na ushindani mkubwa."

Kepa, ambaye ni mchezaji wa klabu hiyo aliyesajiliwa kwa kitita cha pauni milioni 71, alikaidi jitihada za Sarri kumuondosha uwanjani na kumuweka kipa mwenza Caballero kabla ya Manchester City kushinda kwa penalti.

## *Cavani kurudi PSG wiki hii*

**PARIS,** Ufaransa

EDINSON Cavani anapanga kurudi kuichezea Paris Saint-Germain wiki hii, kocha Thomas Tuchel amethibitisha.

Mfungaji huyo mwenye rekodi ya kufunga mabao hapo PSG, aliumia wakati wakishinda dhidi ya Bordeaux mapema mwezi huu na alikosa mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora mapema mwezi huu dhidi ya Manchester United, akijiunga na Neymar kwenye orodha ya majeruhi.

Lakini miamba hao wa Ligue 1, walishinda 2-0 bila ya nyota hao kwenye dimba la Old Trafford na sasa Cavani anakaribia kurudi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay jana Jumanne hakucheza dhidi ya Dijon kwenye mchezo wa robo fainali ya Kombe la Coupe de France, na Tuchel ana matumaini kwamba atakuwapo kwenye mechi ya wikiendi baada ya kujiunga na kiosi hicho kwenye mazoezi.

"Edi atafanya mazoezi na sisi wiki hii. Anazungumza na madaktari wetu," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Alifanya vizuri kwenye mazoezi na tuko vizuri. Natumaini anaweza kucheza Jumamosi dhidi ya Caen."

PSG itacheza na United jijini Paris siku nne baada ya mchezo dhidi ya Caen, huku Cavani akitarajiwa kucheza kwenye mchezo huo.



## Rooney: Fainali Ulaya ni Man City vs Barca



**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Wayne Rooney ameitabiria Manchester City kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na itakutana na Barcelona.

Mchezaji huyo wa sasa wa DC United, Rooney alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na United mwaka 2008 na anaamini City ambayo inajipanga kushinda mataji manne msimu huu chini ya Pep Guardiola, inaweza kutinga fainali, ambayo itafanyika jijini Madrid katika dimba la Wanda Metropolitano, kwa mara ya kwanza katika historia.

"Nitakuwa na Manchester City v Barcelona," alisema Rooney akiiambia DAZN wakati alipoulizwa utabiri wake kwenye fainali ya michuano hiyo.

"Naweza kukuambia nani nataka awe juu, ningependa Barcelona kushinda kama wakiwa wao."

Rooney akiwa na United walifungwa mara mbili kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akisawazisha kwenye mchezo ambao baadaye walifungwa 3-1 katika dimba la Wembley mwaka 2011.

Alipoulizwa kuhusu uzoefu wake wakati akikatishwa tamaa mwaka 2009, Rooney aliongeza: "Nafikiri kile kilikuwa kitu cha kujifunza, wakati ambao unapoteza kwenye mechi kubwa.




# LUKAKU: NITACHEZA POPOTE MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

ROMELU Lukaku amesisitiza kwamba hajali ni sehemu gani anacheza kwa Manchester United, akisema kuwapo tu uwanjani ni jambo la heshima wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer akipambana kumaliza matatizo ya ushambuliaji.

Marcus Rashford, Jesse Lingard na Juan Mata walipata majeraha dhidi ya Liverpool Jumamosi, huku tayari Anthony Martial akiwa majeruhi, na Lukaku kwa sasa ndio mwenye jukumu la kuziba pengo lake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ameanza katika mechi 15 za Ligi Kuu msimu huu na amefunga mabao 15 yakiwa machache zaidi tangu alipoanza kucheza kikosi cha kwanza msimu wa 2012/13, lakini amesisitiza wiki hii kwamba yupo tayari kufanya kile timu inachokihitaji.

Akinukuliwa na ESPN wiki hii, alisema: "Kama kocha anataka kunitumia mimi, nitafanya kwa hali na mali kuisaidia timu. Tuna wachezaji wengi ambao ni majeruhi. Tunatakiwa kuwa na morali chanya. Sisi ni Manchester United, na unatakiwa kucheza popote ili kushinda.

"Kwa sasa mimi ni mchezaji natakiwa kucheza na kufunga, hivyo si tatizo kwangu mimi kuisaidia timu na ninataka kufanya hivyo kila mchezo," alisema.

# Rodgers aruhusiwa Celtic kutua Leicester City

**LONDON,** England

BRENDAN Rodgers anatarajiwa kuwa kocha mpya wa Leicester City baada ya Celtic kumpa ruhusu ya kufanya mazungumzo na klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

'Mbweha' (Foxes) hao wapo tayari kuziba nafasi ya kocha waliyemtimua, Claude Puel, mapema iwezekanavyo. Kocha wa Kikosi cha Kwanza, John Kennedy, anajiandaa kuchukua nafasi ya kuiongoza Celtic katika mechi ya leo ya Ligi Kuu ya Scotland dhidi ya Hearts.

Hata hivyo, kocha wa zamani, Neil Lennon, ndiye anayejiandaa kuiongoza timu hiyo hadi mwishoni mwa msimu kama raia mwenza huyo wa Ireland Kaskazini, Rodgers, atathibitishwa kuondoka.

"Brendan ameainisha kuwa hii ni fursa aliyoihitaji kuitafiti zaidi," Celtic ilieleza katika taarifa yake.

Kocha huyo wa zamani wa Liverpool, Rodgers alikatisha kwa kifupi katika mahojiano na BBC wakati alipoulizwa kuhusu nafasi hiyo ya Leicester baada ya kuibuka na ushindi dhidi ya Motherwell Jumapili.



# Mourinho: Nataka kufanya kazi na watu ninaowapenda

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amebainisha kwamba kwa sasa anataka kufanya kazi na watu anaowapenda.

Kocha huyo raia wa Ureno amekuwa hana kazi tangu Desemba mwaka jana baada ya kufukuzwa kule Manchester United.

Mourinho amesema tayari amekataa ofa kadhaa kwa sababu ya mtazamo wake na kwamba kwa sasa anataka kufanya kazi na watu ambao atafurahia kufanya nao kazi.

"Kama ni klabu isiyo na mtazamo, siwezi kwenda. Nilikataa kwa sababu nilitaka kufanya kazi na klabu yenye mtazamo wa juu zaidi," amesema kocha huyo wa zamani wa Real Madrid na Chelsea akinukuliwa na Gazeti la Telegraph.

"Hicho ni kitu cha kwanza. Nataka kuwa na timu ninayoipenda na watu ambao ninaowapenda kufanya nao kazi.

"Nataka kufanya kazi na watu ambao nitafurahia kufanya nao kazi, ambao naweza kushirikiana nao na kuwa na mawazo sawa.

"Nilipata kile nilichokitaka nikiwa kule kule Inter Milan. Kuna klabu kama hizi. Kwa hakika hii ni kitu muhimu zaidi kwa mafanikio ya klabu."

Mourinho aliiongoza United kutwaa taji la Europa, EFL na lile la Ngao ya Jamii, lakini timu hiyo ilianza msimu huu vibaya.



# DONDOO Z… KA MAGAZETI Y… YA




# ‘RONALDO KAPOTEA MABINGWA ULAYA’

## ●●● Tangu atue Turin, amekuwa chanzo cha kujiamini na kuhamasisha kikosi hicho…

**TURIN,** Italia

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini, amefunguka kuwa nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo, msimu huu hana ufanisi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kama aliokuwa nao kipindi kilichopita, lakini anaamini kuwa kwa ujumla ana msimu mzuri Italia.

**Kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, pia alitoa utabiri wake kuhusu ‘Kibibi Kizee’ hicho cha Turin kutwaa taji la Ulaya msimu huu.**

Tangu atue Turin, Ronaldo amekuwa chanzo cha kujiamini na kuhamasisha kikosi hicho, ameisaidia timu hiyo kuwa kileleni mwa Ligi Kuu Italia, Serie A na kuiweka kwenye nafasi nzuri Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Aidha, Ronaldo, 34, pia ndiye anayeongoza kwa kutupia kwenye ligi hiyo akiwa na mabao 19 hadi sasa na kinara wa utoaji wa pasi za mwisho kwa sasa, lakini ameziona nyavu mara moja tu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno pia ameshalimwa kadi nyekundu msimu huu.

Lakini kwa upande wa Juventus, imekumbana na kipigo kutoka kwa miamba ya La Liga, Atletico Madrid katika mechi ya kwanza ya hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, hivyo inakabiliwa na wakati mgumu wa kupindua matokeo kwenye mechi ya marudiano Italia.

Hata hivyo, licha ya kibarua kigumu kilichopo mbele yao, Mancini ameitaka Juventus kutokea nyuma ikiwa imefungwa kama ilivyofanya dhidi ya Real Madrid msimu uliopita.

Akizungumza na Tiki Taka (kupitia Football Espana), kocha huyo alisema, “Juve-Atletico? Wanajua itakuwa mechi ngumu. Hakuna kanuni ya kichawi ya kutokea nyuma, lakini Juve ni timu yenye uzoefu na walitokea nyuma wakiwa wamelala 3-0 nyumbani dhidi ya Real Madrid msimu uliopita.”

Mancini aliongeza kuwa Ronaldo bado hajafanya vizuri kwenye michuano hiyo ya Ulaya, lakini bado amefanikiwa “vitu vingi muhimu”.

“Pengine Ronaldo hajafanya kwenye Ligi ya Mabingwa kile alichokifanya wakati uliopita, lakini mara zote amefanikiwa vitu muhimu.”

“Anafanya vizuri Serie A. Nadhani kwa daraja lake, ni ngumu popote. Ligi Italia ni ngumu kama ilivyo England na kidogo sana huko Hispania, lakini kwangu mimi, anayo msimu mzuri.”

Juventus itapaswa kushinda mechi ya marudiano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati itakapoikaribisha Atletico Madrid Machi 12, mwaka huu.

Kwingineko, mechi ijayo kwa ‘Bianconeri’ hao ni ya Serie A dhidi ya Napoli Jumapili usiku.

## ZISIKUPITE

### KEPA KAMTOA MACHOZI SARRI

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri alilia kwa kipa Kepa Arrizabalaga kwenye chumba cha kubadilishia nguo Uwanja wa Wembley kwa kitendo cha mlinda mlango huyo kukataa kufanyiwa mabadiliko (‘sab’)kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Ligi ***(Carabao Cup). (Sun)***

### RENNES: TUTAICHAPA ARSENAL

KIUNGO wa Rennes, Clement Grenier, amefunguka kuwa wataichapa Arsenal kwenye Ligi ya Europa kama walivyoitoa Real Betis raundi ya 32. ***(Goal)***

### RODGERS ANUKIA LEICESTER

LEICESTER City imepiga hatua katika mchakato wa kumteua kocha wa Celtic, Brendan Rodgers, kuwa kocha wao mpya. ***(Guardian)***

### AMPIGIA DEBE SOLKSJAER

NAHODHA wa zamani wa Manchester United, Gary Neville, amesema itakuwa “uasi” Old Trafford kama Ole Gunnar Solksjaer hatateuliwa kuwa kocha wa kudumu. ***(Daily Mirror)***

### YAKOMAA KWA BISSAKA

ARSENAL inaongoza mbio za kumsajili beki wa kulia wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka, 21, na ipo tayari kufika dau la pauni milioni 40 zinazotakiwa kutolewa na wapinzani wao wa EPL. ***(Sun)***

### ICARDI ANASTAHILI UNAHODHA

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini, amesema Mauro Icardi anastahili kuwa nahodha wa Inter Milan. Mancini alimpa unahodha Muargentina huyo wakati akiinoa Inter, lakini hivi karibuni mshambuliaji huyo alinyang’anywa kitambaa hicho. ***(Goal)***

### APUUZA UVUMI LEICESTER

KOCHA wa Burnley, Sean Dyche amepuuzia tetesi kuwa anawindwa na Leicester. ***(Burnley Express)***

### CHELSEA, UTD KWA ROMAGNOLI

MANCHESTER United na Chelsea zinajipanga kumfuata nahodha wa AC Milan, Alessio Romagnoli,. Lakini zitakabiliwa na ushindani katika kuipata saini ya beki huyo wa kati kutoka kwa mabingwa wa Serie A, Juventus. ***(Calciomercato, via Manchester Evening News)***

### ‘HAKUNA SHIDA NA BALE’

BEKI wa pembeni wa Real Madrid, Sergio Reguilon, amesisitiza kuwa hakuna tatizo na Gareth Bale. Uhusiano wa Bale na wachezaji wenzake unaonekana kutokuwa mzuri kwa sasa. ***(Goal)***

### LEEDS KUUZWA ISIPOPANDA EPL

MMILIKI wa Leeds United, Andrea Radrizzani, atahitaji kufikiria kuiuza klabu hiyo kama watashindwa kufanikiwa kupanda Ligi Kuu England - kwa sababu itamuwia vigumu kuiwezesha kwa msimu mwingine kucheza Ligi Daraja la Kwanza maarufu kama ‘Championship’. ***(Daily Mail)***

### CHELSEA KUMUUZA PALMER

CHELSEA inajiandaa kumpiga bei kiungo Muingereza Kasey Palmer kwa pauni milioni nne, licha ya mchezaji huyo kutowahi kucheza kikosi cha wakubwa, na Bristol City inatazama kuufanya mkataba wake wa mkopo kuwa wa kudumu. ***(Sun)***

## Kili Marathon kufunga barabara Moshi

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAANDAAJI wa mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2019, wametangaza barabara zitakazofungwa kwa muda fulani Jumapili ili kuruhusu mbio hizo kufanyika kwa usalama zaidi.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji hao, ilieleza kuwa tangazo hilo limetolewa mapema ili kuwapa wakazi wa Moshi nafasi ya kujipanga vizuri hasa kwa wale ambao watakuwa wakielekea kanisani.

"Waendesha magari na vyombo vingine vya moto wanatakiwa kuchukua tahadhari kila mara na kuendesha taratibu kwa sababu barabara zitakuwa na wakimbiaji wa mbio tofauti," ilisema taarifa hiyo.

Waandaaji hao walisema Machi 3, magari kutoka Arusha hayataruhusiwa kupita katika kona ya YMCA na mzunguko wa askari kuelekea Dar es Salaam kuanzia saa 12:30 hadi saa 2:30 asubuhi.

Aidha, magari kutoka Dar/ Marangu/Himo hayataruhusiwa kuingia Moshi kuanzia saa 12:30 hadi saa 2:30 na barabara kutoka Machame hadi Sokoine itafungwa pale Shanty Town kuanzia saa 12 asubuhi.

Kwa mujibu wa waandaaji, barabara kutoka Rau hadi Moshi itafungwa kwa ajili ya mbio za kilomita tano za Grand Malt kuanzia saa 1:15 hadi saa mbili asubihi.

Kuhusu maeneo ya kuegesha magari, waandaaji hao walisema kuna maeneo mawili mashariki mwa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kwa kupitia barabara ya Uru na kuingia viwanja vya MoCU na sehemu nyingine ni katika viwanja vya Chuo cha Polisi Moshi.

Daladala zitaruhusiwa kushusha abiria katika maeneo ya kuegesha magari au pembeni mwa barabara, lakini barabara ya MoCU kutokea Sokoine itafungwa kuanzia saa 12 asubuhi na daladala zitakazokuwa zinatoka upande huo zitalazimika kushusha katika kona ya barabara za Sokoine na Kilimanjaro.

Katika hatua nyingine, zoezi la kuchukua namba linaingia katika hatua ya lala salama ambapo kwa Moshi linatarajiwa kuanza leo (Jumatano) na kesho katika Hoteli ya Keys.

Zoezi hilo litafanyika kuanzia saa nne asubuhi hadi saa 11 jioni na Februari 28 kuanzia saa nne asubuhi hadi saa mbili usiku kwa ajili ya mbio za kilomita 42, 21 na uandikishaji wa kilomita tano.

Wadhamini wa mwaka huu ni Kilimanjaro Premium Lager, wakiwa wadhamini wa mbio za kilomita 42, Tigo mbio za kilomita 21 na Grand Malt kilomita tano Fun na wadhamini wa meza za maji KK Security, Keys Hotel, Kilimanjaro Water, TPC Sugar, Simba Cement, AAR, Kibo Palace, Barclays Bank, Precision Air na CMC Automobiles.

# KAGERE, BOCCO WATABIRIWA KIATU

**Na Faustine Feliciane**

KINARA wa mabao Ligi Kuu Tanzania Bara (TPL), Salim Aiyee, amewatabiria kufanya vizuri zaidi washambuliaji wa Simba John Bocco na Medy Kagere katika kuwania Kiatu cha Dhahabu kinachotolewa kwa mfungaji bora wa msimu.

Aiyee anayekipiga kwenye kikosi cha Mwadui FC ya Shinyanga, aliliambia gazeti hili jana kuwa kwa kasi ya wachezaji hao pamoja na idadi ya mechi walizonazo inatoa nafasi kwao kuweza kufunga mabao mengi zaidi.

**Alisema washambuliaji hao wa Simba wamekuwa kwenye kasi kubwa huku wakishirikiana vyema uwanjani.**

"Wako vizuri zaidi kwangu mimi ukilinganisha na washambuliaji wengine, mtu kama Kagere ana kasi na anakuja vizuri, lakini pia ukiangalia idadi ya mechi ambazo timu yao wamecheza utaona wana nafasi kubwa zaidi ya kufunga mabao mengi kama wataendelea na kasi hii ya sasa," alisema Aiyee.

Aidha, alisema hata mshambuliaji wa Yanga, Heritier Makambo si wa kumbeza kwenye mbio hizo za kuwania Kiatu cha Dhahabu.

Simba imecheza michezo michache zaidi ya timu yoyote mpaka sasa ikicheza michezo 18 kabla ya mechi ya jana dhidi ya Lipuli FC, ikizidiwa kwa michezo saba na vinara Yanga.

Wakati, Aiyee akiwaongoza washambuliaji wengine kwa kufikisha mabao 13, Makambo anamfuata akiwa na mabao 12 huku Kagere akipachika mabao 11 wakati Bocco mwenyewe amefunga mabao saba kabla ya mchezo wao wa jana ambao Simba walikuwa wakiumana na Lipuli FC ya Iringa kwenye Uwanja wa Samora, Iringa.




Wachezaji wa Azam FC, wakipongezana wakati wakishangilia moja ya mabao 3-0 waliyoshinda dhidi ya Rhino Rangers kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam juzi na kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho maarufu FA Cup. **PICHA: BIN ZUBEIRY**

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 25 | 19 | 4 | 2 | 42 | 17 | 61 |
| 2. Azam | 25 | 14 | 8 | 3 | 33 | 16 | 50 |
| 3. Simba | 18 | 14 | 3 | 1 | 38 | 6 | 45 |
| 4. Kinondoni MC | 27 | 9 | 13 | 5 | 31 | 18 | 40 |
| 5. Lipuli | 27 | 9 | 11 | 7 | 23 | 21 | 38 |
| 6. Mbao | 27 | 9 | 9 | 9 | 19 | 24 | 36 |
| 7. Alliance | 28 | 9 | 9 | 10 | 23 | 29 | 36 |
| 8. Coastal Union | 26 | 7 | 13 | 6 | 25 | 26 | 34 |
| 9. Mwadui | 28 | 9 | 6 | 13 | 29 | 30 | 33 |
| 10. Stand United | 28 | 9 | 6 | 13 | 27 | 35 | 33 |
| 11. JKT Tanzania | 27 | 7 | 11 | 9 | 15 | 17 | 32 |
| 12. TZ Prisons | 27 | 7 | 11 | 9 | 19 | 22 | 32 |
| 13. Ndanda | 26 | 8 | 8 | 10 | 17 | 27 | 32 |
| 14. Ruvu Shooting | 28 | 7 | 10 | 11 | 21 | 33 | 31 |
| 15. Mbeya City | 25 | 8 | 6 | 11 | 26 | 29 | 30 |
| 16. Kagera Sugar | 26 | 6 | 12 | 8 | 19 | 25 | 30 |
| 17. Mtibwa Sugar | 24 | 8 | 5 | 11 | 21 | 20 | 29 |
| 18. Singida United | 25 | 7 | 8 | 10 | 18 | 24 | 29 |
| 19. Biashara Utd | 26 | 5 | 8 | 13 | 18 | 29 | 23 |
| 20. African Lyon | 27 | 4 | 9 | 14 | 16 | 32 | 21 |

## *Iringa wafurahia tiketi za elektroniki*

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

UONGOZI wa timu ya soka ya Lipuli, umeeleza kufurahishwa na uamuzi wa kuanza kutumia tiketi za kielektroniki katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Samora mkoani hapa.

Tiketi hizo zilianza kuuzwa juzi kwa ajili ya mashabiki kuingia uwanjani kushuhudia mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya wenyeji Lipuli FC dhidi ya mabingwa watetezi, Simba kutoka jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mhasibu wa Lipuli FC, Tumaini Lupelo, alisema mfumo huo utasaidia sana kudhibiti mapato na vile vile utapunguza gharama za ukaguzi wa tiketi ambao walikuwa wanautumia zamani.

Lupelo alisema anaamini utapunguza pia msongamano wakati wa kuuza kwa sababu wanaanza kuziuza siku moja kabla ya mchezo hali inayosaidia kuhudumia mashabiki wengi.


Aliwataka mashabiki wa soka wa Iringa kutoa ushirikiano kwa kufuata mfumo huo mpya uliotambulishwa.

Lipuli inayofundishwa na Selemani Matola imekuwa moja ya timu zinazofanya vizuri na haiko kwenye janga la kushuka daraja.

# Michezo

Jumatano Februari 27, 2019

Nipashe



'Ronaldo kapotea Mabingwa Ulaya'

HABARI UK. 30



Beki wa Lipuli FC, William Lucian (kushoto), akiwahi kuokoa hatari dhidi ya mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Samora jana na wenyeji kuchapwa 3-1. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Simba hizi sasa sifa

## ●●● Yainamisha Uwanja wa Samora na kuvunja mwiko, kituo kinachofuata ni Algeria...

**Na Somoe Ng'itu,** IRINGA

SIMBA imepiga hadi sifa! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema kufuatia kukamilisha ratiba ngumu ya siku 10 kwa kucheza mechi nne za Ligi Kuu Bara na kuvuna pointi zote 12 baada ya jana kuifumua Lipuli FC kwa mabao 3-1 katika mechi kali iliyopigwa Uwanja wa Samora mjini Iringa.

**Wekundu wa Msimbazi hao, baada ya mechi ya Al Ahly ya Ligi ya Mabingwa Afrika waliyoshinda kwa bao 1-0, walianza mechi za Ligi Kuu kwa kuibuka na ushindi kama huo dhidi Yanga Uwanja wa Taifa Februari 16 na kisha siku tatu baadaye kuichapa African Lyon 3-0 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.**

Februari 22, ikarudi Uwanja wa Taifa na kuichapa Azam FC mabao 3-1 kabla ya jana kuibuka na ushindi kama huo Uwanja wa Samora, ambapo sasa itaingia kambini kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini Algeria dhidi JS Saoura hapo Machi 9, mwaka huu.

Kama walivyofanya watani zao Yanga kwa kuifunga Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, katika mechi ya jana Simba nao wamevunja mwiko kwa kuondoka na ushindi wa kwanza mkoani Iringa ikiwa ni msimu wa tatu tangu Lipuli iliporejea katika Ligi Kuu.

Simba ambayo imecheza mechi 19 na bado inaiwakilisha Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kwa ushindi huo sasa imefikisha pointi 48 wakati Lipuli iliyoshuka dimbani mara 27 imebakia pointi zake 38.

Mabao ya kiungo Mzambia wa Simba, Clatous Chama yaliwafanya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenda mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 2-1.

Chama alifunga bao la kwanza dakika ya tano ya mchezo akimalizia pasi iliyopigwa na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na kuifanya Lipuli iliyoanza mpira kwa kukamia kujipanga upya.

Lipuli ilitulia na kufanya mashambulizi ya kushtukiza kwenye lango la Simba na ilipofika dakika ya 18 ilifanikiwa kusawazisha kupitia kwa Paul Nonga ambaye alimalizia vema mpira wa kugongeana waliyocheza langoni mwa Simba.

Simba ilitulia na kuanza kujipanga upya na hatimaye dakika ya 44 kiungo wake Muzamiru Yassin alifanyiwa faulo ambayo ilizaa bao la pili lililofungwa na Chama aliyepiga mpira uliotinga moja kwa moja wavuni.

Mshambuliaji aliyeko katika kasi kutoka Rwanda, Meddie Kagere alifunga bao la tatu akiwahi mpira aliotanguliziwa huku kipa Mohamed Yusuph akiwa ametoka katika eneo lake dakika ya 57.

Baada ya bao hilo Lipuli walionekana kushindwa kuwa na nidhamu na matokeo yake beki wake, Paul Ngalema alionyeshwa kadi nyekundu na refa, Florentina Zablon kutoka Dodoma kutokana na kumpiga kiwiko John Bocco.

Hata hivyo, wachezaji wa Simba walipoteza nafasi mbalimbali za kushambulia baada ya mipira mirefu waliyokuwa wakiipiga nje ya "vipimo sahihi" na kumruhusu kipa wa Lipuli, Mohamed kuidaka kirahisi au kupotea kwa kutoka nje.

Safu ya kiungo ya Lipuli ambayo ilikuwa chini ya Seif Karihe, ilijitahidi kuonyesha uhai lakini mabeki wa Simba, Paschal Wawa, Yusuph Mlipili na Mohamed Hussein ilijitahidi kuokoa mashambulizi yao.

# Yanga yaitangazia hatari Alliance

**Na Faustine Felician**

KIKOSI cha Yanga kinaondoka kesho kwa ndege kwenda Mwanza tayari kwa mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Alliance FC, huku kocha Mwinyi Zahera akiwatangazia hali ya hatari wapinzani wao hao.

Zahera, alisema ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wao uliopita wa Kombe la FA dhidi ya Namungo FC ya mkoani Lindi umewapa morali ya juu wachezaji wake na wanaifuata Alliance huku wakiwa na uhakika wa ushindi.

"Tunaondoka Alhamisi (kesho), tunafahamu Alliance ni timu nzuri na watakuwa wazuri zaidi wakicheza kwao, tunawafuata kwa lengo moja tu la ushindi, tutacheza soka letu na kupambana nao," alisema Zahera.

Alisema kwa sasa michezo yote ya Ligi Kuu ni migumu hasa kutokana na kila timu kukamia kupata ushindi kwenye mzunguko huu wa pili.

"Ligi ni ngumu sana, kila mchezo kwa sasa ni muhimu kwa sababu ukipoteza mchezo unampa nafasi mpinzani wako kuongeza pointi kitu ambacho kinaweza kikaleta shida baadaye kwenye maamuzi ya ubingwa," alisema Zahera.

Aidha, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kikosi cha timu hiyo kipo kwenye hali nzuri na hakuna majeruhi mpya mpaka kufikia jana.

"Tumeanza maandalizi ya safari, hakuna mchezaji majeruhi mpya, kila mmoja yupo vizuri na tunaendelea na maandalizi kuelekea kwenye mchezo wetu," alisema Saleh.

Kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza Oktoba 19, mwaka jana, katika Uwanja wa Taifa, Yanga ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Alliance.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >